

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Arobaini – Tarehe 8 Juni, 2020

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tukae. Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI-KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)

Na. 376

Halmashauri Nchini Kuwezesha Kukusanya Mapato

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwezesha Halmashauri za Wilaya kuimarisha uwezo wa kukusanya mapato ya kugharamia shughuli za maendeleo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha ukusanyaji mapato kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Serikali imeanzisha Mfumo wa ukusanyaji Mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (*Local Government Revenue Collection Information System -LGRCIS*) ambao ni Mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia za kielektroniki unaotumia vifaa vijulikanavyo kwa jina la *POS* mashine (*point of sale-machine*).

Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali ilinunua na kugawa mashine za kukusanya mapato (*POS*), 7,227 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.685 na kuzigawa kwenye halmashauri nchini hasa zenyeye uwezo mdogo wa kifedha. Serikali inaendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji na udhibiti wa mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuziwezesha halmashauri kuongeza uwezo wa kukusanya na kudhibiti mapato.

Na. 377

Ujenzi wa Kituo cha Afya Makuyuni

MHE. JULIUS K. LAIZER aliuliza:-

Akiwa katika ziara mwaka jana kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Jafo alitembelea Kituo cha Afya Makuyuni kinachojengwa kwa nguvu za wananchi na kuahidi kuwa Serikali itatoa fedha za kumalizia ili kuunga mkono juhudii za wananchi.

(a) Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kumalizia ujenzi wa Kituo cha Afya Makuyuni, Lemoot na Naalaransi ambavyo wananchi wameonyesha juhudii?

(b) Je, ni nini kauli ya Serikali katika kuunga mkono juhudii za wananchi waliojenga Zahanati na Vituo vya Afya

kote nchini hasa kwa kuwa ni sera ya Serikali ya kujenga kituo kwa kila kata na zahanati kila kijiji?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA aliijibu:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha huduma za Afya Wilaya ya Monduli, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Monduli kiasi cha Shilingi milioni 800 kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa Vituo vya Afya Monduli na Mto wa Mbu, ujenzi huo umekamilika.

Vilevile katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga kiasi cha Shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha maboma kwenye Vituo ya Afya vya Lemoot, Naalarami na Lashaine.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga kiasi cha Shilingi billioni 27.75 kwa ajili ya kukamilisha maboma matatu ya Zahanati kwa kila Halmashauri nchini ili kuunga mkono jitihada za wananchi.

Na. 378

Wahitimu wa Ualimu ambao Bado Hawajapata Ajira

MHE. MARY P. CHATANDA aliuliza:-

Wahitimu wa kada ya walimu wa masomo ya *Arts* ngazi ya Stashahada na Shahada kuanzia mwaka 2015 hadi leo hawajapata ajira.

Je, nini hatima ya Walimu wa kada hizi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Korogwe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Utumishi wa Umma, nafasi za ajira za watumishi wa kada mbalimbali wakiwemo Walimu hutengwa kulingana na vipaumbele vya Serikali. Katika miaka ya nyuma ambapo Watumishi wa Umma wenye sifa walikuwa wachache, Serikali ilioa ajira za moja kwa moja kutoka vyuoni (*direct entry*) kwa kada zote.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwa na watumishi wa kutosha na ili kupata watumishi wenye sifa, weledi na uadilifu, Serikali ilibadilisha utaratibu wa ajira za moja kwa moja na kuanza kutoa ajira kwa njia ya ushindani kupitia usaili wa watumishi wa kada mbalimbali isipokuwa Walimu na Watumishi wa Kada za Afya.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni, Utumishi wa Umma umekabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa baadhi ya kada katika soko la ajira hususan kwa baadhi ya kada za Afya na Elimu (Masomo ya Sayansi). Kutokana na changamoto hii, Serikali imeweka kipaumbele cha ajira mpya kwa Walimu wa Masomo ya Sayansi, Hisabati, Kilimo, Biashara na Elimu Maalum pamoja na fani ya Fundi Sanifu wa Maabara za Shule.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwepo kwa Walimu ziada wa Masomo ya Sanaa (*Arts*) katika Shule za Sekondari hususan katika maeneo ya mijini, Serikali iliwaagiza Waajiri katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya Walimu na kuhamishia Walimu wa ziada katika Shule za Msingi na Maeneo yenye upungufu mkubwa wa Walimu ili kuweka uwiano mzuri wa Walimu kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itaajiri Walimu wa Masomo ya Sanaa (*Arts*) pale idadi ya Walimu wa Masomo ya Sayansi, Hisabati, Kilimo, Biashara, Elimu Maalum na Mafundi Sanifu wa Maabara za Shule katika shule za sekondari itakaporidhisha. Aidha, wakati Serikali ikiendelea na mchakato wa kujaza nafasi za Walimu wa Sayansi, wahitimu wa kada ya Ualimu

wa Masomo ya Sanaa wanahimizwa kutafuta ajira katika Taasisi nyingine za umma na shule binafsi.

Na. 379

Taratibu Zinazotumika Kufungua Balozi Mpya

MHE. ALLY SALEH ALLY aliuliza:-

Katika dunia inayokua kwa mfungamano na uhusiano wa kiuchumi na kidiplomasia ni wazi kuwa suala la kufungua balozi mpya huwa lazima kadri ya hali inavyohitaji:-

- (a) Je, ni taratibu gani zinatumika kufanya maamuzi ya idadi ya balozi duniani kwa wakati mmoja?
- (b) Je, mgawanyiko wa balozi kwa kila bara hufanywa kwa misingi ipi?
- (c) Je, kuna dira inayoonyesha mipango ya ufunguzi wa balozi mpya?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa nchi kufungua Ubalozi katika nchi fulani hutegemeana na maslahi ya Taifa katika masuala ya kisiasa, kiuchumi, kidiplomasia, kijamii, kiulinzi, na kadhalika. Maslahi hayo na uwezo wa nchi kifedha ndiyo huongoza nchi yetu kufungua Balozi katika nchi/ukanda upi na kwa wakati gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajumla ya Balozi 43, Balozi nane kati ya hizo (Qatar, Cuba, Jamhuri ya Korea, Israel, Algeria, Namibia, Sudan na Uturuki) zimefunguliwa katika kipindi cha

Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Serikali inaendelea kufanya tathmini mbalimbali kila mara ili kubainisha maeneo/nchi ambazo tunahitaji kufungua Ubalozi kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yanayotokea ndani na nje ya nchi.

Na. 380

Ukosefu wa Watumishi na Vitendea Kazi Idara ya Maji Kibiti

MHE. ALLY S. UNGANDO aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti ina upungufu mkubwa wa watumishi wa Idara ya Maji na vitendea kazi kama gari na pikipiki hivyo kusababisha watumishi kushindwa kutimiza majukumu yao kwa tija:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizosababisha kushindwa kupeleka Watumishi wa kutosha?

(b) Je, ni lini changamoto hizo zitapatiwa ufumbuzi?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti iligawanywa tarehe 1 Septemba, 2016 na kuzaliwa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti. Mgawawanyo huo ulihusisha Rasilimali Watu na vifaa, hivyo Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti kupitia Idara ya Maji ilipata mgao wa jumla ya Watumishi wanne (4), (Wahandisi wawili (2) na Fundi Sanifu wawili (2)) pikipiki moja (1) na baadhi ya vitendea kazi vidogovidogo. Hivyo kuwa na upungufu wa Wahandisi (2) na Fundi Sanifu kumi na mbili (12) na vitendea kazi ikiwemo gari na pikipiki.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuanzishwa kwa *RUWASA* Watumishi wote na vitendea kazi vyote vilivyokuwa vinatumika katika Idara za Maji za Halmashauri zilihamishiwa katika Ofisi za *RUWASA* Wilaya. Serikali kuitia Wizara ya Maji katika kuhakikisha watumishi wa kutosha na vifaa vinapatikana imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ambapo mpaka sasa Ofisi za *RUWASA*-Kibiti zimepokea jumla ya watumishi wanne (4) na kufanya jumla ya watumishi kufikia nane (8) wakiwemo Wahandisi (2) na Fundi Sanifu wawili (2). Aidha, kuitia bajeti ya mwaka 2020/2021 *RUWASA*-Kibiti imepanga kununua pikipiki mbili (2) kwa ajili ya ufuatililaji wa miradi ya maji. Vilevile, utaratibu wa kununua magari na kuhakikisha kila Wilaya ina gari na usimamizi unafanyika.

Na. 381

Kukarabati Bwawa la Kijiji cha Mwamihanza – Maswa

MHE. MASHIMBA M. NDAKI aliuliza:-

Bwawa la kijiji cha Mwamihana linahudumia Vijiji vya Mwamihanza, Kidema na Ngonwa lakini linaingiza maji kidogo kwa sababu limejaa mchanga:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati bwawa hilo ili liendelee kuwapatia maji wananchi pamoja na mifugo yao?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto kubwa ya huduma ya maji inayowakabili wananchi wa Vijiji vya Mwamihanza, Ngonwa na Kidema. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali katika mwaka huu wa fedha 2019/2020 inatekeleza Mradi wa Maji Ngonwa – Kidema kuitia Programu ya malipo kwa matokeo

(P4R) ambapo mradi huo unakadiriwa kugharimu fedha kiasi cha Shilingi milioni 320. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha wananchi wa Ngonwa na Kidema wapatao 4,351 kunufaika na huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendelea na juhudzi za kutatua tatizo la maji katika vijiji hivyo kikiwemo Kijiji cha Mwamihanza, Serikali imepanga kukarabati Bwawa la Mwamihanza katika bajeti ya mwaka 2020/2021.

Na. 382

Tatizo la Kukatika kwa Umeme – Ngara

MHE. ALEX R. GASHAZA aliuliza:-

Tangu Wilaya ya Ngara iunganishwe kwenye umeme wa *Grid* ya Taifa mapema mwaka 2017 kumekuwepo na tatizo kubwa la kukatika ovyo kwa umeme na wakati mwingine kuwa na msongo mdogo na hivyo kutokidhi mahitaji.

Je, ni lini tatizo hili litaisha?

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa, Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kukatika kwa umeme katika Wilaya ya Ngara hususan katika kipindi cha nyuma kulitokana na changamoto mbalimbali ikiwemo kuchakaa kwa miundombinu ya umeme tokea Chato hadi Ngara kupitia Biharamulo; wananchi kuchoma moto mapori kwa lengo la kupata malisho mapya na hivyo kusababisha nguzo kuungua na pia umbali wa laini ya msongo wa kilovoti 33 kutoka Geita kupitia Wilaya ya Chato, Biharamulo hadi Ngara na kusababisha umeme unaofika Wilayani Ngara kuwa mdogo.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) katika kutatua tatizo hilo imefanya yafuatayo:-

(1) Kufunga kifaa cha kuongeza nguvu ya umeme (*Automatic Voltage Regulator - AVR*) chenye uwezo wa 3MVA katika eneo la Nyakaura;

(2) Kufanya matengenezo ya miundombinu ya umeme ikiwemo kazi ya kubadilisha nguzo pamoja na vikombe chakavu;

(3) Kufunga kifaa kinachoitwa *Capacitor bank* katika Wilaya ya Biharamulo. Kifaa hiki kinasaidia kuongeza nguvu ya umeme katika Wilaya za Biharamulo na Ngara; na

(4) Kuendelea kufanya maboresho ya miundombinu ya umeme katika maeneo ya Biharamulo hadi Ngara pamoja na kusafisha njia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hali ya upatikanaji wa umeme katika Wilaya ya Ngara imezidi kuimarika ikilinganishwa na kipindi cha nyuma kutokana na *TANESCO* kuendelea na maboresho mbalimbali ya miundombinu Pamoja na usafishaji wa njia ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme unaotumika Ngara unatoka katika *feeder* ya Nyakato-Mwanza kupitia Sengerema, Geita hadi Ngara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Mkoani Geita kupitia mradi wa Bulyahulu-Geita kutawezesha kuongeza nguvu ya umeme unaosafirishwa kwenda Ngara na hivyo kumaliza tatizo hilo.

Na. 383

Fidia kwa Wananchi Waliopisha Nguzo za Umeme Kata ya Njia Nne – Mkuranga

MHE. RUTH H. MOLLEL aliuliza:-

Wananchi wa Kata ya Njia Nne, Wilayani Mkuranga walitoa mashamba yao kwa ajili ya kupisha nguzo za umeme na kuahidiwa kulipwa fidia.

Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi na wajibu wake wa kuwalipa wananchi hao fidia?

WAZIRI WA NISHATI alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) inatekeleza mradi wa kujenga njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 400 kutoka Somanga Fungu hadi Kinyerezi Dar es Salaam. Njia hii inapita katika Wilaya za Kilwa, Rufiji, Kibiti, Mkuranga, Temeke na Ilala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandalizi ya ujenzi na kupata ushoroba (*way leave*), jumla ya wananchi 3,901 wanatakiwa kupisha njia ya ujenzi wa mradi huo na hivyo kustahili kulipwa fidia ya Shilingi 69.1. Serikali kupitia *TANESCO* illanza kulipa fidia kwa wananchi hao. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 jumla ya shilingi bilioni 59.7 zimelipwa kwa wananchi 3,347. Malipo ya shilingi bilioni 9.4 kwa wananchi 554 yanaendelea kufanyiwa kazi ili nayo yalipwe kadri inavyostahili mara baada ya maandalizi hayo kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali kupitia *TANESCO* inaendelea na maandalizi ya malipo kwa wananchi wote waliobaki.

Na. 384

Tume ya Maendeleo ya Ushirika

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

Lengo la kuanzisha Vyama vya Ushirika nchini (*AMCOS*) lilikuwa kuwakusanya pamoja wakulima na kuwa na nguvu ya kusimamia malipo mazuri toka kwa wanunuzi, lengo hili limekuwa kinyume na matarajio ya wakulima ambapo wahusika wa *AMCOS* nyingi wamekuwa wezi wa fedha za wakulima kwa kutowalipa na kuwaibia kupitia upimaji wa kilo hususan kwenye pamba.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo hili kwa wakulima wa pamba nchini?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia Vyama vya Ushirika nchini kwa kufuata kanuni na taratibu kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 kwa lengo la kuimarisha ufanisi na kupunguza dosari mbalimbali za kiutendaji ikiwa ni pamoja na wizi na matumizi mabaya ya fedha za wakulima.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Mara una jumla ya Vyama vya Ushirika vya Msingi (*AMCOS*) 559; kati ya vyama hivyo 133 sawa na asilimia 23.8 vimekaguliwa. Ukaguzi uliofanywa kwenye vyama hivyo vya mazao (*AMCOS*) katika mkoa huo umebaini dosari kadhaa katika vyama hivyo ikiwemo uandishi mbovu wa vitabu, ubadhirifu wa fedha wa jumla ya shilingi milioni 47.1 na hivyo wakulima 103 kutokulipwa stahili zao. Kwa upande wa Wilaya ya Bunda pekee zipo jumla ya *AMCOS* 119 ambapo *AMCOS* 21 sawa na asilimia 17.65 zimekaguliwa. Aidha, Wilaya ya Bunda Vijijiini kumebainika upungufu wa fedha kiasi cha shilingi milioni 45 na kesi tatu (3) zipo mahakamani ili wote watakaobainika kuhusika wachukuliwe hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuibiwa kwa wakulima kupitia mizani, Serikali kupitia Wakala wa Vipimo (*Weight and*

*Measures Agency-WMA) hufanya ukaguzi kila mwaka kabla ya msimu kuanza ili kuhakiki ubora wa mizani hizo. Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi ya Pamba Tanzania wanaendelea kuhakikisha kwamba mizani zinazotumika zimehakikiwa na kuwekewa alama maalum (*seal*) ili kuzuia kuchezewa kwa lengo la kumuibia mkulima. Aidha, Serikali imeelekeza Kampuni zinazonunua pamba kuwalipa wakulima fedha za mauzo ya pamba kupitia akaunti zao za benki na sio kupitia *AMCOS*.*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria wale wote watakaobainika kuhusika katika wizi wa aina yoyote ikiwa ni pamoja na kuwaibia wakulima. Vilevile Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaendelea kuwabana viongozi na watendaji wa Vyama vyta Ushirika kwa kutoa adhabu kali kwa wahusika wa ubadhirifu wa fedha na mali za umma pamoja na kutoa mafunzo rejea mara kwa mara ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Na. 385

Mpango wa Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Suguti

MHE. ESTER A. BULAYA aliuliza:-

Serikali kupitia Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Ziwa ilipima na kuandaa michoro ya ujenzi wa bwawa la umwagiliaji kwenye Mto Suguti eneo la Kijiji cha Kiwasi, sasa ni zaidi ya miaka mitano(5) hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

Je, ni lini Serikali itafufua na kuwapa imani wananchi kuwa Serikali inatoa ahadi na kuzitekeleza kwa kujenga bwawa hilo kwa ajili ya umwagiliaji?

WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amosi Bulaya, Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali kupitia Ofisi ya Umwagiliaji ya Kanda ya Mwanza ilifanya tathmini ya awali (*preliminary design*) na kupata michoro ya awali na kubaini uwezekano wa kujenga bwawa lenye uwezo wa kuhifadhi maji kiasi cha meta za ujazo milioni sita. Aidha, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imewasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu; Sera, Uratibu na Uwekezaji andiko lenye jumla ya Sh. 271,889,601,517.71 kwa ajili ya mapitio na kuwasilishwa kwa wabia wa maendeleo ili kuweza kutelekeza ujenzi na ukarabati wa mabwawa ya umwagiliaji katika mikoa kame ya Tanzania ikiwemo Bunda ambapo kati ya hizo Sh.3,060,000,000.00 ni kwa ajili ya kufanya upembuzi wa kina pamoja na ujenzi wa bwawa la umwagiliaji katika bonde la mto Suguti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara fedha hizo zitakapopatikana Serikali itaanza kutekeleza upembuzi wa kina na ujenzi wa bwawa hilli utaanza mara moja. Aidha, Serikali inaendelea na juhudzi za kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza miradi ya umwagiliaji nchini ikiwemo Mradi huu wa Bwala la umwagiliaji katika Bonde la Mto Suguti.

SPIKA: Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

MAAZIMIO YA BUNGE

**Azimio la Bunge la Kuitaka Serikali Kutobadili Uamuzi wa Jiji
la Dodoma Kuwa Makao Makuu ya Nchi na Shughuli za
Serikali**

na

**Azimio la Bunge la Kumpongeza Spika wa Bunge la
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Mafanikio ya
Bunge la Kumi na Moja**

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimuitem
Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula ili awasilishe

Maelezo ya Azimio pamoja na Azimio husika. Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba sasa niwasilishe Azimio la Bunge la kuitaka Serikali kutobadili Uaamuzi wa Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi na Shughuli za Serikali, kwa mujibu wa Kanuni ya 54 (1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kipekee kabisa kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Azimio la Bunge Kuitaka Serikali kutobadili Uamuzi wa Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi na Shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu zinaonesha kuwa mara baada ya Uhuru wa Nchi yetu, nje na ndani ya Bunge, yalijitokeza mawazo ya kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi.

Aidha, mwanzoni mwa miaka ya 1970 Serikali ilianzisha mchakato kwa kuwashirikisha wananchi kupendelekeza mkoaa ambao utakuwa Makao Makuu ya nchi. Matokeo ya ushirikishwaji huo, Wananchi wengi waliunga mkono wazo la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi. Mwaka 1973 Rais wa Kwanza wa Tanzania na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliutangaza Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine uamuzi wa kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ulitokana na ukweli kwamba Dodoma ni eneo la kimkakati katika masuala ya ulinzi na usalama, ipo katikati ya nchi na Mikoa mingine Kijiografia na imewezesha huduma kusogezwa karibu na wananchi hivyo kurahisisha utawanyaji wa maendeleo nchini. Aidha, Makao Makuu kuwa Dodoma kunaleta ufanisi na tija katika uendeshaji wa shughuli za Serikali na kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa uamuzi huo umekuwa ukifanyika hatua kwa hatua ambapo awali wananchi katika Mikoa mbalimbali walitoa michango ya hali na mali katika kuwezesha ujenzi wa Makao Makuu. Sehemu ya michango hii iliwezesha kuanzisha ujenzi wa Jengo la Mikutano la Chimwaga lililotanguliwa na uwepo wa Ikulu ya Chamwino. Jengo hili awali lilikuwa limekusudiwa kutumika kwa ajili ya Mikutano ya Bunge japo matumizi yalibadilishwa. Pia kwa vipindi mbalimbali hatua ziliendelea kuchukuliwa, kama vile kuandaa *Master Plan* ya Mji wa Dodoma na kutenga eneo maalum kwa ajili ya Mji wa Serikali. Kuhamisha Makao Makuu ya Wizara kadhaa kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, kuhamisha Makao Makuu ya Bunge Dodoma, ujenzi wa Ukumbi mkubwa wa Bunge na Ofisi zake pamoja na ujenzi wa Chuo Kikuu kikubwa zaidi nchini cha Dodoma (UDOM).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hitimisho la mchakato wa kuhamisha Makao Makuu ya nchi na shughuli za Serikali kuja Dodoma, Mji wa Dodoma umepandishwa hadhi na kuwa Jiji na Sheria ya kulitambua rasmi Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi imetungwa [*The Dodoma Capital City (Declaration) Act, 2018*]. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, hadi sasa Viongozi Wakuu wa Serikali Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri na Watumishi wengine wa Serikali tayari wamehamia Dodoma. Vilevile, Wizara zote za Serikali tayari zimeshahamia Dodoma, Ofisi na Taasisi mbalimbali za Umma pamoja na Mashirika ya Kimataifa zimepewa maeneo na zinaendelea na ujenzi wa majengo yao hapa Dodoma, kwa mfano Uhamiaji, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (*NEC*), Jeshi la Magereza, Jeshi la Wananchi, Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Ofisi zingine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua hii ya Dodoma kuwa Jiji, kutungwa kwa Sheria ya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi, Viongozi Wakuu wa Serikali na Watumishi pamoja na Taasisi za Serikali na za Kimataifa kuhamia

Dodoma na kuanza ujenzi wa Makao yao hapa Dodoma, inaonyesha kwamba tayari mchakato wa kuhamishia shughuli za Serikali kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nisome Azimio la Bunge la kuitaka Serikali kutobadili uamuzi wa Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi na shughuli za Serikali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi na shughuli za Serikali ni uamuzi wa Wananchi wengi, uamuzi ambao ulisababisha mwaka 1973 Rais wa kwanza wa Tanzania na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kuutangaza Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi na shughuli za Serikali;

Kwa kuwa, ni ukweli kwamba Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi na shughuli za Serikali kuna faida kubwa kwa wananchi na Serikali kwa ujumla kwani Dodoma ipo katika eneo la kimkakati kwa masuala ya ulinzi na usalama, ipo katikati ya nchi na mikoa mingine Kijiografia. Inawezesha huduma kusogezwa karibu na wananchi na hivyo kurahisisha utawanyaji wa maendeleo nchini na vilevile Makao Makuu kuwa Dodoma kunaleta ufanisi na tija katika uendeshaji wa shughuli za Serikali na kupunguza gharama za uendeshaji;

Kwa kuwa, utekelezaji wa uamuzi wa kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu na Shughuli za Serikali umekuwa ukifanyika hatua kwa hatua ambapo awali wananchi katika Mikoa mbalimbali walitoa michango ya hali na mali katika kuwezesha ujenzi wa Makao Makuu. Sehemu ya michango hii iliwezesha kuanza ujenzi wa Jengo la Mikutano la Chimwaga ambalo lilikusudiwa kutumika kwa ajili ya Mikutano ya Bunge lilitanguliwa na uwepo wa lkulu ya Chamwino;

Kwa kuwa, kwa vipindi mbalimbali hatua ziliendelea kuchukuliwa, kama vile kuandaa *Master Plan* ya Mji wa Dodoma na kutenga eneo maalum kwa ajili ya Mji wa Serikali,

kuhamisha Makao Makuu ya Wizara kadhaa kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, kuhamishia Makao Makuu ya Bunge Dodoma, ujenzi wa ukumbi mkubwa wa Bunge na Ofisi zake pamoja na ujenzi wa Chuo Kikuu kikubwa zaidi nchini cha Dodoma (UDOM);

Na kwa kuwa, mchakato wa kuhamisha Makao Makuu ya nchi na shughuli za Serikali kuja Dodoma umehitimishwa kwa Mji wa Dodoma kupandishwa hadhi na kuwa Jiji, kutungwa kwa Sheria ya kilitambua rasmi Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi [*The Dodoma Capital City (Declaration) Act, 2018*] vilevile hadi sasa Viongozi Wakuu wa Serikali akiwemo Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri na Watumishi wengine wa Serikali tayari wamekwishahamia Dodoma;

Na kwa kuwa, Wizara zote za Serikali tayari zimeshahamia Dodoma ikwemo Ofisi na Taasisi mbalimbali za Umma pamoja na Mashirika ya Kimataifa na zimepewa maeneo na zinaendelea na ujenzi wa majengo yao hapa Dodoma;

Na kwa kuwa, ni kweli kwamba kwa hatua hii ya Dodoma kuwa Jiji, kutungwa kwa Sheria ya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi, Viongozi Wakuu wa Serikali na Watumishi pamoja na Taasisi za Serikali na za Kimataifa kuhamia Dodoma na kuanza ujenzi wa Makao yao hapa Dodoma, inaonyesha kwamba tayari mchakato wa kuhamishia shughuli za Serikali kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma umekamilika;

Kwa hiyo basi, kwa kuwa ni wazi kuwa tayari shughuli za Serikali zinafanyika Dodoma na ni kweli kwamba Dodoma ndio Makao Makuu ya nchi yetu, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo tarehe 08 Juni, 2020 kwa kauli moja linaazimia kama ifuatavyo:-

(a) Kuitaka Serikali, Mamlaka au mtu yejote kutotengua uamuzi wa Wananchi wa kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi;

(b) Kuitaka Serikali na Taasisi zake kutohamisha kwa namna yoyote shughuli za Serikali kutoka Dodoma kwenda sehemu nyingine yoyote nchini; na

(c) Kuitaka Serikali kuhakikisha kwamba inaendelea kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuboresha na kuendeleza miundombinu ya Jiji la Dodoma wakati wote ili kulifanya kuwa na mandhari inayoendana na hadhi ya Makao Makuu ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba kutoa Hoja. (*Makofi*)

MHE. ANNE KILANGO MALECELÀ: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu. Sasa nimuite Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga ambaye nae atawasilisha maelezo ya Azimio pamoja na yale ambayo yanahusiana na Azimio hili ambalo kwenye Taarifa zetu linaonekana B.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu Kanuni ya 54(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016, natoa hoja kwamba Bunge lako tukufu lijadili na kupidisha Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mbunge), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha Bunge la Kumi na Moja kupata mafanikio tunayojivunia sisi sote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii adhimu ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu hoja hii inayotambua weledi, maarifa, ubunifu, uzalendo na juhudhi zake zilizopelekeea Bunge la Kumi na Moja kupata mafanikio tunayojivunia sisi sote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nitumie dakika moja au dakika mbili/tatu hivi kumpongeza

Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano aliotupatia sisi Wabunge katika kutekeleza majukumu yetu, lakini pia kwa uongozi wake thabiti na wenye maono ya mbali, uliowezesha kupata mafanikio tunayojivunia kama nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kwamba huwezi kuelezea mafanikio tuliyoapata katika nchi bila kumtaja Jemedari wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini ni ukweli pia usiofichika kwamba huwezi kuzungumzia mafanikio hayo bila kutaja mchango wa Bunge lako tukufu. Hali kadhalika, huwezi kutaja mafanikio hayo bila kutaja jina la Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mbunge), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema nimewiwa kuwasilisha Azimio hili kwasababu kubwa moja. Sababu yenyewe ni kutambua mchango wa Mheshimiwa Spika katika maendeleo ya Taifa hili yaliyopatikana katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano hatuwezi kuacha kuzungumzia mchango wa Mheshimiwa Spika wa kuliongoza Bunge hili kuitisha Miswada na Sheria mbalimbali na Bajeti za Serikali zilizopelekea kupata mafanikio tunayojivunia leo hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nani asiyejua kwamba bajeti za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa ya *Standard Gauge* kutoka Dar es salaam mpaka hapa Dodoma zilipitishwa na Bunge lako tukufu. Nani asiyejua bajeti ya kujenga Vituo vya Afya kila Kata na Hospitali za Wilaya 67 nchi nzima zilipitishwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nani asiyejua kama bajeti ya mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme wa

zaidi ya *megawatts* 2,115 la Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ilipitishwa na Bunge lako tukufu. Kama vile haitoshi nani asiyejua bajeti za ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya barabara, maji, bandari, meli, madarasa na kadhalika zilipitishwa na Bunge lako tukufu. Lakini kubwa zaidi nani asiyejua kuwa sheria ya kuitamka Dodoma kuwa makuu ya nchi pamoja na bajeti ya kugharamia ujenzi wa miundombinu na ofisi mbalimbali za Serikali na kuwezesha Serikali kuhamia Makao Makuu Dodoma ilipitishwa na Bunge lako tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba Bunge lako tukufu limefanya mambo mengi ya kujivunia katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano. Bila utayari na ushirikiano wa Bunge lako tukufu kwa Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pengine mafanikio tunayojivunia leo ingekuwa vigumu kuyafanikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya kufanikisha matokeo hayo ya Serikali ya Awamu ya Tano, pia Spika amekuwa kiongozi mwenye maono, ubunifu, weledi, msimamo na ushawishi wa hali ya juu katika kuongoza utekelezaji wa Bunge letu tukufu. Katika kipindi chake tumeshuhudia mabadiliko mengi ya kifalsafa, kimiundombinu na kiteknolojia ambayo yameweza Bunge la Kumi na Moja kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila Mheshimiwa Spika Ndugai na alichokifanya na Corona hii, wote na sisi tunetoka nje kama walivyotoka wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo uliyoyafanya katika kipindi chako ni mengi sana, lakini naomba nitaje machache ambayo yamenifanya niwiwe kuwasilisha Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, Kubuni wazo la Bunge Mtandao (*e-Parliament*). Ni katika kipindi chako Wabunge tumeshuhudia mabadiliko makubwa ya

uendeshaji wa Bunge letu tukufu. Ametutoa kwenye ujima wa Bunge analogia (*analog*) na kutuleta katika utandawazi wa Bunge Mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge kupata vishkwambi, najua wengi hilo hawataelewa, lakini mlichoshikilia ambazo zinaitwa *tablet* ndiyo vishkwambi hivyo ambavyo tunatumia katika shughuli mballimbali za Kibunge ni mchango wake pia. Jambo la kushangaza na la kujivunia zaidi ni kwamba mfumo wa Bunge Mtandao, yaani *e-Parliament*, umebuniwa na watumishi wa Bunge na kupata msaada kutoka kwa Mamlaka za Serikali Mtandao (*e-Government*). *This is ours. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba matumizi ya Bunge Mtandao yatapunguza sana gharama za matumizi ya karatasi na wino wa kuchapisha nyaraka mballimbali za Bunge zinazowasilishwa na Ofisi za Bunge, Wizara, Taasisi mballimbali za Serikali kwa ajili ya shughuli za Bunge. Mathalani nimeelezwa kuwa Ofisi ya Bunge inatarajia kuokoa zaidi ya shilingi bilioni nne kwa mwaka baada ya kuanza kutumia Bunge Mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nimeelezwa kwamba inakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi bilioni 100 zinatarajiwu kuokolewa kutoka kwenye matumizi ya Wizara na Taasisi mballimbali za Serikali kutokana na matumizi ya Bunge Mtandao ambapo sasa Wizara na Taasisi za Serikali zimepunguza matumizi hayo kwa zaidi ya asilimia 90 ya uzalishaji wa nyaraka zinazotakiwa kuwasilishwa Bungeni, badala yake wanawasilisha nakala mango yaani *hard copy*, chache kwa ajili kumbukumbu na nakala tete (*soft copy*) kwa ajili ya matumizi ya Waheshimiwa Wabunge na Sekretarieti ya Bunge. Hata miti sasa hatutaikata sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kupunguza matumizi yasiyo ya lazima. Katika kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu kutimiza ndoto yake ya kuleta maendeleo ya kweli katika nchi yetu, Bunge lako Tukufu likiongozwa na Mheshimiwa Spika lilikubali kubana matumizi yake kwa

kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kama vile kupunguza safari zisizo za lazima nje ya nchi. Kumbuka huu ni mhimili unaojitegemea na kiongozi wake ni Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuthibitisha hilo, nimefanya utafiti mdogo tu na kubaini kuwa bajeti ya mwisho ya Bunge la Kumi yaani bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 ilikuwa takribani shilingi bilioni 173.77 wakati bajeti ya mwisho ya Bunge la Kumi na Moja unaloliongoza wewe Mheshimiwa Spika, yaani bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 ni shilingi bilioni 121.79. Kwa takwimu hizo utagundua kwamba Bunge lako Tukufu limeweza kubana matumizi na kuokoa fedha za Umma takribani shilingi bilioni 51.98 na hii ni kila mwaka ambapo zimekwenda kutumika kugharamia miradi ya maendeleo inayotekelizwa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, kuongezeka kwa ufanisi na kumbi za mikutano. Kabla ya Bunge hili la Kumi na Moja, Ofisi ya Bunge imekuwa ikitabiliwa na changamoto ya uhaba wa kumbi za kufanya vikao vya Kamati na vyumba vya Ofisi za Watumishi wa Ofisi ya Bunge. Kwa sasa changamoto hiyo imekuwa historia kwa sababu ubunifu na jitihada za Mheshimiwa Spika na Ofisi ya Bunge kukamilisha ujenzi wa Jengo la Utawala, yaani ile *Annex* ambalo lina kumbi tisa za mikutano zinazotumiwa na Kamati za Kudumu za Bunge, vyumba vya ofisi vinavyotumiwa na Watumishi wa Idara ya Kamati za Bunge, Sehemu ya Milki na Majengo na Sehemu ya Uchapishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile jengo hilo lina sehemu ya kutolea huduma ya chakula (*Canteen*), huduma za kibenki Tawi la Benki ya *NMB* na *CRDB* yako pale; huduma za afya, Kituo cha Afya chetu cha Bunge kiko pale. Huduma hizo ni muhimu na zimerahisisha sana maisha ya Waheshimiwa Wabunge wanapokuwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika, umefanikisha kupatikana kwa kumbi nyingine mbili katika jengo la Msekwa, yaani Msekwa D na Msekwa C na kumbi mbili katika Jengo

Kuu la Utawala, yaani ukumbi Na. 9 na Na. 231. Aidha, tunaona kuna ujenzi unaoendelea katika jengo kuu la Utawala ambapo imeelezwa kuwa inaongezwa sakafu ya tano (*5th Floor*) ambapo itakuwa na Ukumbi mkubwa mmoja wenye uwezo wa kubeba watu 200 kwa wakati mmoja, kumbi ndogo nne na vyumba nya ofisi sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la kumbi za mikutano ndani ya maeneo ya Bunge limesaidia kuondoa kabisa gharama ambazo zilikuwa zinatumika kukodi kumbi za mikutano wakati wa vikao nya Kamati. Inakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi milioni 120 kila mwaka sawa na shilingi milioni 600 kwa miaka mitano zitaokolewa baada ya Bunge kuanza kutumia kumbi zilizopo katika majengo niliyoyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, maboresho ya miundombinu. Jambo lingine ambalo sisi kama Bunge tunajivunia ni maboresho ya miundombinu mbalimbali ya Ofisi ya Bunge. Katika kipindi cha Bunge la Kumi na Moja tumeshuhudia ujenzi wa *lift* katika jengo kuu la Utawala na jengo la *Utawala Annex*. Ujenzi wa *lift* hizo umeondoa adha ya Waheshimiwa Wabunge na kuwawezesha huduma za kiofisi kwa urahisi zaidi. Huko nyuma Mbunge alikuwa analazimika kupanda ngazi hadi ghorofa ya nne katika jengo la Utawala jambo ambalo lilikuwa ni adha kubwa kwa Wabunge na wageni wanaotembelea ofisi ya Bunge. Sasa aaah, mambo safi! Hakuna tena kupanda ngazi, ni mwendo wa kuteleza tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kulinda hadhi, staha na taswira ya Bunge. Naomba mnisikilize kwa makini. Bunge la Kumi na Moja ndiyo Bunge lenye idadi kubwa ya Waheshimiwa Wabunge vijana na Wabunge kutoka Vyama vya Upinzani kuliko kipindi chochote cha historia ya nchi yetu. Hivyo, kwa vyovypote vile uendeshaji wa Bunge lenye mchanganyiko wa namna hiyo unahitaji kiongozi shupavu, msimamo thabiti, hekima, busara, maono, usikivu na mwenye kufanya maamuzi magumu. Narudia hilo; "na mwenye kufanya maamuzi magumu." (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kumung'unya maneno, Kiongozi wa Bunge mwenye sifa hizo ni Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge na Spika wa Bunge hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ya Bunge la Kumi na Moja ni mengi sana, siwezi kuyasema yote. Hata hivyo, hatuwezi kuzungumzia hayo yote bila kutambua mchango wa wewe Mheshimiwa Naibu Spika. Naomba niseme hili neno msije mkaulizia *man; what man means? You are the right hand man*, Kiingereza kinalewaka, sasa msileté mambo ya jinsia tena hapa. (*Makofî/ Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa niwasilishe Azimio la Bunge la kumpongeza Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mafanikio ya Bunge hili la Kumi na Moja. Naomba yote ambayo nimeyaacha kuyasoma kwa sababu ya muda, yote yaingie kwenye *Hansard*.

KWA KUWA, Bunge chini ya uongozi wa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge, Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limetoa mchango mkubwa katika mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano;

NA KWA KUWA, Bunge la Kumi na Moja limeendeshwa kwa ubunifu na viwango vya hali ya juu ikiwa ni pamoja na kuongeza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano katika uendeshaji wa shughuli zake;

NA KWA KUWA, Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge, amechangia kubuni wazo la kubadilisha mfumo wa uendeshaji Bunge kutoka Bunge analogia (*analogy*) na kwenda kwenye mfumo wa Bunge Mtandao (*e-Parliament*);

NA KWA KUWA, mfumo huo utasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa Bunge na Serikali kwa zaidi ya shilingi billioni 100 kwa mwaka na kurahisisha uendeshaji wa Shughuli za Bunge;

NA KWA KUWA, katika kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu kutimiza ndoto yake ya kuleta maendeleo ya kweli katika nchi yetu, Bunge la Kumi na Moja likiongozwa na Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge, lilikubali kubana matumizi yake kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kama vile kupunguza safari zisizo za lazima nje ya nchi kwa Wabunge na Watumishi wa Bunge;

NA KWA KUWA, hatua hiyo imesaidia kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 50 kila mwaka fedha ambazo zimeekelezwa kwenye miradi ya maendeleo inayotekelawa na Serikali ya Awamu ya Tano;

NA KWA KUWA, Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Yustino Ndugai amechangia sana kukamilika kwa ujenzi wa Jengo la *Annex* na kuanzisha ujenzi wa sakafu ya tano (*5th Floor*) katika jengo kuu la Utawala hatua ambayo imesaldia kuongeza kumbi za mikutano ndani ya maeneo ya Bunge;

NA KWA KUWA, ongezeko la kumbi limesaidia kuokoa kabisa gharama ambazo zilikuwa zinatumika kukodi kumbi za mikutano wakati wa vikao vya Kamati;

NA KWA KUWA, inakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi milioni 120 kila mwaka sawa na shilingi milioni 600 kwa miaka mitano zimeokolewa baada ya Bunge kuanza kutumia kumbi zake zilizopo katika majengo niliyoyataja;

NA KWA KUWA, katika kipindi cha Bunge la Kumi na Moja tumeshuhudia ujenzi wa *lift* katika Jengo Kuu la Utawala na Jengo la *Utawala Annex* zimeondoa adha ya Waheshimiwa Wabunge na kuwawezesha kupata huduma za kiofisi kwa urahisi zaidi;

NA KWA KUWA, kwa kipindi chote Spika wa Bunge, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai amesimamia nidhamu na utulivu wa Bunge na kuhakikisha kuwa Bunge linatekeleza majukumu yake kwa kufuata demokrasia, uwazi na uzalendo kwa nchi yetu; (*Makof!*)

NA KWA KUWA, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai amefanikisha kulinda hadhi na heshima ya Bunge letu kwa wivu na kulifanya kubaki na hadhi linayostahili;

KWA HIYO BASI, katika kutambua jitihada, ubunifu, uzalendo na mchango wa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuliwezesha Bunge na Taifa kupata mafanikio niliyoyaeleza ikiwa ni pamoja na kubuni na kuanzisha mfumo wa Bunge Mtandao (*e-Parliament*), kufanikisha ujenzi wa Kumbi za Mikutano ya Kamati, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima kwa Bunge, kuboresha miundombinu kama vile kuweka *lift* katika majengo ya utawala na kulinda na kuhifadhi hadhi na heshima ya Bunge;

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkutano wake wa Kumi na Tisa, Kikao cha Arobaini cha Tarehe 8 Juni, 2020 linaazimia kumpongeza Spika Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge, kwa mchango wake katika mafanikio ya Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofii)

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Bunge hoja imeungwa mkono. Kwa hiyo, baada ya mawasilisho hayo ya Maazimio hayo mawili tutaendelea na uchangiaji, Ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge walioomba kuchangia kwenye hoja hii. Tutaanza na Mheshimiwa Adamson Emanuel Mwakasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni na Mheshimiwa Mwanne Mchemba ajiandae.

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika hizi haya maazimio mawili. Kwanza, nalipongeza Bunge lenyewe chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Spika kwa kuamua kuja na maazimio haya mawili, ni muhimu sana. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa jinsi alivyolishughulikia hili suala la kuhamishia Makao Makuu ya Serikali hapa Dodoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ni kitu kingine na utekelezaji ni kitu kingine. Makao Makuu ya Serikali kuhamia hapa Dodoma ilianza muda mrefu kama tulivuosomewa toka mwaka 1973, ndiyo Mheshimiwa Baba wa Taifa Hayati Julius Kambarage Nyerere alikuwa ametoa maamuzi ya kuhamia hapa, lakini ni Marais wengi wamepita katika kipindi cha miaka yote hiyo, siwabezi wale Marais lakini ukweli ni kwamba Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imeweza kukamilisha kuhamia Dodoma. Namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama ilivyosomwa kwenye taarifa, kuhamia Makao Makuu Dodoma kumerahisisha mambo mengi sana hasa katika utendaji wa shughuli za Kiserikali. Kuna neno moja pale tumelitumia kuitaka Serikali kutobadili uamuzi. Kuna siku moja ilitokea hoja hapa ya Mheshimiwa Mbunge mwenzetu ya kutaka Mheshimiwa Rais aongezewe kipindi, hapa ndipo naiona ile hoja pia kwamba ina mashiko. Maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, anaweza kuja ambaye hatumtaraji akabadilisha maamuzi haya na wakati hata mipango yenye mingine bado inaendelea kuimarisha Makao Makuu kuja Dodoma. Siyo vibaya, naendelea kusema kwamba unaposema Katiba ya Nchi, siyo Msahafu wala Biblia kwamba haibadilshwi. Kwa hiyo, bado pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais katika maeneo mengi amekuwa akitamka kwamba yeye hapendi kuongezewa kipindi, lakini naomba niseme kwamba kwa miradi ambayo ameianzisha, ameibuni na inaendelea, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakasaka, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mch. Msigwa.

T A A R I F A

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza mchangiaji, ameongea maneno ya hatari kidogo kwamba Katiba siyo Msahafu. Nilitaka nimwambie tunapoingia Bungeni kwa mara ya kwanza huwa tunaapa hapa kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nilitaka nimkumbushe hilo na siyo vinginevyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakasaka unaipokea taarifa hiyo?

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei kwa sababu ukweli unabaki kwamba Msahafu au Biblia huwezi kulinganisha na Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza hivyo kwa sababu unaweza ukaanza jambo, kwa mfano sasa hivi Mheshimiwa Rais ameanzisha miradi mingi sana ya maendeleo ambayo kwa vyovyyote vile katika miaka 10 haiwezi kumalizika. Anaweza akatokea mwagine akasimamisha mipango hiyo; hiyo ndiyo hoja, ingawa hatuombei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hiyo ndiyo hoja yangu. Naendelea kumpungeza Mheshimiwa Rais kwa hilo lakini na kwamba Serikali isije ikabadilisha mtazamo na sheria ambayo ilitungwa mwaka 2018 kutambua kwamba Dodoma ndiyo Makao Makuu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye Azimio la pili la Kumpungeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb) na ambaye ndiye kiongozi wetu wa huu muhimili; kwa maana kwamba yeche ndiye Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukakmbuka wakati tunaanza Bunge hili la 11, kama isingekuwa uimara wa Mheshimiwa Spika pamoja na ninyi mnaomsaidia leo hii ingefikia mahali Wabunge wengine wangeweza kupanda hata juu ya meza hizi; lakini sasa ukiangalia chini ya uongozi wa Mheshimiwa Spika, Job Ndugai Bunge sasa limetulia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Ndugai pamoja na wewe kwa kazi nzuri iliyofanyika. Hata leo unaona kidogo watu wanachomekea chomekeea maneno upande wa upinzani kwasababu wanaona Bunge linaelekea mwishoni; lakini pale mwanzoni walikuwepo mpaka ambao walikuwa wanajaribu na kuchana karatasi za Bunge leo wametulia; na haya yote ni kwasabbau ya uongozi imara wa Mheshimiwa Spika. Bunge sasa limetulia na kila mmoja anaona. Kile ambacho wananchi wametutuma sasa ndicho tunakifanya kwasababu hatukutumwa hapa ili tufanye vurugu, tumetumwa tuweze kuwawakilisha Wananchi wetu. Baada ya kusema hayo machache napenda kuunga mkono maazimio yote mawili. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nilikuwa nimetaja Mheshimiwa Raphael Chegeni atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Godbless Lemma ajiandae.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi hii. Mimi nami niungane na wenzangu wote waliosoma maazimio mawili pamoja na mchangiaji wa kwanza kujaribu kuelezea yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono maazimio yote mawili; la pili napenda nimuelezee Mheshimiwa Job Yustino Ndugai kwa kifupi sana, inawezekana baadhi yetu hamumfahamu vizuri jinsi alivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai ni mwanasayansi ambae amekamilika na amebobea, ni Mbunge wa Kongwa tangu mwaka 2000 mpaka sasa hivi,

alikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Malisili, amekuwa mwakilishi wa tawi letu la CPA (*Common Wealth Parliamentary Association*) kwa Tanzania katika *regional* ya Afrika kwa miaka mitano, amekuwa mchezaji wa mpira, beki namba mbili. Naomba niwakumbushe muelewe, huyu ndiye Job Ndugai. Alikuwa mwanamichezo mzuri sana, beki namba mbili; mimi nilikuwa forward namba tisa, kumpita ilikuwa ni kazi. Kwahyo hii ni moja ya sifa ya Mheshimiwa Ndugai

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Mheshimiwa Ndugai amekuwa Naibu Spika kama ulivyo wewe hapo kwenye kiti hicho. Aliongoza vizuri kiti hicho chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Spika Anne Makinda, lakini leo hii ndiyo Spika wetu wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; lakini isitoshe ni Baba wa familia na ni mtu mwema sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwasababu kuna watu wana tafsiri tofauti wanapomuona Mheshimiwa Job Yustino Ndugai. Mheshimiwa Ndugai kwa mambo ambayo yamezungumzwa hapa leo hii, ninaamini Wabunge wote tutaungana kwa pamoja kumpongeza na kulipongeza azimio ambalo linampongeza kama Bunge. Tuache roho za ubinafsi, na naomba Roho Mtakatifu awashukie baadhi yetu hapa tusiwe na miyo migumu, tuwe na miyo laini ya kuunga mkono azimio hili. Na niseme kwamba wale amba wana miyo migumu basi washindwe na walegee. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Spika Ndugai huyu huyu ameongeza Bunge amba lina mchanganyiko mkubwa sana wa Wabunge. Wabunge wa aina mbalimbali, wamekuwa na haiba mbalimbali, wamekuwa na mambo yao mbalimbali lakini amesimama imara kuhakikisha kwamba Bunge hili kama Muhimili linasimama vizuri. Najua katika kipindi chake tumeona baadhi ya gharama zimeokolewa na gharama hizi zimekwenda kwenye maendeleo ya wananchi, ambayo ndiyo tunayoyataka. Sidhani kama kuna Mbunge hapoa anaweza kuliona hili na akalibea. Ni Bunge hili kuitia kwa Spika huyu amezimamia kikamilifu matumizi sahihi ya fedha za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe utakuwa shuhuda, kwamba chini ya Mheshimiwa Ndugai umekuwa Naibu Spika mzuri sana mpaka watu wa Mbeya wanakutamani wakupe nafasi ya Mbeya Mjini kwasababu ya uongozi mzuri wa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni Spika huyu huyu Ndugai bila kupepesa macho ameanzisha suala la Bunge mtandao. Ni Mabunge machache hapa duniani yeny e-Parliament, yeny Bunge mtandao; na kwa Afrika ni moja ya Bunge jema na zuri sana linaloendeshwa kwa kutumia Bunge mtandao. Mwanzoni tulikuwa na tatizo kubwa sana la kubeza haya, lakini tunaangalia *the cost and benefit analysis*.

Ninaomba Waheshimiwa kwa watu wenye akili timamu tumieni akili zetu kuelewa haya wala si kupayuka payuka. Tumeweza kuokoa fedha nyingi kupitia suala la Bunge mtandao. Zaidi ya shilingi bilioni 100 zimeokolewa na fedha hizi zimekwenda katika ku-support shughuli za maendeleo ya wananchi ambapo kila Mbunge amekuwa akililia kwamba apate fedha kwenye miradi mbalimbali. Hii miradi haikuja hivi hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana ni binadamu, anaweza kuwa na mapungufu yake ya hapa na pale lakini amesimamia haki ndani ya Bunge hili na niseme Wabunge wenzangu bila kupepesa macho; kuna wale ambao mnaweza kuwa mmechukia lakini mchukieni kwa kiasi kwasababu anatimiza wajibu wake kama Spika wa Bunge; na ndiyo maana leo hii Bunge limekuwa na heshima kubwa sana ndani na nje ya nchi hasa kwa utekelezaji wa miradi kupitia bajeti ambao zinakuja hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba Mheshimiwa Spika amekuwa mshauri mzuri wa Mheshimiwa Rais. Mmeona mambo mengi sana yanakwenda sasa hivi kwasababu wewe pamoja na Mheshimiwa Spika mmekuwa washauri wazuri wa Mheshimiwa Rais juu ya jinsi gani bajeti za Serikali zipite hapa Bungeni kwa maslahi mapana ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai ameweza kufanya mambo mengi sana. Licha ya kufanya shughuli za upanuzi wa Bunge, majengo ya Bunge, nafasi mbalimbali za Wabunge, Wabunge hatukuweza kusafiri kwa kipindi hiki lakini tulikuwa na mkakati maalum wa kuunga jitihada na maono makubwa ya Mheshimiwa Rais. Tumeona mambo mengi yamepita hapa Bungeni, kuna baadhi ya watu walikuwa wanaona kwamba hayawezi kupita kwa usimamizi wako na Mhehsimiwa Spika mambo yamekwenda kwa maslahi mapana ya Watanzania.

Sasa naomba tu kama binadamu, kama kuna namna ya kuweza kumpongeza kwa njia ya pekee tuendelee kumpongeza Mheshimiwa Spika. Naunga mkono hoja hii na maazimio yote mawili hata la Dodoma kwasababu Dodoma ni Dodoma lazima tutaendelea kubaki Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanne Mchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lemma, Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua ajiandae.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hizi mbili; Azimio la Makao Makuu pamoja na Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo leo wa kusimama na kuchangia na kuyasema yale ambayo niliyapanga kumshukuru Mwenyezi Mungu. Kwahiyoo, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, namshukuru Mwenyezi Mungu kunitoa hofu katika kipindi chote hiki cha bajeti na tatizo kubwa la corona. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa maono yake kwa Watanzania kuwapa moyo kuhusu suala zima la corona. Ametupa ujasiri mkubwa. Tulipita katika tingitingi kubwa sana kwasababu upepo ule

ulivyopita Bunge liliyumba lakini Mheshimiwa Spika na Rais wetu hawakuyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe ni shahidi, mimi mwenyewe nilikuwa nakuandikia *ki-note* nakwambia kwanini huvi barakoa mbona watu wanavaa barakoa? lakini ulisema namuamini Mwenyezi Mungu. Halikadhalika, Mwenyezi Mungu na maombi yetu sisi Watanzania leo tumefika hapa tulipofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi nimpongeze Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika ni Mbunge ambae amekubalika na amebarikiwa na Mwenyezi Mungu. Bunge hili alivyoliendesha ndivyo alivyokuwa tangu mwanzo akiwa Naibu Spika kama wewe kwahiyo sifa zote anazo. Hata kama watu wana mapungufu, wanamchukia lakini anatenda haki sana katika Bunge hili kwasabbau Bunge hili angeyumba lingemyumbisha lakini amefanyakazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hilo tu, nimpongeze Spika kwa maamuzi yake. Wakati Bunge linayumba watu wanasema Bunge lina corona yeye alisimama akasema Bunge halivunjwi na Bajeti itasomwa na Bunge litafika mwisho wake.

Kwa hiyo nampongeza sana kwa uamuzi wake huo kwasababu angetetereka na Serikali ingetetereka maana yake tungeahirisha kila kitu, tungeahirisha uchaguzi, tungeahirisha kila kitu. (*Makof*)

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo mimi nataka kusema...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanne Mcchemba kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa John Heche

TAARIFA

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yangu ni ndogo tu; mbona wanapomsifia Spika wanakutenga wewe, kwanini? Hawa ni wabaguzi

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche Azimio linahusu Mheshimiwa Spika ambaye ni Mheshimiwa Job Yustino Ndugai ndiyo Azimio linamhusu. Mheshimiwa Mwanne Mcchemba.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuliona hilo. La kwanza nimekutaja lakini Azimio hili la Bunge ni la Mheshimiwa Spika sasa siwezi kutaka vile lakini nakubali kwamba wewe umenisaidia kuchanganua kwamba Azimio hili ni la Mheshimiwa Spika lakini unaposema Mheshimiwa Spika kwamba ni Azimio lake anao wanaomfuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio limekutaja kwamba ni mionganoni mwa wafanyakazi wazuri ambao mmetutetea na yeze anaelewa na ndiyo maana anacheke.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jingine; azimio hili wako wengine ambao lazima tuwataje. Kuna Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa anakaa pale kutwa hakuogopa corona; Mheshimiwa Waziri Mkuu amekaa hapo mwanzo mpaka mwisho. Kwa kuititia azimio hili hili la Mheshimiwa Spika mimi nampongeza pia Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nampongeza Katibu wa Bunge; Katibu wa Bunge nae kuititia kwenye Azimio la Mheshimiwa Spika mimi nampongeza na yeze amesimamia vizuri sana, Katibu wa Bunge hakuyumba. Hata hivyo azimio limetaja kwamba na yeze pia ni mionganoni ambao walikuwa sambamba na Mheshimiwa Spika na kufanya ushauri mzuri kwa Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika azimio hilo pamoja na kuunga mkono lakini nichukue nafasi hii

kuwapongeza pia Mawaziri na Manaibu Waziri kwa kupitia Spika kwasababu sitapata nafasi tena ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwapongeze wafanyakazi wa Bunge, nao walivumilia kwasababu ilishatangazika kwamba Bunge lina corona, Bunge lina corona wenzetu walitoka lakini sisi tukawa majasiri na tukapitisha Bajeti bila kupingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hilo, Wahudumu hawa vijana ambao wanatuhudumia humu ndani kwa kweli wamefanyakazi kubwa, wamefenyakazi bila woga, wamevumilia kwa kweli hata wao pia kma kungekuwa na kupandishwa daraja, kungekuwa na kupewa tunu wangepewa tuzo hawa vijana, hawakuyumba ndani ya Bunge hili. Kwahiyohayonayo ni maazimio ya Mheshimiwa Spika kwasababu hawa wako chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hilo tu; ningependa pia kuzungumzia habari ya uchaguzi, kwamba Mheshimiwa Spika Mwenyezi Mungu amjaalie apite bila kupingwa. Wanakongwa tunawaomba hiki ni kioo chetu cha jamii. Na mimi naomba pia na kwako kama alivyosema Mheshimiwa Chegeni tunakuombea Mbeya na wewe ushinde. Wewe ni Mbunge wa Viti Maalum una nafasi yoyote ya kwenda kugombea. Chagua, amua lakini sisi tunakuamulia kagombee Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niombe naendelea tena lakini niombe azimio hili ambalo nilitaka kulizungumzia ni kwamba la Makao Makuu; azimio hili mimi naunga mkono, wamesema sana, taarifa ya azimio la Bunge limesema kwahiyoh mimi naunga mkono kwamba kwa sasa sidhani kama watabadilisha atakaekuja Kiongozi yoyote. Viongozi wa CCM wana nidhamu na kwasababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndiyo itakayotawala milele ndani ya Serikali hii kwahiyoh nina imani hawatabadilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyoh baada ya kusema hayo mimi niunge mkono maazimio yote mawili ni kwamba

tutashinda na uchaguzi asilimia 100 kwa 100 kwa Rais anashinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, Mheshimiwa Amina Mollel ajandae.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tofauti kubwa kati ya kiburi na ujasiri. Sasa nimewasikiliza Waheshimiwa Wabunge ndani kwenye maazimio yote mawili, sina mgogoro mkubwa wa Dodoma kuwa Makao Makuu ila Dodoma inakuwa Makao Makuu katika karne ambayo ulipaswa kuiona Dodoma inafanana na Abudhabi, kuiona Dodoma inajengwa kama miji inayojengwa wakati teknolojia za ujenzi ni kubwa zaidi Dunia kuliko miaka 50 iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia barabara ukiwa juu ya ndege, ukiangalia majengo ya Serikli yanavyoota kama uyoga, *infrastructure* zake kipindi hiki ambacho dunia inakimbilia kwenye upandaji miti na mazingira na maua ukaambiwa kwamba Dodoma ni mji ambao unajengwa ndani ya miaka mitano ukiangalia *infrastructure system*, ukiangalia ramani za majengo, ukiangalia hata barabarani jinsi ambavyo kuna *organization decor* ya miti unaweza ukafikiri maamuzi ya kujenga Dodoma yalijengwa wakati simu ya mezani haijavumbuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa kwenye ndege unakuja *airport* ukiangalia hizo bati, mabati ya kawaida, ma-alumium, manini unasema hao watu wanaojenga Mji Mkuu wa kisasa leo wameshindwa vipi *ku-set standard* za kimataifa? Kwamba leo si tu mtu angekuja Dodoma kwasababu ni Makao Makuu lakini mtu ange-*feel* kuja

Dodoma kwasababu ni mahali ambapo *Town*iko-organized na barabara ni pana za kutosha. Sasa ninyi mnafikiri kujenga jiji ni lami, mnafikiri kujenga miji ni taa za barabarani. Ndiyo maana Babati Mjini mmeweka taa za barabarani, mkiweka *solar* mnafikiri ndiyo *city* na nyie wote mmesafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya ni moja; Bunge hili *Wabunge* wengi hawajasafiri kwahiy*o comparison* ya Dodoma mnafanya na Temeke ndiyo maana Madiwani wa Temeke wanakuja kujifunza Dodoma; hapa Dodoma hakuna cha kujifunza. Mji gani huu? Si jambo baya Dodoma kuwa Makao Makuu, kwanza ni katkati ya nchi watu wote wanapa-*access* vizuri; lakini mji unajengwa kama uyoga. Kujenga Makao Makuu ya kisasa kungekuwa na *long term plan* kwamba uwe mji ambao watu wangependa kuja kutembea na kuangalia angalau majengo tu. Unapita unaangalia majengo ya Serikali yote yamekaa Kichinachina.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Wewe umetoka wapi tena wewe?

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Dodoma.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Godbless Lemma kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Felister Bura.

TAARIFA

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa msemaji kwamba *master plan* ya Dodoma haipo Afrika Mashariki, wala haipo Afrika. Mji wa Dodoma utakavyojengeka, Roma haikujengeka siku moja na Dodoma haiwezi kujengeka kwa siku moja.

Kwa hiyo, nimpe taarifa kwamba Mji wa Dodoma utakuwa mzuri sana kutokana na *master plan* iliyopo; wataalam walioshughulikia *master plan* iliyopo walishirikishwa

kutoka nje na ndani ya nchi; na mwisho, walioleta *master plan* ni wazalendo walioaminika na Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Godbless Lema unaipokea taarifa hiyo?

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, hapania, hanielewi huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi; maamuzi ni maamuzi *recently*. Anasema kwamba Mji wa Dodoma utajengwa si ndiko huku tunaona unajengwa Chako ni Chako ama utajengwa wapi tena? Si ndiyo hii tunaona *airport*, ukienda leo *Area D* na *Area C* ile unaona hawa watu waliokuwa wanatoa mawazo ya kufunga barabara ile area yote ile *mmesha-block economy*. Hivi unajuliza hawa wanao-plan walishindwa kutengeneza bridge kwamba Ndege zipite juu pale magari yaendelee kupita kama kawaida? Sasa nilichosema ni kwamba, hauoni *clear concept* ya kuifanya Dodoma kuwa mji bora kuliko Mji wowote nchi hii, hauoni hiyo; na hicho ndicho ninachosema.

Sasa ukiniambia kwamba Dodoma itajengwa; hiki tunachokiona ukienda Abu Dhabi ama ukienda Abuja; Abuja imejengwa miaka ya nyuma, Dodoma inajengwa sasa, barabara zake zilitakiwa zifanane na miji mingine mikubwa ya fahari kabisa ya duniani. Sasa hii ni *fla project* kwa ajili ya uchaguzi na imekataa...

TAARIFA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Godbless Lema kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Juma Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe tu taarifa rafiki yangu hapa kwamba, hili Azimio siyo Azimio la kulinganisha miji; kuna tofauti hili Azimio

hatulinganishi miji hapa kwamba mji upi umefanya nini, mji upi umefanya nini, Azimio letu lilioko mezani asome vizuri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Godbless Lema unaipokea taarifa hiyo.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, chama chetu ama mimi mwenyewe sikatai Dodoma kuwa Makao Makuu. *Plan* ya Makao Makuu ya Nchi siyo bustani ya uyoga, hii *planilitakiwa* iwe kwenye *life span* hata ya miaka 20 ili kuwe na *proper structure*. Sasa ukiangalia Dodoma leo, yaani ukiangalia Dodoma leo ndiyo maana wafanyakazi wote wa Serikali wanaoishi hapa Ijumaa Dar...

T A R I F A

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, taarifa hiyo itakuwa ya mwisho kwa Mheshimiwa Godbless Lema.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka nimpe taarifa msemaji Mheshimiwa Lema, tunazungumzia Azimio la Mji wa Dodoma na la Mheshimiwa Ndugai, ameingiza Makao Makuu ya Chama chake, nataka nimpe taarifa Chama cha Mapinduzi kiko Dodoma na jengo lake lina hadhi, ukienda Dar es Salaam na Mikoa mingine na wilaya majengo yana hadhi, sasa ye ye sjui anataka kutufananisha na jengo lipi la chama chake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Godbless Lema malizia mchango wako.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru umemuelewa huyu mama, hivi Viti Maalum vinashida sana yaani hiyo michakato uko ndani itakuwa inashida sana na majimboni huko. Naomba unilindie muda wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ni hapa ndani ya Bunge, limekuja Azimio hapa. Katibu naomba unilindie muda wangu. Hapa limekuja Azimio kwamba Mheshimiwa Ndugai amefanya vitu vikubwa sana, amefanya Bunge limeanza kutumia *tablet*, sasa Bunge ni la kisasa, kwenye karne hii kutumia ...

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanne Mcemba kanuni inayovunjwa.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, msikilizeni.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilinde...

NAIBU SPIKA: Msikilizeni mimi ndiyo niliyempa fursa

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, 64(1) sitaisoma naomba nitoe maelezo kidogo, Mheshimiwa aliyekuwa anachangia hivi sasa amesema ndiyo shida ya kuwa na Viti Maalum, kwa hiyo naomba afute kauli yake Viti Maalum ni Mbunge kama Wabunge wengine.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hili ngoja nilitolee maelezo kidogo, tulishapata kuongea humu ndani mara kadhaa, Wabunge wote kiapo chao ni kimoja na Wabunge wote wana hadhi sawa. Humu ndani hakuna mtu anapimwa uwezo wake wa kuwa Mbunge kwa namna anavyozungumza, hayupo. Anapimwa kwa kuwa Mbunge kwa kiapo alichokula, amekuja vipi humu ndani, kapita njia hipi humu ndani, ye ye ni Mheshimiwa Mbunge ana hadhi sawa na Mbunge mwingine yeyote. Kwa hiyo, nisingependa

tuvute huu mjadala wa Wabunge wa Viti Maalum wanapatikana viyi kwenye vyama ambavyo vinawaleta humu ndani. Wabunge wote wana hadhi sawa. Kwa hiyo, tutoe heshima wanayostahili. (*Makof*)

Mheshimiwa Godbless Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni *spinning* tu, mimi nareshimu sana Wabunge wote, siwezi kuwasema wabunge Viti Maalum wakati mbele yangu amekaa Mbunge Viti Maalum. Nimesema hivi maswali ama taarifa ambazo hazieleweki zinasababishwa na michakato inayoanza karibuni ya Viti Maalum na Majimbo ndiyo maana mtu anaibuka kuomba taarifa ili aonekane eeh ndiyo nimesema hivyo hata...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lema, Lema humu ndani...

Waheshimiwa Wabunge leo tunalo Azimio la kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa sababu maalum ya namna alivyoliendesha Bunge la Kumi na Moja. Sababu moja wapo ni hilo la kushughulika na Wabunge 393, sasa humu ndani mimi kama msaidizi wa Mheshimiwa Spika nawafahamu Wabunge, nawafahamu Wabunge wa Viti Maalum, kama ni kwenye mitandao na mimi niko kuna Wabunge hawana adabu hata kidogo, lakini tusiende huko Mheshimiwa Lema, kama ni mchakato wa baadaye ama wa sasa Wabunge wote kwa sasa na tuko Bungeni wana hadhi sawa. Ikiwa ni pamoja na kuwavumilia hata wale tunaosema hawana adabu.

Mheshimiwa Lema malizia mchango wako.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nisibishane na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye moja ya maazimio ya kumpongeza Mheshimiwa Spika, Ndugu yangu rafiki yangu Kitwanga alisema ni pamoja na Bunge kutumia *tablet*, hivi *serious* kwenye karne hii tunakuja kulipongeza Bunge kwa

Wabunge kutumia *computer,serious!* Yaani Mabunge mengine kwa ushawishi wa Spika na Wabunge wanajadili Mataifa yao kufanya utafiti sayari ya *mars*, waone kama waone kama wanaweza wakauza viwanja binadamu wakaishi huko *incase* kuna *atomic* bomu leo tunakuja hapa tunasema hapa tunalipongeza Bunge kwa Spika kutuleta *tablets.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kama umeoa *ten years ago*, halafu unampeleke mke wako kanga, halafu unataka wakwe waje wakupongeze umeleta kanga kwa mke wako. Hebu tuwe *serious* na mambo makubwa, ndiyo maana nilisema kunatofauti katika kiburi na ujasiri, wajibu wa Bunge ni kutunga sheria bora. Ukiponja wajibu wa Bunge utajua upongeze nini? wajibu wa Bunge ni kuisaidia Serikali, kuishauri Serikali na kuiadhuru Serikali. Sasa tukitaka kupongeza tuijilize Spika amesaldia wapi kwenye sheria mbovu katika nchi hili juu ya Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kesho hapa unakuja Muswada nilikuwa naupitia na Mheshimiwa Salome, ukiangalia unajiuliza uko wapi uongozi wa Bunge kuruhusu baadhi mambo kuingia ndani ya Bunge. Sasa kama leo tunapongeza *tablets* kwamba ndiyo kazi ambayo tunaweza tukaipongeza, kazi ya kwanza ya Bunge la kidemokrasia ni uhuru wa Bunge ambalo Bunge hili kwa miaka zaidi ya mitano halijawahi kuonekana hadharani, kwa kusema kwamba kuna gharama lakini *TBC One* inafanya vitu vingine vya ajabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uko wapi uhuru wa Bunge, leo makosa, makosa ambao Wabunge kwa kutofautiana ni kimitazamo, siyo matusi kimitazamo, yamewafanya Wabunge wengine sasa ni hivi ni kweli hatuwezi kushinda ama Azimio haliwezi kuzuiwa, ila Mungu anaangalia moyo na binadamu anaangalia nje. Sisi ngoja tuangalie *tablets*, Mungu anaouona moyo, kweli leo mnaweweza mkasema Bunge hili kwa miaka mitano iliyopita limekuwa *effective*, demokrasia tu ya Bunge hili imekuwa imekuwa *effective*. Mnasema ameruhusu hawa vijana waongee, mimi sihitaji hiari kuongea ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *actually* Katiba na

sheria ndiyo imenileta huku na wananchi, mimi simo humu ndani kwa *favour*, siyo fadhila. Hii ni *term* ya pili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni juzi tu Mheshimiwa Spika amefunguliwa kesi huko wapi Dar es Salaam juzi. Mheshimiwa Cecil Mwambe ameonekana kwenye vyombo vyahabari anapokewa na Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Bashiru. Mheshimiwa Spika anamrudisha, nikajuliza hivi hata Katibu Mkuu wake alishindwa kupiga simu, aseme huyu mtu ameshakuja kwetu mara mbili kapokelewa na Polepole, iko wapi hadhi ya Bunge. Waheshimiwa iko wapi hadhi ya Bunge? Wote nyie tutaondoka hapa mchakato unaanza kesho kutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba bado muda wangu uuchukulie sana.

MBUNGE FULANI: Endelea bwana.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, tutaondoka kesho kutwa, wewe utakwenda kwenye mchakato wako Mbeya, mimi nitakwenda kwenye mchakato wangu Arusha, Mheshimiwa Mgombea Urais hapa anaweza akawa mgombea wetu wa Urais, ataenda kwenye mchakato wake wa urais. Kila mtu anakwenda kwenye mchakato wake, Bwashehe naomba unisikilize.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna dhambi Bunge hili imefanya ni kusaidia demokrasia iuawe. Watu mnasema kwamba CCM itaishi milele, sio tabu Chama chochote cha siasa kuishi milele, lakini kama Mtu hataishi milele hakuna chama kitakachoishi milele. Kazi ya Bunge hili hata tukiongea sana leo hatuwezi kusaidia sana kwa sababu muda umekwisha. Hatuna siku tano, siku kumi na mbili mbele, tunakwenda kuanza mchakato mpya, ila kila ubaya uliofanywa na Bunge hili na sauti zinazojali wema na haki zikashindwa kusaidia ndani ya Bunge hili, wakati unakuja ambapo *karma is a gangster, karma itamlipa* kila mtu kwa kadri alivoytenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine ukiangalia mawazo ya Wabunge wengi wa Chama cha Mapinduzi...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MBUNGE FULANI: Muda gani wewe ni Naibu Spika?

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unilindie muda wangu tafadhali.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda unatunzwa na Katibu. Mheshimiwa Lema malizia mchango wako.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nasema Waheshimiwa Wabunge kazi yetu sisi haikuwa kupongeza Bunge. Kwanza eti haiwezekani Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Spika likatoka kwetu. Eti *surprise* ya *happy birthday* unajifanyia mwenyewe eti *happy birthday* najifanyaje *surprise* ya *happy birthday*? Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Spika tungesikia Kenya wamesema kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *is purely democratically* ama Bunge lijalo lingesema kwamba kwa kweli Bunge lile lilikuwa ni *purely democratically*. Sasa leo unajifanyia *birthday* mwenyewe halafu unajipongeza, unajifanyaje *surprise* mwenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Bunge ni kuimarisha demokrasia, mkatafakari Bunge hili limeimarisha demokrasia? Kazi ya Bunge ni kujenga mahusiano. Wakati wa Bunge liliopita la mama Anna Makinda, tulikuwa tunaminyana humu ndani, Waheshimiwa Mawaziri wanajua tukitoka hapo nje ni marafiki. Leo mtu anafiwa wa CCM mnagombania hata miili huko Mbeya umeona, yaani hata ile *culture ya love* ambayo ilitakiwa kujengwa na Mhimili wa Bunge haipo, leo mnasema amejitahidi sana hatukukimbia *corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hamkukimbia *corona* na *corona* kweli Mheshimiwa Ummy anatuambia imeisha. Halafu

nyie wote mnajua haijaisha, tukikaa huko kantini kwenye kahawa mnajua haijaisha, mnajua mambo yanaendelea, lakini sasa hairuhuswi hata *kuvaa barakoa humu ndani kwa sababu zina sura ya chuchu*. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa mnasema Mheshimiwa Spika amepiga mzigo wa kutosha apongezwe, mimi Mheshimiwa Spika ni rafiki yangu sana. Mheshimiwa Spika ni rafiki yangu siku nyingi sana, namheshimu sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lema hiyo maneno ya barakoa inafanana na nini embu ondoa hiyo habari. Ile ni barakoa na imetengenezwa vile kitaalam kwa ajili ya kazi mahsusii.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika, naondoa yale maneno yaliyoongewa huko nje yalikuwa sio mazuri naondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema mimi binafsi, *personal* sina shida na wewe binafsi wala Mheshimiwa Spika ila kiutendaji hakuna Bunge limefanya vibaya kama Bunge hili katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kesho mtaleta Muswada wa Sheria wa kujilinda mtakapotoka msishtakiwe. Hata ukipita Bunge litakalokuja hata litakuwa la CCM sisi wote tutaondoka, haki huo ni ugomvi wa Mungu. Watakuja Waheshimiwa Wabunge wa Chama chenu hicho hicho na siku moja watatunga sheria watageuza sheria zote mbaya katika Taifa hili na zitaanza kufanya kazi kurekebisha Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama kungekuwa kuna vitu vya kupongeza tungesema. Katibu tayari au bado kidogo?

NAIBU SPIKA: Ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Muda umeshaisha Mheshimiwa.

WABUNGE FULANI: Endelea Mheshimiwa.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Naibu Spika...
(Makofii/ Kicheko)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lema kengele ya pili imekwisha kugonga.

MHE. GODBLESS J. LEMA: *So it's over sio*, haya poa.
(Kicheko)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura ajiandae.

MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata muda wa kuchangia kidogo. Ningependa kuanza kwa kusema kuna tofauti kubwa kati ya macho na kuona. Unaweza kuwa na macho lakini usione na unaweza kuwa na macho ukaambiwa utazame ukashindwa kutazama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya maamuzi ya kuifanya Dodoma iendelee kuwa Makao Makuu, ni suala la maslahi ya Kitifa na kwa maana hiyo kila mpenda nchi yake ataunga mkono. Nami natumia fursa hii kuunga mkono Azimio hilo, lakini pia naunga mkono Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kazi kubwa aliyofanya kuongoza Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili limefanya mambo mengi katika kipindi chake cha miaka mitano. Aliyewasilisha Azimio amesema, lakini hatuwezi kuyataja yote ni mengi, mengi sana. Yapo mapinduzi makubwa yaliyofanywa kwenye mifumo yetu ya sheria kusimamia sekta ya madini na faida yake tunaiona leo. Yako mambo mengi, lakini haya tu yaliyofanyika katika kipindi hiki kifupi ambayo wenyewe macho wanayo, lakini hawayaoni ni muhimu kuyataja angalau kidogo. Uamuzi wa kufikiria tu kwamba Bunge letu

liendeshwe katika mfumo wa Bunge Mtandao nayo ni mapinduzi makubwa. Mapinduzi makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa ikiwa mtu anabeza mambo haya muhimu ambayo yametufikisha hapa leo tulipo, bila ya kutumia Bunge Mtandao, leo hii tungewezaje kuendesha Bunge kwa urahisi na kwa gharama nafuu namna hii. Ni muhimu kuona umuhimu wa ubunifu na fikra za Mheshimiwa Spika katika kutupeleka hapa tulipo. Matumizi yenye tu ya Bunge Mtandao yamedhihirisha weledi wa hali ya juu wa Watumishi wa Bunge waliopo chini ya Mheshimiwa Spika kwa kitendo cha kutengeneza *platform* ambayo ni *very interactive and user friendly*. Kila Mbunge amejifunza siku moja na kuweza kuitumia, hata wale ambao walikuwa hawawezi kutumia mitando.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo kubwa na ni la kipekee kabisa, ni muhimu na lazima tulizungumze. Kimsingi Bunge limehawilisha kabisa fikra za Wabunge kutoka kuendesha shughuli za Kibunge za kizamani na kuendesha shughuli za Kibunge kwa njia za kisasa. Bila shaka bila ya umahiri, uweledi na msimamo wa Mheshimiwa Ndugai tusingefika hapa tulipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunatakiwa kutekeleza majukumu yetu, tukiwa pamoja, nchi yetu na dunia kwa ujumla iliingiwa na fazaa ya ugonjwa wa *corona*, hakuna asiyejua. Bila shaka, bila ya kuwa na matumizi ya Bunge Mtandao tusingeweza kutekeleza majukumu yetu ya kuisaidia nchi ili iende. Kwa sababu Bunge liliendelea kuendeshwa bila ya Wabunge kusongamana na bila ya Wabunge kukaribiana. Haya ni mapinduzi makubwa sana, bila Mheshimiwa Ndugai nani angekuwa na moyo mkuu kama yeye wa kuwataka Wabunge waendelee kushiriki katika shughuli za kibunge katika mazingira hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe wa kweli, wakati tuna Mheshimiwa Ndugai anafanya maamuzi ya kuendelea na shughuli za Bunge wakati nchi yetu imekumbwa na fazaa ya janga la *corona*, hakika alifanya kazi hiyo kwa *pressure* kubwa

ya ndani ya Bunge na nje ya Bunge, lakini hakulala, badala yake aliendelea kufanya uamuzi wa sisi kuendelea kufanya kazi kwa maslahi ya nchi. Hata wale waliothikisa kibiriti, kiliwalipukia wenyewe. Tuliendelea kuchapa kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, amebuni kwa kiwango cha hali ya juu utaratibu wa kuendelea na taratibu za Kibunge. Niseme hakika ni busara kuwa na Spika kama Ndugai kimsingi sisi kama Wabunge tunamtegemea tunamwamini amekuwa akitulinda na tunadhani ataendelea kutulinda nasema kwa kauli yangu na moyo wangu wa dhati kongole sana Ndugai kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais aHsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Amina Mollel atafatiwa na Mheshimiwa Felista Aloyce Bura, Mheshimiwa Peter Msigwa ajiandae.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kusimama hapa tena. Kabla ya yote naomba niunge mkono maazimio yote mawili azimio la kumpongeza Mheshimiwa Rais vilevile azimio la kumpongeza Spika wetu mpendwa wetu Job Yustino Ndugai.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kadhaa nimetamka hapa Bungeni nikisema kwamba Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ni zawadi ya watanzania kutoka kwa Mwenyezi Mungu na ninarudia tena kwa kusema kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ni zawadi kwetu sisi watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni zawadi kwa sababu ni Rais mwenye ujasiri mwenye udhubutu, mwonyesha njia na ametuonyesha njia na bado anaendelea kutuongoza katika hiyo njia ya kuelekea uchumi wa kati katika Taifa hili kufikia mwaka 2025. Kwa hiyo, kipekee kabisa kwa moyo wangu wa dhati tunajivunia Mheshimiwa Rais tunajivunia Makamu

wa Rais tunajivunia Waziri Mkuu pamoja na Baraza lake lote la Mawaziri kwa utendaji mzuri ambao leo hii ndio wanaotuwezesha pia kusimama hapa na kumpongeza Rais pamoja na Mheshimiwa Spika kwasababu siku zote katika mafanikio hawa wote kwa pamoja wamesaidia kufanikisha hayo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tukiwa wadogo tunasikia kuhusiana na makao makuu kuwa Dodoma lakini leo hii kwa kweli tunaona kabisa mafanikio haya kwa vitendo na historia imeandikwa na itaendelea kuwepo kutokana na maono ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuhamishia Makao Makuu kuwa Dodoma.

Leo hii tunapopitisha azimio hili ni dhahiri kabisa kwamba yale yote sasa na itakuwa ni vugumu kwa mwingine yeote mwenye maono tofauti kuja nakubadilisha makao makuu kuyaondoa hapa na kupeleka maeneo mengine. Mengi yamesemwa lakini wanasema kupanga ni kuchagua tulipanga hatimaye tukachagua na sasa umechagua huu ni mwanzo na bado tunaendelea kuifanya Dodoma kuwa mji wa kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka michache tu mitatu hivi sasa tangu tumehamia Dodoma haya ndio maajabu kwa kweli ambayo kila siku tunasema Rais Dkt. John Pombe Magufuli ni Rais wa mfano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji huu Dodoma baada ya miaka 10 sio Dodoma hii ya sasa itakavyokuwa na hata hivi sasa kwa miaka 3 tu tumeona mafanikio haya ya Dodoma. Mtu ambaye ameondoka katika Mkoa huu wa Dodoma miaka 5 akija sasa atasahau Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sisi kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nikiwa Mbunge kutoka katika Chama Tawala chama ambacho ndio chenye Serikali hii kwa kweli najivunia sana kuwa na Rais mwenye maono mbeba maono Rais Dkt. John

Joseph Pombe Magufuli. Sisi kwetu tuzidi kumuombea Mwenyezi Mungu ampe afya njema tumeona tunajivunia kwa yale ambayo amekuwa akyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niseme tu kwamba katika azimio la pili la kumpongeza Mheshimiwa Spika, hapa kwa kweli tuna kila sababu pia ya kumpongeza hasa kwa kulifanya Bunge hili kuwa Bunge la kisasa. Ni miongoni mwa wawakilishi katika Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Mwaka 2017 tulikwenda nchini Nigeria na moja ya maazimio ambayo alipitisha ni kuyataka Mabunge yaliyo chini ya Jumuiya ya Madola kuanza kutumia teknolojia mpya ya mtandao na hivi sasa tunaona kwamba Mheshimiwa Spika ametekeleza jambo hili na ni miongoni mwa nchi chache ambazo tayari zinatumia E-Mtandao kwa kweli hongera sana kwa Mheshimiwa Job Ndugai pamoja na wewe kwasababu wanesema kwamba katika mafanikio yoyote yale wewe pla upo nyuma kwasababu umekuwa ukimsadia hapo kwa hiyo, kwa kweli tuna kila sababu ya kujivunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika azimio wakati likiwasilishwa hapa walizungumzia mpaka kuhusiana na yale ambayo ameyafanya katika Bunge hili. Na katika Bunge hili ndio Bunge ambalo kwa kweli tumeshuhudia pamoja na changamoto mbalimbali lakini Spika wetu amesimama na kuwa mwongoza njia na kutuongoza sisi hata katika mapambano ya ugonjwa wa Corona tulilogopa na wakati mwingine tulikuwa tunajifungia ndani. Lakini kauli ya Mheshimiwa Spika kwamba Bunge ni lazima liendelee lakini pia mwongoza njia Mheshimiwa Rais Dkt John Joseph Pombe Magufuli tulipata ujasiri na nchi yetu ya Tanzania imenusurika na tunamshukuru sana ndio faida ya kuwa na viongozi ambaao wanakuwa na hofu ya Mwenyezi Mungu na hili kwa kweli litaendelea kuwa historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mbunge ninayewakilisha watu wenye ulemavu nilisema hapa kwamba tangu nimekuja sijawahi kufika ghorofa ya nne lakini kupitia kwa Mheshimiwa Spika hatimaye amekamilisha jengo la utawala kuwa na lift, kwa hiyo sio sisi tu na mmesikia

kwamba wengine wanasema na wao wameweza kufika huko hili ni jambo la kujivunia kutokana na maono, ujasiri na uchapakazi ambao umeonyeshwa na Rais wetu pamoja na Spika wetu ambaye kwa kweli ni Spika wa viwango. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na Bunge hivi sasa tunaona kwamba ni Bunge ambalo kwa kweli limekuwa na nidhamu ya hali ya juu ni Bunge ambalo kwa kweli humu ndani ukitaka kufanya fujo wewe mchezee Spika akiwa hapo, mchezee Naibu Spika akiwa hapo na umetulia kweli kwenye kiti chako na sheria zikiwa kichwani mwako hongera sana Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana Mheshimiwa Spika na tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu kwamba tunapoelekea katika Bunge la Kumi na Mbili wewe kama mwanamke uende ukafanikiwe huko Mbeya na sisi tupo ambao ni askari katika kushambulia majukwa tutakuja huko kukuunga mkono. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa Spika wetu tunamwombea kila la heri apite bila kupingwa ili tuje tuendeleze mapambano haya. Viti Maalum kwa kumalizia tu kwamba tumeshuhudia utendaji mzuri mawazo mazuri ushauri mzuri ambao umekuwa ukitolewa na Wabunge wa Viti Maalum. Viti Maalum ni Wabunge majasiri na hata kama wapo wachache basi wahukumiwe kutokana na makosa yao na Viti Maalum viendelee kuwepo kutokana na kwamba Mheshimiwa Naibu Spika tumekuwa hapa tukishirikiana kwa pamoja na kumsaidia Rais wetu ahsante sana. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Felista Aloyce Bura atafatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau ajiandae.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia maazimio haya mawili. Mwaka 2015 ilikuwa mwaka wa 43 tangu Serikali ilipotangaza kuhamia Dodoma na Mheshimiwa Rais wetu jasiri jemedari mwenye kuamua na kusimamia maamuzi yake. Tarehe 25 Julai, 2016 alitangaza Serikali kuhamia Dodoma waliombeza wakamwona kwamba ni nguvu za soda lakini

alipoamua aliamua tunaona Serikali imehamia Dodoma. Na nimakikishie Mbunge aliyesema kwamba Dodoma inajengwa hovyo tuna *master plan* ambayo hajawahi kuiona. Na ile *master plan* ipo pale jiji ye yeyote anayetaka kwenda kuona *master plan* ya Dodoma akaione na uwanja wa ndege unaozungumzwa sio huu tunaouona uwanja wa ndege wa kimataifa wenyewe kuweza kuhudumia ndege 50,000 kwa mwaka unajengwa pale Msalato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumejenga stendi ya mabasi ya mkoa ya kimataifa kama anaitaka kujua Dodoma ni makao makuu akaone. Tunajenga barabara za mizunguko *ring roads* yenye kilometra 220 anayetaka kujua aende jiji akaone. *Master plan* ya Dodoma ni ya kimataifa , reli zitapita hapa kuanzia Kongwa kwa Mheshimiwa Spika kuja Dodoma Mjini hujapata kuona. Treni ya mwendokasi kituo chake kikuu kitakuwa Dodoma haijapata kutokea na haya yote yamefanikiwa kwasababu ya uongozi wa Ndugai, Mheshimiwa Spika bila yeye kuwa na mahusiano mazuri na muhimili anaosimamia haya yote tusingeyaona, haya yote yasingetokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na namshukuru sana Mheshimiwa Spika nampongeza pamona na wewe Naibu wake aliyetaka kuchezea meza yenu hamkukubali waliotaka kuwabeza hamkukubali watu walipewa adhabu hapa miezi mitatu wako nje ya Bunge kwa sababu ya kutokuheshimu kiti. Nakupongeza Naibu Spika, nampongeza Spika kwa kuwa jasiri hawakutaka kuchezewa hata sisi hawakutaka tuchezewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uongozi wako na kwa uongozi wa Spika tumeona juzi Serikali imelipa *US Dollar* milionii 100 kwa sekta ya madini tungepata wapi na tume aliyoiunda Mheshimiwa Spika ndio matunda yake haya. Unawezaje kusema mafanikio ya sekta ya madini bila kumtaja Spika, bila kutaja tume zile alizoiunda. Marekebisho ya sheria mbalimbali, Sheria ya Madini watu walikuwa wanaogopa wale wawekezaji lakini Bunge liliposimama imara Rais aliposimama imara sheria imepitishwa wale wawekezaji

wamekuja wenyewe wanatembea kwa magoti. Natamani kusema Spika hoyee kwa kazi nzuri anayoifanya. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Hoyeee!

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakuombea kwa Mwenyezi Mungu akutangulie katika kile unachokitamani.

WABUNGE FULANI: Ameni.

MBUNGE FULANI: Mbeya Jiji!

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwa upande wa Dodoma Mheshimiwa Ndugai anapita bila kupingwa na sisi tupo. Kwa hiyo waliodhani kwamba lugha ya matuzi lugha isiyo na staha Mheshimiwa Spika angevumilia hakuvumilia walimtukana kwenye mtandao alisimama imara kwa nini tusimpongeze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanasema eti tunampongeza kwa *tablet!* Hatumpongezi kwa *tablet* tunampongeza kwa mambo makubwa yaliyofanywa na Bunge hili na ikiwemo *tablet* ikiwemo! Mbona wa zamani hawakuleta *tablet* hizo, mbona wa zamani hatukuona haya tumeona kwenye kipindi chake. Mbona Miswada mbalimbali iliyoleta mapato makubwa ndani ya Serikali mbona wengine hawakuyafanya? Yamefanyika katika kipindi hiki kwa usimamizi wake kwa uelewano wake na mhimili anayoisimamia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na sisi Wabunge ametupa nafasi kuna Mbunge ambaye hakupata madawati, madawati yale yalinunuliwa na fedha zilizotoka hapa Bungeni. Tunajenga sekondari ya wasichana na wale wasichana watatoka kila mkoa ni uamuzi wa Bunge hili na uamuzi wa Bunge hili lilitosimamiwa na wewe Naibu Spika, maamuzi yaliyosimamiwa na Spika na tulimlaumu tumechangisha fedha na hatuoni kinachoendelea sasa

wasichana kutoka pande zote za Tanzania mikoa yote watakuja kusoma hapo Bunge *Girls High School.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaposema tusimpongeze Spika hata sikuelewi, unaposema tusimpongeze Serikali kwa makao makuu kuhamia Dodoma hata sikuelewi. Bunge lililopita wapinzani walitusema sana miaka 43 hamhamii Dodoma maneno tu, maneno tu leo Serikali imehamia Dodoma wamegeuka mbele nyuma, nyuma mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa lakini naendelea kuunga mkono azimio hili watanzania wanafurahi sasa hivi wanawake waliokuwa wanaona waume zao saa nane usiku Dar es Salaam sasa hivi wanaonekana saa moja nyumbani. Dar es Salaam muda mwingu ulikuwa unaishia njiani wafanyakazi wanachukua muda mrefu barabarani kwa ajilli ya foleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi anayekaa *Area C* mtumishi wa Serikali dakika ngapi yupo Ihumwa, yupo Mtumba muda mfupi kabisa. Kwa hiyo shughuli za Serikali zinakwenda na ndio maana mwaka huu sasa hivi mapato ya Serikali yamepanda kwasababu kuna uwajibikaji. Serikali isipowajibika Bunge lipo tunaulizwa anayesema Bunge ni dhaifu, ni dhaifu yeye siyo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Udhifu wa mtu mmoja usijumuise kwa wote Bunge hili liko imara kuliko Mabunge yaliyopita. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya kazi kubwa mapato yameongezeka na ndio maana hospitali zinajengwa, miradi mikubwa inafanyika umeme kule Rufiji kazi inaendelea, treni tunajenga, hospitali watu wanapata madawa wanatibiwa. Juzi Mheshimiwa Rais kaajiri madaktari 1000 uliwahi kuona wapi, madaraja yanajengwa, maji wanawake wanapumzishwa ndoo vichwani tunataka nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi iliyofanyika na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi wa Spika wa Jamhuri ya Muungano ndugu Job Ndugai na wewe ukimsaidia ni jambo

la kupongezwa. Kipindi kilichopita wanawake na vijana ndio walikuwa wanapata mikopo sasa hivi tumetunga sheria wenyewe wanawake, vijana, na walemavu wapate mikopo. Kama Mheshimiwa Mbunge usimamii eneo lako hilo ni la kwako unawanyima wananchi wako faida matunda ya nchi hii usiwanyime matunda ya nchi hii. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio hili naliunga mkono na nikuombee kwa Mwenyezi Mungu wewe pamoja na Spika wetu Mungu awajalie turudi na sisi tukirudi hatufanyi ajizi tunarudi hapa na mtarudi hapa kwa kishindo niwaambie na safari hii nitoe tu angalizo kwamba Chama Cha Mapinduzi tunaweza tukashinda kwa kura nyngi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi naunga mkono azimio zote mbili kwamba tumpongeze Mheshimiwa Spika kwa kazi kubwa aliyofanya pamoja na watendaji wengine. Lakini kwa Dodoma kuwa Makao Makuu naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano, naipongeza sanaa chini ya jemedari wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kumsahau jemedari wetu wa Bunge hili Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa uongozi wake mzuri katika Bunge letu hili Mungu ambariki Mungu amlinde, asante sana. (*Makofi/Vigelegele*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa atafatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mheshimiwa Cosato David Chumi ajiandae.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kazi kubwa ya Bunge ni sisi kama Wabunge sisi ni *tax payer representative* hili neon mpaka namaliza Bunge hili nimelirudia *over and over and over*. Kazi ya kwanza ni *tax payers representative* na kazi ya pili ni kuhakikisha tunatunga sheria na tunasimamia kile tunachokitunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati azimio hili limeletwa la kuhamia Dodoma Bunge hili lilikiuka katiba ya nchi na ni kitu kibaya kama Wabunge tunakiuka Katiba ya Nchi.

Ukisoma katika Ibara ya 98 imezungumza mambo ambayo mabadiliko yake yahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara, theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana nzima, *agenda* nzima ya kuhamia Dodoma ni nzuri, alianzisha Mwasisi wa Taifa letu, Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere. Hakuna anayekataa *agenda* ya kuhamia Dodoma, lakini sisi kama Wabunge ni lazima tuwe na wivu mkubwa wa kulinda mhimili huu. Tuwe na *zeal* ya kuhakikisha tunalinda mhimili huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma katika Katiba hii nawe ni Mwanasheria, katika mambo ambayo yanahitaji theluthi mbili, ukisoma hapa yako nane. Jambo la kwanza linasema, kuwapo kwa Jamhuri ya Muungano, lazima theluthi mbili; upande wa Zanzibar na Bara. Lazima hii ifuatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo tulikiuka katika Bunge hili ni kuwepo kwa Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano. Bila kuzomeana hapa, bila kuzodoana hapa, tujiulize Wabunge tuliomo humu ndani, ni lini tulipiga kura ya theluthi mbili kuitisha Ofisi ya Mheshimiwa Rais kuwa Dodoma? Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, wewe ni Mwanasheria hapo; tulipiga kura lini katika Bunge hili tunakwenda kumaliza sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa badala ya kuzomeana na kuzodoana, haya mambo tujadiliane kama Wabunge, kama Wawakilishi, kama *taxpayers' representatives*. La pili, tulilalamikiana hapa siyo hilo tu, hilo ni kubwa la kuvunja Katiba ya nchi na tuliapa hapa kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lining, kuhamia Dodoma...

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mch. Msigwa, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

T A R I F A

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu anayoyazungumza Mheshimiwa Mch. Msigwa yanagusa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuna upotoshaji, ni lazima niweke rekodi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, anazungumza juu ya mambo ambayo mabadiliko yake yanahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar. Amekwenda katika orodha Na. 2 katika orodha iliyopo hapo inayohusu kuwapo kwa Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri yake anasema, hilo ni suala la uwepo wa Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano Dodoma. Siyo sahihi. Katiba inachozungumzia ni kuwepo kwa hii taasisi inayoitwa Rais. Siyo mahali ambapo taasisi hiyo ya Rais itaweka Ikulu yake au Makao yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo naomba nilitolee ufanuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mch. Msigwa, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. MCH. PETER S. MSINGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo taarifa siipokei. Nataka nikuhakikishie, hiki kipengele kama hatujafuata pamoja na nia nzuri ambayo mmefanya, watakapokuja watu wengine watatu-*question*, tuli-*violate* Katiba. Mwanasheria Mkuu wa Serikali nakuheshimu sana, sikubaliani na taarifa yako.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mch. Msigwa, kaa kidogo, utamalizia mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, sisi hapa ndani sote tuliapa kuilinda Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naamini kwenye vishkwambi vyetu wote tunayo nakala ya Katiba, kwa hiyo, wote tunaweza kwenda kwenye Ibara ya 98(1)(b) ambayo unakwenda kuisoma pamoja na Orodha ya Pili; na hiyo Orodha ya Pili ndiyo ambayo Mheshimiwa Mch. Msigwa alikuwa akiipitia. Katika kuipitia kwake, kwenye mchango wake ameeleza kwamba yaliyoko hapa (na ninyi mtaipitia hiyo Katiba) yanataka kama kuna mabadiliko yoyote, basi yafanywe kwa utaratibu uliowekwa hapo.

Kama alivyokuwa ameeleza kwenye eneo hilo ni sawa kabisa, kwamba mabadiliko ya haya maeneo nane lazima yafuate huu utaratibu wa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge kutokea Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge kutokea Tanzania Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge, jambo mahususi kwenye hili, ni hili Na. 2 hapa linaloeleza kuhusu kuwepo kwa Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano. Ukiyasoma maneno haya ambayo yameandikwa kwa lugha fasaha kabisa ya Kiswahili, yanaelezea uwepo wa ofisi, hayaelezei ofisi kuwa wapi, hayaelezei mahali ofisi itakapokuwa, inaeleza uwepo, siyo mahali itakapokuwa.

Kwa hiyo, hakuna mahali popote ambapo Bunge hili ama mtu mwingine yeyote aliyefanya maamuzi ya kujenga ofisi mahali popote pale aliyeunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, Katiba hii haijavunjwa mahali na Bunge au na hata Serikali kuamua kujenga ofisi mahali fulani. Kwa hiyo, hilo likae hivyo na hiyo ndiyo tafsiri kwa sababu hapa hakuna mtu aliyelekea Mahakamani na huo sasa ndiyo mwongozo sahihi wa tafsiri ya kifungu hiki cha Katiba hapa Bungeni. (*Makof!*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mch. Msigwa, kwenye hiyo hoja ya Katiba kuvunjwa kwenye hicho kifungu, halipo hilo suala. Endelea na mchango wako kwenye masuala mengine.

MHE. MCH. PETER. S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru. Kwa kifupi niseme tu, kuja Dodoma; *moving from Dar es Salaam to Dodoma, it was unbudgeted, unprepared, unplanned, uneconomical and according to me unconstitutional.*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mch. Msigwa, sasa twende vizuri. Nimeshatoa maelekezo. Habari ya kuwa *unconstitutional* ama *constitutional*, nimeshatoa maelekezo. Huwezi tena kuja na maelekezo juu ya hilo nililolitolea maelekezo.

Kwa hiyo, elezea mambo mengine, habari ya kuwa *unconstitutional* haipo, kwa sababu ndiyo tafsiri halisi ya Katiba hii niliyoitoa mimi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, haya nimelitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowenza kusema, hata tukipigiana makofi kwa ushabiki, *fanaticism*, ukweli utabaki pale pale kwamba chombo hiki ni chombo cha kuwawakilisha wananchi kufanya mambo ya msingi, siyo mambo ya ushabiki. Hii Katiba ndiyo tumeisoma, tulinde na tulitendee Bunge haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hoja ya pili; rafiki yangu, Mheshimiwa Kitwanga, anasema tumpongeze Spika. Kama Mheshimiwa Lema alivyosema, mambo ya humu ndani siyo *personal*. Binafsi tumekaa na Spika miaka kumi, Waziri Mkuu miaka kumi hapa na rafiki yangu, Mheshimiwa Jenista miaka kumi. Tumekaa miaka kumi hapa ni marafiki, lakini *when it comes to business* lazima tuambizane ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili azimio aliloleta Mheshimiwa Kitwanga *actually* halimsaidii Spika. Kwa maoni

yangu, wakati wa Bunge la Awamu ya Kumi kama ni demokrasia ndiyo ilikuwa inapaa, lakini Bunge hili kama kweli tunatekeleza *practices* za *Commonwealth Parliament*, hili Bunge limeshusha kwa kiwango kikubwa sana demokrasia. Hili Bunge haina hata maana kuliita linafuata taratibu za *Westminster* kwa sababu Bunge hili ni Bunge ambalo linanyima uhuru wa mawazo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Nsanzugwako utanisaidia; Mabunge ya *Commonwealth* yanasema waruhusu wachache waongee, wengi wafanye maamuzi. Kwa namna yoyote ile sisi wachache hatuwezi kuzuia maamuzi yenu, lakini Bunge hili linazuia wachache kusema, linafanya maamuzi lenyewe. Katika historia Bunge hili limetoa adhabu kubwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mahali hapa kwa mujibu wa Katiba ni mahali penye uhuru wa mawazo ili tujenge Taifa letu. Lengo letu mawazo yanapokinzana, duniani kote dunia imeendelea kwa mawazo kiznani. Hili ndiyo Bunge limezuia... (*Makof!*)

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Alishakataza taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakasaka. Mimi nahesabu taarifa, zikishafika idadi fulani hata wewe nitasema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: *Mr. President.*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lema najaribu kukulinda ili usije ukapata taabu kwenye chama chako. Nadhani mko kwenye mchakato, sasa ukishamwita hapo *Mr. President*, usije ukaja kwa Mheshimiwa Spika kwamba mambo yamekuwa si mambo huko.

Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

TAARIFA

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimpe tu taarifa mzungumzaji, amezungumza hapa kwamba Bunge hili haliwapi kabisa nafasi ya walio wachache kusema, kwa maana ya kwamba walio wengi ndiyo wanasesma. Sasa sijui kidogo labda mhemko umemzidia maana ye ye mwenyewe ndiye anayesema hapo. Sasa sijui anaposema hawapewi nafasi ya kusema sijui ni ipi? Yeye mwenyewe anazungumza muda huu, labda aseme anafanya nini pale alipo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Kicheko/Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mch. Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mabunge ya *Commonwealth* wachache wanaongea, wengi wanafanya maamuzi. Nirudie tena, hata tuongee vipi upande huu, hakuna mnachokitaka ninyi kinaweza kuzuiwa, lakini mtusikilize. Bunge hili katika historia ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limezuia *speeches* zetu, zinakuwa-edited na Spika, zinahaririwa na Spika. Uhuru wetu wa mawazo hauzungumzwi hapa, halafu leo mnasema tumpongeze kwa kitu gani? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili limetoa adhabu kubwa sana. Hatujaja hapa kwa fadhila. Sijaingia Bungeni hapa kwa fadhila ya mtu, wananchi wa Jimbo la Iringa Mjini wamenileta hapa na wala sitegemei fadhila za mtu kurudi hapa. Kama sina *merit* sitarudi, kama nina *merit* nitarudi, hakuna atakayeizua. Nakuja hapa kuwasemea wananchi, nataka kusoma mawazo walionituma wananchi, Bunge hili linakataza, halafu leo mnasema tupongeze, tupongeze kitu gani? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge liliopita la Marehemu Mheshimiwa Samuel Sitta lilipeleka Wabunge wengi duniani kwenda kujifunza namna Mabunge ya *Westminster* yanavyofanya kazi. Tulikuwa na *democracy* inayokua ya

kuliendeleza Taifa letu, kwa sababu *democracy* siyo ugomvi. Hapa tumebakia tunashangilia kama mpira wa Simba na Yanga halafu tunapongezana.

Mheshimiwa Kitwanga hili azimio unampotosha Spika. Kama anafanya kazi nzuri litakuja Bunge lingine litasema. Ndiyo maana akina Marehemu Mheshimiwa Sitta tunawasema mpaka leo, hawakufanya wakati wao. Ndiyo maana akina Mheshimiwa Anne Makinda pamoja na kwamba tulibishana ...

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSINGWA: ...kuna mambo tunayosema leo kwa sababu walifanya kazi yao. Hatuwezi kujisifia wenyewe.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mch. Msigwa, kuna taarifa. Waheshimiwa Wabunge, hiyo itakuwa ni taarifa ya mwisho kwa Mheshimiwa Mch. Msigwa.

TAARIFA

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Azimio hili linampongeza Spika wetu kutokana na kazi nzuri katika Bunge hili la Kumi na Moja. Ndiyo maana katika Bunge la Kumi Mheshimiwa Mch. Msigwa alilidanganya Bunge na hatimaye akaomba msamaha kwa watu wa Iringa kutokana na kauli yake aliyokubali kwamba alilipotosha Bunge kwa kusema kwamba Kinana ni jangili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaoomba msamaha ni watu wenye nguvu. *Strong people ask for forgiveness. And strong people forgive. I am*

one of them. If you make mistake, you admit. Bahati nzuri yule niliyemwomba msamaha amesema mimi ni mtu muungwana, who do you think you are? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowea kusema, wajibu wetu hapa ni kuhakikisha tunasimamia mambo ya msingi. Hatujaja hapa kupigiana makofi. Mheshimiwa Ndugai, Spika wetu kama anafanya vizuri, vizazi vinavyokuja vitasema. Wengine hapa mnapongeza kwa kutaka *favours*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni Bunge ambalo lime-*cripple* demokrasia; ni Bunge ambalo limeua mjadala wa mawazo; ni Bunge ambalo limewatiisha watu wanaogopa kuzungumza; hapa ni mahala pa kuzungumza; *this is a place of dialogue*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnapotukataza tusizungumze, tukazungumzie wapi? Hili ni Bunge lime-*cripple* mazungumzo. Kwa bahati mbaya tunamaliza muda wake na wengi mnakuwa huko pemberi mnasema lakini pale hasira ilizidi. Huwa hamsemi ninyi? Halafu sasa hivi hapa mnasema tunapongeza, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hebu tuwe wakweli na tumwogope Mungu. Linganisheni Mabunge yote, hata wakati wa Bunge la chama kimoja la Pius Msekwa mambo yanayofanyika hapa hayakuwa hivyo. Ninayozungumza hapa siyo *personal*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *I respect you*, namheshimu Mheshimiwa Spika, lakini hili mmelileta hapa nami binafsi katika *record*, hili ndilo Bunge ambalo limeshusha heshima na hadhi ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimsikia *Chief Justice*, anaulinda mhimili wake kwa gharama zozote, anatetea Majaji wake, anatetea Mahakimu wake. Bunge hili Wabunge wanadhalilishwa. Mara ngapi hapa madeni ya Wabunge yametajwa huko barabarani. Nani ataheshimu Bunge barabarani huko? Wabunge wanatajwa hapa, wanafukuzwa watu mwaka mzima wanatoka Bungeni kwa kosa la kuongea, halafu leo hapa mnasema tupongeze! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *record* hiyo mimi sitaunga mkono azimio hilo. Nasema wazi bila unafiki, tutendee haki Taifa hili, hapa ni mahali pa mjadala kwa wale waliioututuma. Hili Bunge linatakiwa lilindwe kwa wivu. Huu ni mhimiili! *It is a holy place.* Asubuhi hapa tunasimama, "Eeh Mungu utusaidie tufanye maamuzi ya haki."

Mheshimiwa Naibu Spika, nikileta hotuba yangu hapa, peleka huko! Toka! *We are not schoolboys, we are leaders.* *We are treated like schoolboys here, we are leaders. Influence* imeenda mpaka mitaani. *We are not even respected huko barabarani!* *We are leaders!* Tumetumwa kuja hapa, halafu watu mnataka *favours* hapa, mnapongezana pongezana, *for what?* *For God's sake, for what?* Kwa lipi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *and this is not personal.* Narudia tena, *it is not personal.* Nazungumza kitu cha Spika, hakuna uhalali wowote wa kulipongeza Bunge hili. Bunge hili linatakiwa liwaombe msamaha Watanzania, hatujatenda haki ya kuwatumikia Watanzania. Hakuna uhuru wa mawazo hapa! *Freedom of speech* imekandamizwa kwa kiwango kikubwa katika Bunge hili.

La pili, hata mngekuwa *fair* Mheshimiwa Kitwanga ungetuunganisha kwenye hilo azimio lako, pamoja na...

MBUNGE FULANI: Hivi Mheshimiwa Msigwa na Mheshimiwa Lema wamepewa dakika ngapi?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Siyo hao tu, hata Wenyeviti basi mngeunganisha mwapongeze wote, kama mnataka hivyo ili wabebe msalaba wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowea kusema, *to cut the story short*, Bunge hili katika historia ya Mabunge lime-cripple uhuru wa mawazo ndani ya Bunge. Limezia speeches nyingi za Wapinzani, Bunge hili halijataka mawazo yasisikike, Bunge hili limekubali kwamba Serikali izuie hata mawazo ya Wabunge yasisikike kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mitano tumekuwa gizani, wananchi hawatusikilizi tunaongea nini ndani ya Bunge. Bunge hili lilkubali Bunge *Live life* halafu hapa mnasema tunapongezana. Kuweka *lift*; huo ni wajibu wake. Eti mtu anasema tunapongeza mmepitisha bajeti ya *Stiegler's Gorge*, mmepitisha *standard gauge*, kwani ile ilikuwa ni fadhila! Kuweka *internet* nalo tuanze kupongezana hapa, *seriously* kwenye ulimwengu wa *digital economy!* Kwani tulikuwa tunapitisha kwa fadhila! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ililetta mpango mzuri ambao una tija, Bunge litapitisha tu. Sasa inaonekana eti kutimiza wajibu wake tunapongeza, sasa kazi ya Bunge ni nini? Kazi ya Bunge ni kufanyaje hapa? Vimewekwa viti *canteen*, tunapongeza. *Are we serious?* Yaani Bunge tumekuwa *reduced to that level* kwamba tunapongeza *tablet, hii tablet!*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninyi ni mashahidi, wakati mimi ni Waziri Kivuli wa Mambo ya Nje nilikuwa nasoma na *IPodya Apple* hapa kabla hatujaanza wote hapa. Akina Elon Musk wanaenda angani sasa hivi huku tunapongezana na *tablets!* *Are we serious* Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? *The United Republic of Tanzania Assembly tunapongeza tablets;* mtu anatoa na povu tunapongeza *tablets.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme, hebu Wabunge tutendee haki Taifa letu. Kama mawazo yetu ni kupongeza *tablets* tunaingiaje kwenye *digital economy?* Tunaingiaje watoto sasa hivi wanasoma kwa *zoom nyumbani*, wanasoma wamekaa, *seriously!*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya Bunge linaisha, hebu tunyanyue *standard* ya Bunge. Tukinyanya *standard* ya Bunge na wananchi huko pemberi watanyanya. Tukishusha *standard* ya Bunge na wananchi huko watashuka. Kwa nini tunaongea vitu hivyo? *Let us think big guys*, hebu tuache hayo mambo.

Mheshimiwa Kitwanga unampotosha Spika wetu.

MBUNGE FULANI: Sana, sana, sana.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Unampotosha Spika wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili azimio niwashauri Wabunge wenzangu liondolewe, lisipitishwe, tuhakikishe tunaongea mambo ya msingi. Ni kweli kuna mambo mazuri ambayo Mheshimiwa Job Ndugai ameyafanya kama Spika, lakini siyo haya mliyoleta hapa. Haya tunatimiza wajibu wetu. Eti bajeti ilipitisha *Stiegler's Gorge*; kweli! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ufanuzi utatolewa hapo baadaye, lakini tusome vizuri hilo Azimio. Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, vishkwambi vimetajwa kama mfano. Ni mabadiliko ya kulipeleka Bunge kwenye Bunge mtandao. Kwa hiyo, lazima tuyaweke haya mambo vizuri. (*Makofi*)

Nilikuwa nimekwishamtaja Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Cosato David Chumi na Mheshimiwa Alhaj Juma Nkamia, ajiandae.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii, nami niweze kuchangia maazimio haya mawili yaliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru binafsi pamoja na Mwanasheria Mkuu kwa darasa zuri la Katiba ambalo mmelitoa kwa msemaji aliyemaliza kuongea muda mfupi uliopita. Ninyi wanasheria mna msemo wenu, kwamba haki si tu lazima itendeke bali pia haki ni lazima ioneckane inatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitakachokifanya hapa, na labda niseme mimi nitachangia tu azimio hili la

kumpongeza Mheshimiwa Spika wetu; nitakachokifanya mimi hapa si tu kumtendea haki Mheshimiwa Spika wetu bali ni kuionesha kwa maneno haki hiyo ambayo yeye anastahiki kuipata kutokana na kazi nzuri aliyolifanya Bunge hili kwa kipindi cha miaka hii mitano alichokuwa anatuongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, waswahili wanasesma usione vinaelea bali vimeundwa. Mheshimiwa Spika wetu huyu mpaka kufika hapa alipofika; na amesema vizuri Dokta Chegeni hapa; ukiiangalia historia yake kuanzia elimu, kazi zake na mpaka leo amekuwa mwanasiasa ambaye ni kiongozi wa mhimili basi ametoka mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi tu ukiangalia *CV* ya Mheshimiwa Spika wetu, mionganoni mwa shule alizopita ni pamoja na Shule ya Sekondari ya Kibaha, na kila mmoja anafahamu kwamba ni shule ya vipanga. Kwa hiyo Mheshimiwa Spika wetu amepata elimu hiyo katika Shule ya Sekondari ya Kibaha ambayo pia Mheshimiwa Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete amepita pale. Hata hivyo pamoja na hayo yote pamoja na kupata diploma yake pale kwenye kile chuo cha Mweka, baadaye na kupata *degree* yake ya kwanza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na *masters* kule Norway, lakini pia wengi pengine hawafahamu kama Spika wetu pia ni mwanasheria; ana *degree* ya Sheria ya Chuo cha *Open University* cha Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kuweka hili jambo katika muktadha mwema, wengi hapa wamezungumza utendaji wa Mabunge yaliyopita, hususan lile Bunge la tisa ambalo lilikuwa linaongozwa na marehemu mzee wetu Mzee Samuel Sitta.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nimefanya kautafiti kadogo na katika kupekuapekua kwangu nimekutana na gazeti la *Daily News* la mwaka 2010. Gazeti la terehe 09 Oktoba, baada ya kuwa Bunge lile limeshamaliza muda wake ulipofika unakaribia uchaguzi kuna taasisi inaitwa Uwazi Twaweza walifanya utafiti wa *on line* wakaja na *findings* zifuatazo, wakati ule, hilo Bunge ambalo linasifikasi Bunge la

tisa la Mheshimiwa Samuel Sitta. Walikuja na *findings* zinasema Mheshimiwa Job Youstino Ndugai ndiye alikuwa *the most active Member of Parliament* wa Bunge la Tisa. Kinachoongea ni takwimu si maneno yangu ni maneno ya watafiti. Katika utafiti wao wamekuja na takwimu zifuatazo; kwanza wanasema Mheshimiwa Spika Ndugai katika Bunge lile alifanya *interventions* 376 kwa maana ya maswali, michango, swali la nyongeza na vitu kama hivyo, miongozo, 376. Akauliza maswali ya msingi 29, akauliza maswali ya nyongeza 60 na akafanya michango mingine mbalimbali zaidi ya 287.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utafiti wao wakasema huyu ndiye *the most active Member of Parliament* wa Bunge la Tisa, Bunge la Mzee Samuel Sitta. Sasa ili kuweka hili jambo katika muktadha mwema zaidi aliyekuwa wa pili kwenye utafiti ule ni Mheshimiwa dada yetu mpendwa sana Jenista Mhagama kwa mujibu wa utafiti ule. Na aliyekuwa wa tatu ni Dkt. Wilbroad Slaa, wa nne ni aliyekuwa Mheshimiwa Godfrey Zambi na wa tano alikuwa Mheshimiwa Zitto Kabwe. Nimeyasema hayo ili kuweka sawa tu, kwamba huyu mtu ambaye leo tunamuenzi kwa kumpongeza hii kazi aliifanya tangu akiwa *back bencher*, hajawa Naibu Spika, akiwa Mbunge wa kawaida tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nilichangia hapa siku mbili tatu zilizopita, *last week*, kuelezea namna gani Mheshimiwa Spika wetu alivyoilea na kuipa meno ile Kamati ya Sheria Ndogo. Katika moja ya mambo ambayo tuliyaona, kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ni kwamba ile Kamati ilipokea aina sheria ndogondogo na kanuni zaidi ya 2,601. Katika ya hizo 547 zikafanyiwa marekebisho kutokana na dosari mbalimbali. Hii maana yake ni kwamba kuna mambo 547 ambayo katika hali ya kawaida pengine yalikuwa ni vikwazo na kero kwa wananchi wetu vikaweza kurekebishwa. Haya ni matunda ya Mheshimiwa Job Yustino Ndugai. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye eneo la hadhi na heshima ya Bunge, yamesemwa mengi hapa, kwamba

Mheshimiwa Spika amenyanya hadhi ya Bunge hili. Mimi sitaki kuyarudia yale ambayo waliyazungumza wenzangu, lakini nitazungumza moja tu. Tulipopata mtihani hapa wa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Ndassa, *Senetor*, ninakumbuka na ninamnukuu Spika alisema, ndicho kipindi tulikuwa katikati ya tatizo lile la *pandemic* ya Corona. Mheshimiwa Spika akasimama kwenye Kiti hicho akasema, tukafanya kila linalowezekana kwamba mpendwa wetu huyu aende akazikwe nyumbani kwao, wakati ule wengi wa waathirika wa tatizo lile walikuwa wanazikwa katika mazingira ambayo hayakuwa ya staha zaidi, na kweli lile likatendeka. Kwa hiyo, tunamshukuru sana na tunampongeza sana Mheshimiwa Spika kwa kulinda hadhi ya Bunge na Wabunge wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine Mheshimiwa Spika wetu huyu ni msikivu. Hata Wabunge tulipokuwa tunalalamika hapa wakati ule wa kusafiri na mabasi ya coster akasema basi tutabadilisha mtakwenda na mabasi yenye hadhi ambayo mnaihitaji baada ya kuambiwa akakubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Spika wetu yuko karibu na Wabunge. Mimi binafsi tulipata bahati siku moja tukaalikwa kwenda kushiriki kwenye sherehe ya usomaji wa *Quran kule Kijiji* kimoja kinaitwa Pahi, Kondo huko; Spika wetu akaenda tukakaanaye mpaka saa 05:00 usiku. Kwakweli alionesha ile *humility* tumekaanaye chini, tukalanaye pale na tukashiririnaye mpaka saa 05:00 usiku baadaye akarejea nyumbani kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile imezungumzwa hapa dhana ya kubana matumizi na mengi na takwimu zimetolewa, lakini mimi nataka nisisitize kwenye takwimu moja tu. Kwamba ikiwa bajeti ya Bunge ya 2015/2016 ilikuwa ni bilioni 173, lakini bajeti hii tunayokwendanayo ni bajeti ya shilingi bilioni 121, ameweza kubana matumizi na kwenda sambamba na dhana ya Mheshimiwa Rais ya kubana matumizi na kuhakikkisha kwamba, matumizi ya Serikali yanadhibitiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia mambo madogo mawili; Mheshimiwa Spika wetu huyu ni mwanamichezo mzuri. Na mwenzangu alikuwa ananinong'oneza hapa ananiambia inawezekana labda sijui hivi viti vya Bunge hili vina rangi nyekundu, lakini labda pengine inatokana na dhana ya Spika wetu naye pia, kuwa ni shabiki wa timu ya Msimbazi. Sina uhakika sana na hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema; nilianza kwa kusema kwamba usione vinælea vimeundwa. Mheshimiwa Spika amefanya haya yote, lakini kwa kiasi kikubwa sana ni kutokana na usaidizi wako wewe Mheshimiwa Naibu Spika, usaidizi wa Katibu wetu wa Bunge pamoja na wenyeviti mmeweza kwa pamoja kuliendesha gurudumu hili na mmeweza kulipa hadhi na heshima ya Bunge ambayo tunazungumza hapa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kukushukuru kwa nafasi hii na ninaunga mkono maazimio yote mawili haya yaliyoletwa mbele yetu. Nakushukuru sana, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa David Cosato Chumi, atafuatiwa na Mheshimiwa Alhaji Juma Nkamia, Mheshimiwa Sonia Juma Magogo ajiandae.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe shukrani zangu za dhati. Kwakweli kama nilivyo sema siku moja sijutii kuwa Mbunge wa Mafinga Mjini, *I am enjoying this job* na ninafurahia kwa sababu ya ushirikiano na miongozo mbalimbali ambayo ninaipata kutoka kwa kiongozi wetu wa mhimili huu pamoja na wewe unayemsaidia na maafisa wote wa Bunge na wenyeviti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze kwa kusema, kuna baadhi ya wenzetu, nikianza na utangulizi, hususan kuhusu Azimio hili la Makao Makuu kuwa Dodoma. Mmoja wa wachangiaji amejaribu kuelezea jinsi ambavyo Dodoma

inajengwa na kwamba, haoni kwamba, inaendana na *standard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka nimsaidie tu, sisi wengine Mwenyezi Mungu bahati nzuri ametubariki tumezunguka duniani, sio kidogo, tumezunguka miji mingi sio kwa nguvu zetu kwa neema ya Mwenyezi Mungu. Kila mji unavyojengwa unajengwa uki-reflect hali halisi na tamaduni za watu wa maeneo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda leo *The Hague* haiwezi kuwa sawa na Tel Aviv, ukienda Tehran haiwezi kuwa sawa na Washington DC, kadhalika ukienda London haiwezi kuwa sawa na Abuja kwa hiyo, hatuwezi ku-*copyna* ku-*paste* kila kitu. Sisi lazima tuendeshe mambo kwa mujibu wa utaratibu na tamaduni zetu wenyewe. Kwahiyo maono yake yanaweza kuwa sahihi kwa sababu ya kupenda ku-*copyna* ku-*paste*, lakini apende kufahamu pia kwamba, kinachojengwa hapa *is a capital city is not a commercial city*. Hii sio Dar es Salaam hii ni *capital*, ni makao makuu ya Serikali na ndio maana ukienda Brasilia huwezi kukuta ikawa sawa na Sao Paulo kwa wa hiyo, niliona niseme hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili katika Azimio la Kumuunga Mkono Mheshimiwa Spika wetu. Watu wanazungumzia vishikwambi, unajua unapozungumza kwanza lazima ni vizuri uwe na takwimu halafu uweze ku-*quantify* hizo takwimu. Sasa mimi nataka niwaambie Watanzania na Wabunge wenzangu, kutumia hivi vishikwambi, yawezekana kweli kila mtu alikuwanacho kwa nafasi yake, lakini kama Serikali na Bunge kwa kutumia hivi si kwamba, ni burudani hapana, kuna kitu ambacho tumeokoa, tumeokoa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hapa imesema tumeokoa zaidi ya bilioni 104 kwa kwenda Bunge Mtandao. Sasa labda twende na takwimu na tu-*quantify* hizi takwimu. Kwa mfano, nitatoa tu katika maeneo matatu; fedha hizo tungeweza kujengea vituo vya afya hivi ambavyo tumejenga 208. Maana yake kwa kutumia hiki kitu tunaweza kujenga

vituo vya afya 208, si kitu kidogo *is not a luxurious thing*. Hivyo unapokosoa jaribu kuwa na takwimu na kufanya *quantification*, sasa najaribu kuwaambia kisayansi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tungeweza kujenga madarasa 5,200 ambayo kama zingekuwa sekondari tungejenga sekondari na tunaweza maana yake kujenga sekondari tukitaka kutokana na kuokoa gharama hizo, sekondari 370 kwa ajili ya watoto wa taifa hili, lakini kama zingekuwa ni shule za msingi tunaweza kujenga kutokana na kuokoa kwa kutumia kidude hiki, shule 520 za msingi. Kama ni hospitali kama hizi ambazo tunajenga tungeweza kujenga hospitali 26. Ndiyo maana ya kazi ya Mbunge, kushauri na kuisimamia Serikali tumeshauri na Mheshimiwa Spika akaitika tunatumia vishkwambi tumeokoa fedha ambayo inaenda kufanya kazi kadha wa kadha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda katika barabara tungeweza kujenga barabara zaidi ya kilometra 130 za lami. Kwa maana kama kule Mafinga tungejenga barabara ya kutoka Mafinga mpaka Mgololo, ingeharakisha uchumi wa Watanzania na kuongeza mapato. Tunaposema vituo vya afya maana yake kwamba, kule Bumilayinga tunaweza sasa kujenga kituo cha afya na wananchi wakapata huduma kwa ukaribu. Kwahiylo wakati mwingine tunapochangia humu kama Wabunge ndugu zangu tujaribu kuonesha maana halisi ya uwakilishi kwa kuwaonesha wananchi kwamba tunapoleta maazimio kama haya hatuleti kujfurahisha bali kuna vitu ambavyo vimefanyika na vitafanyika kwa ajili ya kurahisisha maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuhusu hili la kutobadili uamuvi wa Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi. Kwa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi maana yake ni nini;

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza inarahisisha shughuli mbalimbali za utendaji wa Serikali. Ile tu kuwa katikati leo hii afisa wa Serikali au mtu ye yeyote anaweza kuja Dodoma wastani wa saa nane akaja kufanya shughuli zake. Na hapa

ninaweza kuonesha mtu anaweza akatoka Tanga, ni wastani wa kilometra 505, kutoka Bukoba ambako ni mbali kidogo wastani wa kilometra 529, kutoka Songea wastani wa kilometra, kutoka Kigoma wastani wa kilometra 790 au kutoka kwetu Iringa wastani wa kilometra 261. Maana yake ni nini, tunarahisisha utendaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hivyo tu, miji iliyo karibu kibiashara, leo hii kutoka Iringa kuja Dodoma kuna gari kila baada ya nusu saa, ukianzia saa 12:00, 12:30, saa 01:00, saa 01:30 na kuendelea mpaka saa 03:00 usiku kati ya Dodoma na Iringa. Maana yake ni nini, umerahisisha *movement*, lakini *at the same time* hizi *movement* watu watajaza mafuta, Serikali itapata *fuel/levy*, tutaenda kujenga zahanati, tutaenda kujenga barabara, tutaenda kujenga shule za watoto wetu. Kwa hiyo na mimi naunga mkono jambo hilli kwa dhati kabisa, azimio hilli kwa sababu, linaenda kurahisisha utendaji wa Serikali na kwa maana hiyo, kurahisisha maisha ya Watanzania wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuhusu azimio la kumpongeza Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika alikuwa na uthubutu akaunda kamati maalum. Mimi nilikuwa mmoja wa Wajumbe wa Kamati Maalum ya kuangalia uchumi wa bahari kuu (*blue economy*) na tumeona matokeo yake kuna sheria zimekuja zimeundwa. Kuna kamati kama zile za masuala ya madini, leo hii tumejenga ukuta Mererani, kuna nchi zilikuwa zinaongoza kwa kuuza madini ya *tanzanite* wakati sisi ndio wazalishaji; na ndio maana sasahivi kuna watu wengine wame-*panic*, majirani zetu na wanajaribu kuleta figisu za hapa na pale kwa sababu, hakuna tena wanachonufakanacho, lakini ni matokeo ya zile kamati ambazo Mheshimiwa Spika alizindua. Kwahiyo tunapoleta azimio tunaleta azimio kuna vitu *tangible* vinavyotusababisha tulete azimio sio kwamba, tunaleta tu kujifurahisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naunga mkono maazimio yote mawili, na kwakweli nayaunga mkono kwa hoja ambazo nimezitoa za kitakwimu na pia nimezi-

quantify za kisayansi sio bla-bla. Naomba kuunga mkono maazimio hayo na Mungu awabariki sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Alhaji Juma Nkamia, atafuatiwa na Mheshimiwa Sonia Juma Magogo, Mheshimiwa *Engineer Amandus Ngonyani* ajiandae.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye maazimio mawili yaliyopo mbele yetu. Kwanza nikupongeze wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, lakini pia niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wajukuu zetu hawa wawili Mabula na Kitwanga kwa kuleta maazimio haya mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hili azimio la kwanza, kwanza nataka niweke *point clear* maamuzi ya Serikali kuhamia Dodoma hayajafanywa na Rais Magufuli, yalishafanywa toka mwaka 1973, alichofanya Rais Magufuli ni kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi iliyomwelekeza kwamba Serikali ihamie Dodoma. Azimio hili linalositisiza ni kwamba asije akatokea mtu mwingine kesho tena akaja akasema Makao Makuu ya Serikali Chemba, inawezekana, au Iringa kule kwa Mheshimiwa Msigwa au Arusha anapotoka Mheshimiwa Lema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika hapa ni Azimio la kusisitiza kwamba yasijeyakafanyika tena maana yake hata Mobutu aliwahi kufanya, akapeleka Makao Makuu kule Badoliti. Kwa hiyo, kinachofanyika hapa ni kusisitiza tu, lakini nani mwenye wajibu wa kulismamia hili ni Bunge hili lenyewe, kwa sababu ukiwa na Bunge legelege, akaja Nkamia akasema napeleka Makao Makuu ya Serikali Chemba na nyie mkaunga mkono, siyo kosa lake ni kosa la Bunge. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichofanyika hapa alichofanya Dkt. Magufuli ni kuonesha tu ile *integrity, commitment, confidence* na *creativity* kutekeleza yale

yaliyofanyika mwaka 1973, katika Mkutano wa 16 wa Chama cha *TANU*. Maamuzi yale yalifanyika kidemokrasia, mikoa yote ilishirikishwa Bara na Zanzibar, Mkoa uliokataa ni Pwani peke yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kweli kwamba Dodoma ni Makao Makuu ya Nchi, yapo mengi yanafanyika, barabara zinajengwa; mimi nimetembeatembwa nchi nyingi kidogo duniani, inatakiwa sasa hawa watumishi wa Serikali wawe wabunifu kuona namna gani Mji huu kweli utaonekana una hadhi ya Makao Makuu ya Nchi. Si rahisi uko kwenye ndege ukifika Kisasa bati hili la kijani, linalofuata la bluu, linalofuata jeupe, inayofuata ninyumba ya udongo, haiendi hivyo. Sasa kama Serikali imefanya maamuzi, hao wanaosimamia sasa Manispaa na Jiji ndiyo wanatakiwa waoneshe kweli hapa ni Makao Makuu ya Nchi yetu. Hili naamini wale wahusika wanaweza wakalichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Azimio hili la Kumpungeza Mheshimiwa Spika. Kwa uelewa wangu mdogo tu ni kwamba hatumpongezi Mheshimiwa Job Yustino Ndugai *as a person*, tunampongeza Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayiteitwa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai. Unapomngeza Spika unampongeza Naibu Spika, Katibu wa Bunge na wafanyakazi wote wa Bunge hili; huwezi kuwataja majina wote ila unataja yule kiongozi wao ambaye ni Mheshimiwa Job Yustino Ndugai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukifika hapa ukasema Mheshimiwa Ndugai hajafanya kitu unamu-*attack as a person*, ni makosa...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juma Nkamia kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Nkamia

kwamba, anadanganya kwamba Azimio hili ni kuwapongeza Ofisi ya Spika pamoja na watumishi wote wa Spika, lakini ukweli tu ni kwamba uksoma Azimio linasema kwamba ni Mheshimiwa Spika Job Ndugai. Kwa hiyo, nafikiri angeweza kunyoosha tu aeleze madhumuni na madhumuni ya Azimio hili, lakini siyo hiki ambacho anakizungumza sasa hivi hapa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwakajoka rafiki yangu, kuna vitu vingine huhitaji kuwa na *degree* kuelewa, unaweza kuwa na elimu ya kawaida kama ya kwangu. Nilichosema Azimio hili nila kumpongeza Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anayeitwa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, sijasema kwamba Azimio hilli linampongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa; ni suala la uelewa tu. Sasa ukizungumza kama upo kwenye *club* ya pombe *is wrong, a good listener is a good speaker*; wakati mwingine kukaa kimya nayo ni bora zaidi kuliko kuzungumza ovyoovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili linaloongozwa na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa ambaye ni Spika yapo mambo makubwa sana limefanya. Hata Mheshimiwa Mwakajoka leo pale anayecheka amefaidika na uongozi wa Mheshimiwa Ndugai. Ni kipindi ambacho tumeona Bunge hili likijisimamia. Mimi ukiwa unaongea yaani kilevilevi namna hiyo naweza nikakupa maneno ya ajabu sana, *so be patient* yaani unazungumza na *wrong figure...*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa...

MHE. JUMA S. NKAMIA: Kwa hiyo, ninachotaka kusema...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nkamia ongea na mimi maana hutamaliza mchango wako kwa mtindo huo...

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivyo kwa sababu na wewe umewaachia pale wanazungumzazungumza ovyo...

NAIBU SPIKA: Zungumza na mimi kwa sababu mimi nasikiliza Bunge zima hata wewe wakati unazungumza muda fulani sikukutaja nilikuacha kimya; mimi naangalia Bunge lote. (*Makofi*)

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni anaweza kuwa na mapungufu yake kama binadamu, lakini tunapima faida na hasara alizozifanya, ni imani yangu kwamba Mheshimiwa Ndugai amefanya kazi kubwa sana ya Bunge hili. Kuna watu wamekuja kutolea mfano hivi vishkwambi hapa, hii siyo *concept, conceptni* kukata *cost, though* kwa wachumi wanaweza kwenda *in a different way*, sitaki kuingia huko ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi hapa Mheshimiwa Msigwa ameonesha pale kwamba ameanza kutumia hapa alipoanza kusoma hapa, mimi nilishaanza kutumia toka 1995 nilipoajiriwa pale Redio Tanzania. Hii siyo kwamba eti hii ni sifa kubwa sana kwamba unakuja hapa unasema eti Mheshimiwa Ndugai ametuletea tu hiki, hapana tunaangalia *cost* aliyokata, je ile fedha sasa itumike kwenda huko kwenye *society* ikalete mafanikio, hicho ndicho tunachozungumza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema jambo moja tu, kuongoza watu ni kazi ngumu sana hasa watu wenye kaliba tofauti, tunahitaji kuvumiliana, kuheshimiana na mbaya zaidi Azimio hili limekuja kipindi kibaya sana, kipindi ambacho kila mtu, wengi wetu hapa wana mihemko, hawaelewi wapo au hawapo, hawajitambui baada ya Oktoba watakuwa wapi, wanarudi kwenye kazi zao za zamani za kuhubiri Kanisani au watarudi kwenye kazi zao za zamani za vichochoroni kule Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.
Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer Amandus Ngonyani*, Mheshimiwa Asha Abdallah Juma ajiandae.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hizi zilizopo mbele yetu. Kwanza kabisa naomba nianze kwa kusema kwamba natambua imani yangu ambayo inasema binadamu hawesi kuwa mkamilifu kwa asilimia mia moja bali Mwenyezi Mungu peke yake. Kwa kulisema hilo natambua kwamba Mheshimiwa Job Ndugai ni binadamu, kuna sehemu alikuwa anateleza kama mwanadamu lakini kuna sehemu ambazo alikuwa akifanya kazi zake kwa uadiliflu na kuleta matunda kwa Bunge letu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kumwelezea Mheshimiwa Job Ndugai kama ni Spika ambaye kwa kweli alikuwa ni msikivu, alikuwa na ubinadamu, upendo na kujali lakini alikuwa pia ni jasiri na mtu ambaye hayumbishwi. Nikija kwa upande wa kwa nini nasema alikuwa ni mtu mwenye upendo na mwenye kujali... (*Makofii*)

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sonia Magogo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Rashid Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, samahani nataka tu nimsahihishe dada yangu anayeendelea kuzungumza anatumia neno alikuwa, sasa ningemnyoosha tu kwamba kwa sababu bado yupo ni vizuri angeweka kama inavyotakiwa kuwa. Ahsantesana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sonia Magogo.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea hiyo taarifa kutoka kwa kaka yangu, ahsante kwa kunisahlhisha. Niseme kwamba amekuwa badala ya alikuwa, nazungumzia tangu huko mpaka sasa hivi kwa sababu sijui ya kesho, sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema kwa nini ana ubinadamu na kujali, Wabunge wengi humu ndani kiukweli tumepitia changamoto nydingi sana katika kipindi hiki chote ambacho tumekuwa Wabunge. Nikitolea mfano wa mimi mwenyewe, nilipitia kwenye changamoto ya maradhi, lakini niliuona ubinadamu wa Mheshimiwa Spika kwa namna alivyokuwa karibu na familia yangu. Si mimi tu, ni wengi humu ndani watakuwa ni mashahidi ambao walipitia hizo changamoto mbalimbali siyo za maradhi tu, changamoto tofautitofauti inaweza ikawa ni Jimboni ama za kifamilia, zozote zile alikuwa yupo tayari kukusikiliza na kuweza kukusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naweza kusema kwamba alikuwa jasiri kwa sababu sisi binafsi kwenye chama chetu tumekuwa na mgogoro na ule mgogoro tunajua ni kiasi gani ungeweza hata kusababisha chama chetu Kikaondoka kwenye *system*,lakini Mheshimiwa Job Ndugai alisimamia ile haki iliyohitajika na mpaka ikafikia kipindi kuna Wabunge walitakiwa kuondoka na sisi tukaingia, tukaapishwa. Hilo linathibitika kwamba alikuwa anatunza ile nidhamu ya vyama vya siasa,kwa sababu mpaka leo ninavyozungumza hapa wale Wabunge ambao waliondoka walikuwa wanaleta matatizo kwenye chama chetu hatupo nao. Kama wangeendelea kukumbatiwa na kubaki kwenye chama chetu ina maana tungepata athari kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, pia ameonesha ujasiri mkubwa sana kipindi cha *corona*. Ugonjwa huu ulipoingia zilitokea changamoto nydingi sana na moja ya kitu ambacho kingeleta hata tataruki kwa wananchi wetu ni kitendo cha kusema kwamba Bunge lifungwe, lakini Mheshimiwa Spika alisimama imara, shughuli za Bunge

zikaendelea na hata ile iliwapa imani wananchi kule ya kuwa na ujasiri wa kuendelea na shughuli za kujenga nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo Mheshimiwa Spika amesimamia marekebisho mengi sana ya sheria ambazo zile sheria kama zingebaki vilevile zingekuwa na athari kubwa kwa wananchi lakini kwa kuwa Mheshimiwa Spika alikubali zile sheria zikaja hapa ndani zikafanyiwa marekebisho, hivi leo kuna athari ambazo zingeweza kutokea kwa wananchi zimeweza kuzuilkia. Kwa hiyo, hii inaonesha pia ni kiasi gani Mheshimiwa Ndugai anajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nikupongeze na wewe kwa sababu pamoja na yote ambayo alikuwa akiyafanya Mheshimiwa Spika alikuwa akipata msaada mkubwa sana kutoka kwako pamoja na Katibu wa Bunge na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa hoja ya Makao Makuu Dodoma. Ni jambo la busara sana na nilipongeze Serikali kwa maamuzi ya kuweka rasmi kwamba sasa Makao Makuu ya Nchi yetu yaweze kuwa *in practice*, naweza kusema sijui, *sorry* lakini pamoja na hilo bado tunashuhudia kuna changamoto nyingi sana. Kwa mfano, maeneo mengine kama Ipagala, Swaswa na llazo ni maeneo ambayo tayari yamejengeka vizuri lakini miundombinu ya kule hasa barabara zake ni mbovu sana, ikifika kipindi cha mvua maeneo yale inakuwa hata wananchi kufika kwenye nyumba zao ni tatizo. Hivyo, niombe pamoja na kusema kwamba kuhamia Dodoma limekuwa ni jambo jema lakini Serikali iharakishe uboreshaji hasa wa miundombinu ambayo ndiyo chanzo na kichocheo kikubwa cha maendeleo na kivutio cha kuwafanya watu waendelee kujenga Dodoma. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, nimalizie kwa kuwashukuru watendaji wote wa Bunge ambao tulikuwa nao kwa kipindi chote, ambao walitupokea hapa Bungeni

na walitusaidia kwa namna moja ama nyingine kuweza kuyakamilisha majukumu yetu. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA:Ahsantesana Mheshimiwa *Engineer Amandus Ngonyani* atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma na Mheshimiwa Zainab Matitu Vullu ajiandae.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na muda huu kuweza kuchangia katika Bunge lako Tukufu hususan Maazimio haya mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utakuwa umeshaangalia hapo mimi nimeshapiga kura, nimeunga mkono Maazimio yote mawili. Natumia fursa hii kuelezea kwa nini nimepiga kura ya kuunga mkono Maazimio hayo mawili. Kwanza nikianza na Azimio la Makao Makuu ya Nchi yabakie Dodoma na yasiweze kubadilishwa na Serikali, taasisi au mamlaka nyingine yoyote ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichanganyikiwa kidogo niliposikia mchango uliohusu sheria tulioipitisha kuhusu Makao Makuu kuwa Dodoma kwamba ilivunja Katiba, nilishtuka sana. Nililazimika kuisoma Katiba yote na nilipofika kwenye ibara ya 98(1)(b) nimekuta yake mambo nane ambayo yameelezwa kwamba hayaruhusiwi kubadilishwa bila *two third majority* kutoka Zanzibar na Bara. Namshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali alinifuliza na ule mshituko na kwa kweli niliposoma ile namba mbili kati ya yale nane, kuwapo kwa Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano nilikuwa na wasiwasi kwamba kwa sababu kule Namtumbo tuna Ofisi ya Rais na kwa kifupi tunaiita ikulu ndogo ipo pale Namtumbo ni Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kweli nimepita kila mkoaa kuna Ofisi ya Rais sasa tunaposema Dodoma hapa kuileta Ofisi ya Rais tunachanganya na Makao Makuu na kwenye orodha Makao Makuu haipo kidogo ilinipa shida lakini nashukuru Mwanasheria Mkuu umeliweka vizuri hilo. Tunaongelea Makao Makuu hatuongelei Ofisi ya Rais, na

Makao Makuu haijaelezwa katika katiba nimepitia vifungu vyote nya katiba hakuna mahala ambapo katiba imesema Makao Makuu ni Dar es Salaam na wala Makao Makuu ni Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepitia sheria ya kusema makao makuu sasa ya nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yawe Dodoma sheria hiyo imepitishwa na sasa tunalipitisha hili azimio na naomba Wabunge wote tuungane tulipitishe hili azimio ili tulipe uzito na ikiwezekana nikuombe Mwanasheria Mkuu wa Serikali tutakapofanya mabadiliko ya katiba au tutakapofanya marekebisho madogo ya katiba tulilete na hili ili tulipe nguvu zaidi. Na ikikupendeza tutafute namna ya kuliweka kwa namna ambayo kama kuna marekebisho yatakayofanyika ya Makao Makuu ya nchi yawe wapi basi yaungwe mkono na *two third* ya Wabunge wote wa Bara na *two third* ya Wabunge wote wa Zanzibar ili tulipe ugumu zaidi wa kufanya mabadiliko ya aina yoyote katika eneo hili la Makao Makuu ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru uamuzi huu ulitolewa mwaka kama walivyosema wenzetu mwaka 1973 lakini utekelezaji umekamilishwa na Serikali Awamu ya Tano, na hivi sasa tunaposema tayari Dodoma ni Makao Makuu ya Serikali na Makao makuu ya nchi. Kwasababu makao makuu siyo majengo, makao makuu siyo barabara wala makao makuu siyo uzuri wa mji. Makao Makuu ni mahala ambapo huduma za kiserikali zinatolewa hata kama kungekuwa na miembe tu tunatolea kwenye miembe bado hapo ni makao makuu tunachoongelea ni huduma za Serikali Kuu zinakotolewa makao makuu na tunataka yawe hapo Dodoma majengo na vingine vyote vitafuata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza uamuzi uamuzi umefanyika watu wamekuja na sasa Serikali iko Dodoma mengine yatafuata na ninauhakika kwa namna nilivyoiona ramani ya makao makuu Dodoma ambao Mheshimiwa Bura aliongelea na bahati nzuri nimeiona kwa kweli hakutakuwa na makao makuu mengine ya nchi yoyote ya Afrika mazuri kuliko Dodoma. Ninauhakika ile ramani itafuatwa na vijana

wetu wa Jiji la Dodoma wako makini sana kuhakikisha hakuna kitu kinachojengwa au kinachofanyiwa kazi kinyume na mpango ule kabambe wa ujenzi wa makao makuu ambayo yatakuwa ni namba moja kwa Afrika nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii vilevile kwasababu inawezekana nisipate muda wa kuongea kwa kweli nichukue fursa hii kuwapongeza sana tena sana Serikali ya Awamu ya Tano mmetupa heshima kwa kuyaleta makao makuu hapa Dodoma kimatendo uamuzi ulifanyika mwaka 1973 lakini nyinyi ndiyo mmehakikisha hilli limefanikiwa na bila uwoga wowote sifa zimwendee Dkt John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliolisimamia hili kwa nguvu sana na aliiitikiwa kwa haraka sana na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa ambaye aliwahi kuhamia kabla hata muda aliopangiwa hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na ullonyesha njia na wengine wote wakafuata kwa hiari ama kwa lazima. Nikupongeze sana Waziri Mkuu kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kwa kiwango kile kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini aliyefuatia katika hilo ni Spika wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania aliruhusu na kwa kweli yeye ndiye aliyetoa kauli ya kwanza Serikali leteni Muswada wa kuhakikisha makao makuu tunaitengeneza inakuwa hapa Dodoma ni yeye aliyetoa kauli kwa mara ya kwanza kama mnakumbuka baada ya hapo ndiyo Serikali ikafanya hiyo kazi ikaleta Muswada. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Job Yustino Ndugai kwa kweli yeye binafsi ametusaidia sana kulitekeleza hilo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Ahsante sana kama nilivyosema nimepiga kura yangu ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Asha Abdullah Juma atafatiwa na Mheshimiwa Zainab Matitu Vullu, Mheshimiwa John Heche ajiandae

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nashukuru kwa nafasi hii adhimu ya kuweza kusimama hapa mbele kukiri kuunga mkono maazimio haya mawili. Azimio la kwanza la kukamilisha makao makuu wa Dodoma na kudhibiti pasitokee mtu yelete au mamlaka yoyote ya kutengua jambo hilo. Azimio la pili ni kumpongeza Mheshimiwa Spika Job Yustino Ndugai kwa jinsi alivyoweza kutekeleza kazi zake akiwa kama Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa nampongeza Rais Dkt. Magufuli alivyosimama kidete kukamilisha kijumla makao makuu kuhamia Dodoma azma ambayo iliasisiwa na hayati Rais wa kwanza Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1973. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Dodoma ni katikati ya nchi na katikati ni pazuri sana Dodoma kwa kuwa katikati ni Dodoma kusogeza huduma katikati kutafikia mikoa mingi kutapanua uchumi na ustawi kutaongeza tija na ufanisi katika maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza sana hatua za Rais wetu Magufuli hizi za hivi karibuni za kuongeza majengo ya Ikulu pale Chamwino na kuweka na kutanua uwezekano wa bustani kubwa ambayo itakuwa na wanyama bustani yetu wananchi wa Tanzania ili kuipa hiba Ikulu Chamwino. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za dhati pia kwa kuhamisha shughuli za Serikali wa mji wa Serikali wa Dodoma wa Mtumba. Katika hili sinabudi pia kumpongeza Waziri Mkuu na timu yake nzima kwa jinsi walivyosimamia ujenzi wa mji wa Serikali wa Mtumba. Bunge liko hapa Dodoma limekuwa likipanua shughuli zake na majengo muhimu yote yamefanyika tumeona pia upanuzi wa hospitali na maabara na kila kitu hapa hapa kwenye maeneo ya Bunge Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria mbalimbali zimeweza kutungwa hapa Dodoma, tena kwa ufanisi majengo ya kupendeza yamejengwa katika mji wa Dodoma yakiwa na

hiba ya kiserikali na yale ya watu binafsi kwasababu tumeweza kuona sehemu nyingine kwa sisi tuliobahatika kupidia Bunge hili hili kwenda mijji mingine ambayo yameigiza hapa Dodoma, kama kule Abuja lakini majengo yetu sisi naona ni mazuri zaidi kuliko hata ya Abuja. Kwa hivyo tutafika na tutaendelea kung'ara katika medani yetu ya kisiasa. Naunga mkono azimio hili kwamba pasijetokea mtu au mamlaka yejote ya kutengua makao makuu kubakia Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la Pili, nisimame kwa heshima na taadhima kubwa kumpongeza Spika Job Yustino Ndugai kwa jinsi alivyoendesha na kusimamia shughuli za Bunge la Kumi na Moja kwa ufanisi mkubwa. Mheshimiwa Spika huyu ameonesha mashirikiano makubwa kwa utendaji kwako wewe, wenyeviti na shughuli zote za kuendesha Bunge zimeendeshwa kwa vizuri sana. Mheshimiwa Job Yustino Ndugai ameonesha mashirikiano kwa kamati zetu kwa kufanya kazi zetu kwa ufanisi tena bila vikwazo. Kupitia mashirikiano hayo tumeweza kutunga sheria na kurekebisha za kutosha kama haja ilivyo stahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika huyu ametuwezesha pia kuwa na Bunge mtandao kupunguza gharama zilizotumika awali hasa kwa uzalishaji wa nyaraka. Bunge limeweza kuokoa fedha nyingi sana ambazo zinatumika kwa maendeleo kwa sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika ameweza kuunda kamati nzito kama zile za makinikia, zilizowezesha Serikali kuokoa mamilioni ya fedha na fedha hizi ambazo zilikwisha kupotea pia ameweza kuunda kamati kama hizo za bahari kuu, Mheshimiwa Spika huyu Job Ndugai kwa karama zake aliweza kusimamia imara kuhakikisha kwamba nidhamu inatawala Bungeni na kwa hilo amefanikisha sana hata pale ambapo maji yalitibuka basi Mheshimiwa Spika Job Ndugai aliweza kuliweka sawa jahazi na kweli Mheshimiwa Spika Ndugai ni nahodha mahiri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Spika kwa kutambua shughuli zake alihakikisha kwamba Bunge la Bajeti linafanyakazi yake pamoja na changamoto za *Covid 19* alisema hakuna kuvunja Bunge mpaka kieleweke alhamdulillahi tunaelekeea ukingoni mwa Bunge mambo yote mswano nani kama Spika Job Ndugai.

Naomba kuunganmkono maazimio yote hayo mawili na kuhakikisha kwamba Bunge hili la Kumi na Moja ni Bunge la kipekee napongeza sana uongozi mzima kuanzia Spika mwenyewe, Naibu Spika, Waziri Mkuu, Mawaziri wote na sisi Wabunge wote mwenyezi mungu atujaalie salama tushinde kwa kishindo na Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi irudi madarakani na akina Msigwa wapotee mbali. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zainab Matitu Vullu atafatiwa na Mheshimiwa John Heche, Mheshimiwa Jacqueline Msongozi Ngonyani ajiandae

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii siku ya leo, nianze kwa kumshukuru mwenyezi mungu aliyetujaalia na kuiona siku ya leo na kupata nafasi ya kuweza kuchangia hoja hizi mbili za makao makuu ya hapa Dodoma na kumpongeza Mheshimiwa Spika Job Ndugai. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba hakuna jambo lisilokuwa na mwanzo suala la makao makuu Dodoma chimbuko lake lilianzia mwaka 1970 wakati huo wa Awamu ya Kwanza wa Baba wa Taifa hayati Mwalimu Nyerere alilizungumza, 1973 likatekelezwa lakini kwa lengo la kufanya makao makuu ya Kiserikali tu. Baada ya hapo kwa uono mkubwa uliokuwepo likafikia kwamba hapa sasa pawe makao makuu ya nchi yetu ya Tanzania ni katikati ya mikoa yote kwa hiyo shughuli zote zikiletwa hapa kutakuwa na changamoto nyingi za kuinua uchumi, maana changamoto ni sehemu ya fursa kuendesha maisha vizuri, mawasiliano yatakuwa mazuri, hivyo basi nguvu hiyo ikaja ikapata msukumo kwa Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Tano Mheshimiwa Dkt John Pombe Joseph Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza sana kwa msukumo ambao ameuweka lakini msukumo huu haukuwa umeachwa ukapokelewa niseme kabla ya yote Mheshimiwa Spika Ndugai akaelekeza kamati zote za Bunge zianze kukutana Dodoma badala ya kuwa na kamati Dar es Salaam kamati ziwe zinakutana Dodoma na Bunge linaendelea hapa hiyo ilikuwa ni awamu ya mwanzo. Lakini kama haitoshi Waziri Mkuu kwa kuitikia kauli ya Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Tano Mheshimiwa Dkt. Magufuli alikuwa ndiyo kinara wa kwanza kuhamia hapa Dodoma akiambatana na Mawaziri wake na Manaibu Mawaziri wakuu wa taasisi mbalimbali wote walihamia hapa Dodoma miundombinu imeboreshwa kila mtu akingia Dodoma anaona mandhari ya mji ulivyo taa ziko kila mahali barabara za lami zipo kila mahali kwa hiyo, mji uko vizuri na wawekezaji wamekuja na wanaendelea kuja hili ni jambo jema na la faraja sana kwa mji wetu huu wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pia sambamba na hilo Mheshimiwa Rais kwa kuona kazi kubwa anayofanya Mheshimiwa Ndugai Spika wetu na juhudhi alizozifanya Mheshimiwa Ndugai ndani ya Bunge hili kwa kusimamia bajeti na maazimio mbalimbali bajeti hizo zimelenga ujenzi wa *SGR*, ujenzi wa umeme wa Mwalimu Nyerere, barabara katika mikoa na wilaya zetu, madaraja, shule, hospitali na zahanati kwa kweli ameona na yeye pia ameridhishwa na kazi anazozifanya Mheshimiwa Ndugai ameona soko kuu la Dodoma? Lipewe jina lake la Job Ndugai naomba mumpigie makofi jamani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sambamba na haya maazimio yote mawili yanakwenda pamoja pongezi kwa Mheshimiwa Rais, pongezi kwa Mheshimiwa Ndugai. Niongeze Mheshimiwa Ndugai yeye ni Spika wetu hapa na sisi ni miongoni wa wanachama wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Mwaka 2017 Mheshimiwa Ndugai alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola ya Afrika sijambo dogo jamani. Mheshimiwa Ndugai amekuwa kwenye kamati mbalimbali za Mabunge ya Afrika na Mabunge ya Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Ndugai yeye sasa hivi anaongoza kamati ya uwekezaji ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Watu wanasema mcheza ngoma hutunzwa na utamu wa ngoma sharti uingie ucheze. Mheshimiwa Ndugai kwa nafasi aliyokuwa nayo na ushawishi aliyokuwa nao ameona kuna kila sababu uwekezaji wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola ufanyike hapa hapa Dodoma ambako itajengwa hoteli ya nyota tano hoteli hiyo itakuwa chachu ya maendeleo kwa watanzania na wa Afrika kwa ujumla na hasa kwa kuwa itakuwa hapa Dodoma italeta ajira, italeta mambo mengi ambayo yatakuwa yanaelekezwa kwenye uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme pongezi hizi hatujakosea mji wa Dodoma unapendeza na watu wanakuja. Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa na yeye anaangalia makao makuu ya mji wetu yanavyokwenda mikutano yote tunaiona sasa hivi inafanyika hapa pamoja na tatizo la corona lakini bado watu wanaweza kufanya mikutano kwa mtandao hivi tungekuwa hatuna hizi *note pad* tungeweza kweli kufanya haya maendeleo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema kuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Ndugai na niseme uongozi wa Mheshimiwa Ndugai kwa kuwa azimio linamgusa, anaongoza kama bata na watoto wake. Watoto mbele bata nyuma maana yake ni kwamba uongozi wake ni shirikishi tunamuona Naibu Spika anang'ara na utaendelea kung'ara Mbeya wanakusubiri wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Najma na Mheshimiwa Chenge wote mnafanyakazi naye kwa pamoja na mnampa ushirikiano hilo ni jambo jema na ni jambo lenye faraja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na mimi nasema naunga mkono hoja ahsanteni sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa John Heche atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mheshimiwa Elias Kwandikwa ajiandae.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia maazimio mawili ambayo yapo mbele yetu. Nami sitazungumza Azimio la Dodoma nataka nizungumze kuhusu Azimio lilitetwa la kumpongeza Mheshimiwa Spika. Kwa kweli hiki ni kituko kingine kinatokea kwenye Bunge hili pamoja na vituko vingi ambavyo vimewahi kutokea huko nyuma. *Personal/hata mimi* sina ugomvi na Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukitofautiana na watu wa CCM na wengine na ninyi katika mazingira ya kikazi tu, lakini kama binadamu sina *problem* yoyote na Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo hayo yanayojitokeza Tanzania sasa hivi kwa watu kulilia sifa ambazo zimepita kiwango cha kibinadamu ni mambo yanayotia aibu na kinyaa. Haya mambo yamefanywa na huko nyuma na viongozi madikteta. Mobutu Sese Seko Kuku Ngbendu Wa Za Banga wa Zaire, alifanya mambo mengi ya hovyo. Alifika sehemu, Mobutu wakati wakati ule *TVzinaanza* inatengenezwa *jingo* ya kwenye *TV* anaonekana anashuka kutoka mawinguni wakati wa taarifa ya habari; watu wanaimba eti Mabotu anawasiliana na Mungu. Mawaziri, viongozi mbalimbali wa Serikali; viongozi *populist duniani* ndivyo walivyo, hawapendi kuhojiwa, wanapenda kusifiwa. Nami siamini kwamba Spika wetu anapenda kufanywa hivyo, kusifiwa.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Naibu, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mary Nagu.

TAARIFA

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Spika nawapongeza wote ambao wanaunga mkono maazimio haya. Nami napenda kumpa taarifa Mheshimiwa aliyekuwa anaongea kwamba watu wanavyofanya kazi nzuri, wanapofanya mambo ambayo yanaleta maendeleo, hakuna ubaya wa kuwaenzi. Kitu kitu kimoja ambacho anapaswa kufahamu siyo yeye mwenye anajienzi,

tunamuenzi sisi. Nawalioleta hoja hii sio Spika mwenyewe, wameleta wale na ninawapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge apokee hilo. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Mheshimiwa Heche, najaribu kufuatilia mchango wako. Azimio lilioko mbele yetu ni Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Spika. Maelezo yako ya hapa mwanzo yanatoa viashiria; na nimesema maelezo ya hapa mwanzo yanatoa viashiria kana kwamba unataka kutoa ulinganifu hivi kwamba Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Spika ni kama Mheshimiwa Spika hivi anafafana na viongozi fulani hivi amba walikuwa wanapendwa kupongezwa, kwa maelezo yako ya mwanzo.

Kama siyo hivyo ulivyokusudia, endelea na mchango wako, kwa sababu nilikuwa nakusikiliza kwa makini njue unaelekea wapi. Maana nataka kuamini hutaki kuonyesha kana kwamba Mheshimiwa Spika amezitaka sifa hizi wakati unafahamu aliyetao hili Azimio ni Mheshimiwa Kitwanga, yupo pale, naye sio Spika, ni Mbunge mwenzetu.

Sasa na mchango wako, labda nitapata tofauti na hicho ninachokiflikiria kwa sasa hivi.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba sana unilindie muda wangu. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba tuijepushe tusije tukawa kama wale. Unisikilize hoja yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mobutu wakati ule ilifika sehemu anamwagiza Waziri wa Fedha kwamba nahitaji dola milioni moja Waziri wa Fedha anamwambia Gavana Rais anahitaji dola milioni mbili. Gavana anamwambia yule anayetoea fedha kwamba Rais anahitaji dola milioni tatu. Zinatoka dola milioni tatu, hii *chain* yote inakung'uta, naye anapata dola milioni moja pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Franco wakati huo akaimba wimbo wa kukataa yale mambo yaliyokuwa yanafanyika pale, akakamatwa akawekwa ndani akafungwa. Akatengeneza sauti kama ya kumsifia Mobutu akiwa ndani, akatolewa akapewa Uwaziri wa Michezo. Sasa madhara yaliyotokea Zaire sitaki kuyazungumza, mpaka leo nchi tajiri kuliko zote Afrika hapa iko kwenye matatizo makubwa kwa sababu ya kuendekeza utaratibu huo.

SPIKA: Mheshimiwa Heche, nasikitika, sitakubaliana nawe kwenye hilo. Kwa nini? Kwa sababu hoja iliyopo mezani kwetu unaifahamu inasema nini.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, narudi kwenye hoja.

NAIBU SPIKA: Ukitaka kuonyesha kana kwamba kwa sababu hao wote uliowataja wao walikuwa wanataka sifa; kwenye hoja hii sio Spika aliyesimama humu ndani kuanza kujizungumzia hayo mambo. Yamezungumzwa na Mbunge, ndiyo maana akatoa hoja, ikaungwa mkono. Kama mtu haungi mkono, wewe unaenda kwenye ile hoja iliyio mbele yetu sasa.

Ukitaka kuonyesha kana kwamba unataka kumlinganisha huyu kiongozi ambaye leo Azimio lake lipo hapa na hao unaowataja, hapana huyu naye ni mwanadamu.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo nazungumza kuhusu aliyeleta hoja.

NAIBU SPIKA: Ngoja, ngoja. Huyu naye ni mwanadamu, huwezi ukamlinganisha na hao unaotaka kutaja na kusema walikuwa wanaendekeza vitu kama hivi. Mheshimiwa Spika hapa ndani kwanza hayupo na ninadhani alifanya makusudi ili asiwepo yeye hapa kwa sababu kama angekuwepo na anazungumza haya, ungesema anajitetea. Sasa Mheshimiwa Spika sio aliyeomba hili jambo, ametoa Mbunge mwenzetu. Kama unapinga hoja hiyo, pinga kwa

hoja zako, usimlingashe Mheshimiwa Spika na hao viongozi unaotaka kuwataja hapa, tafadhali. (*Makofi*)

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ndiyo maana nataka nimwambie ndugu yangu Mheshimiwa Kitwanga, asifanye Spika kama wale watu walivyokuwa wanamfanya Mobutu. Wale watu ilifika sehemu sasa baada ya Mobutu kutoka madarakani wakihojiwa wanasesma tulikuwa tunalazimishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naongopa kwamba huko mbele Kitwanga atakuja kusema kwamba alilazimishwa kuleta hili Azimio hapa. Kwa sababu hili Bunge ni Bunge ambalo limeonea watu sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche, tuelewane vizuri. Hii ni mara ya mwisho kutoa haya maelezo ninayotoa. Mheshimiwa Heche tuelewane vizuri sisi sote ni watu wazima, hakuna mtu ambaye wewe hujamwelewa na hata mimi sitaki kuamini haya maelezo yote wewe hujanielewa. Hakuna mtoto mdogo; mimi nawe ni watu wazima. Kwa hiyo, wewe unajua unachotaka kusema, nami nakijua, kwa sababu nami ni mtu mzima.

Kwa hiyo, tafadhali, tumtunzie heshima yake Mheshimiwa Spika, hajaombwa kupongezwa aliyetoa hoja hiyo ni Mheshimiwa kitwangwa na ameungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Haya ndiyo tumeombwa kuwa na uvumilivu, lakini acha niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili Bunge, Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Tundu Lissu alipigwa risasi akiwa hapa Bungeni akihuduria shughuli zake za Mbunge; na chini ya Bunge hili linaloongozwa Mheshimiwa Spika wetu, mimi namheshimu kama binadamu, kama rafiki yangu, kama Mbunge mwenzangu, likashindwa kumhudumia Mheshimiwa Tundu Lissu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wenzetu hapa akiwemo Mheshimiwa Lema, amefukuzwa mwaka mzima Bungeni kwa kutofautiana mawazo. Mheshimiwa Halima Mdee amefukuzwa miaka miwili hapa Bungeni, wananchi wa Kawe wakanyimwa uwakilishi kwa sababu ya ubabe. Hili Bunge limezuia hoja binafsi za Wabunge ikiwemo hoja ya John Mnyika, ikiwemo hoja ya Halima na wengi tu walioleta hoja binafsi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakuja hapa kupongezana kwa lipi? Kuna siku hata mwandishi wa habari ameandika maoni yake kuhusu Bunge hili akaitwa hapa akatishwa. Msione mmetisha watu wakanyamaza mkafikiri watu wanaunga mkono yale ambayo mnayasema hapa. Mkitaka kujua hili mnalolifanya hapa Watanzania hawalikubali, subiri maoni ya Watanzania. Tena kwa sababu mnatishia watu hata wakiandika kwenye mtandao, leo mngegeuka kuwa *laughing stock* ya dunia, kwamba mmekuja hapa Bunge; nami ningekuwa Spika ningezuia hiyo hoja ili labda iletwe Bunge ambalo nikiwa sipo kwenye kit. Kwa sababu naamini Mheshimiwa Job Ndugai Bunge lijalo hatakuwa Spika wa hili Bunge.

WABUNGE FULANI: Aaah!

HE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo nasema hivyo, kwa sababu hata CHADEMA tuna mgombea pale, atakuwa ameshamwondoa pale, Mbunge wa Kongwa atakuwa wa CHADEMA. Kwa hiyo, angesubiri Bunge lijalo ambalo Spika atakuwa mwingine, lije litambue kwamba labda Mheshimiwa Job Ndugai alifanya kazi kubwa. Bunge hili, kesho zinaingia sheria humu....(*Makofi/Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Kuna taarifa kutoka Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve.

TAARIFA

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nataka nimpe taarifa kaka yangu Heche kuwa

watu wote waliofukuzwa humu Bungeni sio Mheshimwa Spika alifanya kazi hiyo, ni vikao ambavyo vinapitishwa kihalali kuhakikisha wanapata *punishment according* na makosa ambayo wameyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche, unapokea taarifa hiyo?

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza kuhusu Spika kama Kiongozi wa mhimili wa Bunge, simzungumzi kama mtu binafsi. Ndio kiongozi wa Bunge, nasi tunajua *double standard* iliyotokea hapa, kuliwa na *issue* hata ya Mheshimiwa Masele hapa; ilivyokuwa *treated* ni tofauti na sisi ambayo tumekuwa-*treated* hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapozungumzia *treatment* ya Wabunge wa *opposition* na jinsi ambavyo demokrasia imekandamizwa upande wetu, jinsi ambavyo tumeburuzwa; mimi mwenyewe nibebwa hapa na Askari! Mbunge! Mimi Mbunge kama ninyi nyote, kama Spika, nilichaguliwa, tena wananchi wangu walinipatia kura nydingi kweli kweli. Nilibebwa hapa, nimedhalilishwa chini ya uongozi wa Spika Ndugai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nipozungumza kuhusu suala la kumpongeza Spika na kutokumpongeza, *actual/namtakia* mema zaidi isije ikaoneka kwamba labda nyuma ya pazia Mheshimiwa Kitwanga alisukumwa. Kwa sababu Mbunge mwenzetu amechagia hapa, yaani eti leo hii anachangia hapa, Azimio limetoka muda huu huu, yeye ana gazeti la *Daily News* la mwaka 2010; ameenda kwenye *Hansard* za Bunge, ameangalia sijui nani alichangia zaidi, sijui nani alifanya nini; ukiangalia mambo yote yale, sisi ni watu wazima tunaelewa kinachofanyika. Tunajua hapa mambo yanaavyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasi tungependa, kama Spika alikuwa Mbunge mahiri, Bunge la Tisa tungependa

mijadala iruhusiwe na Wabunge wengine wajijenge wawe mahiri kama alivyokuwa ye ye kipindi kilichopita.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche, ili tusilet mgogoro ambao haupo, wewe taarifa ya leo nini kitajadiliwa saa 8.00, umeipata saa ngapi? Wewe yaani. Umejua saa ngapi kwamba kutakuwa na haya maazimio? Umejua saa ngapi?

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, amepata gazeti, amekuwa na copy ya mwaka 2010 hapa.

NAIBU SPIKA: Ndiyo maana...

MHE. JOHN W. HECHE: Kweli!

NAIBU SPIKA: Ndiyo maana Mheshimiwa Spika anasifiwa, kwa sababu ukishakuja hapa, hiki kishkwambi unaweza ukawa umekaa hapo na ukapata hizo taarifa. Wewe ultaka achukue siku tatu kuchukua taarifa ambayo ipo kiganjani? Haiwezekani. Kwa hiyo, saa hiyo hiyo, hata wewe ukiamua kuangalia kwa mfano neno "*double standard*" maana yake nini? Hapo hapo ulipo utaipata. Sasa utaanenze kumtuhumu Mbunge kwamba alipata wapi taarifa? Hapana, twende vizuri tafadhali.

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilitegemea Waheshimiwa Wabunge wezangu hapa wangkuja na Azimio la kushughulikia matatizo ya Walimu wa Shule za Binafsi ambao wamesimamishwa tangu mwezi wa Tatu hawana mishahara; watoto wao wana-*starve*, wanahitaji kula kama sisi, wanahitaji kulipa kodi, wanahitaji kulipia maji, mimi ningelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ukiniambia nije nalo, sitakuja nalo kwa sababu kitu chochote kizuri cha Upinzani kikiletw hapa kinapigwa nyundo, ndicho tunachozungumza hapa. Kuna mtu kule jimboni kwake ana walimu wa shule za binafsi, wako nyumbani, hawana mshahara, eti ameleta Azimio la kumsifia Spika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukipima haya mambo, mtu anakwambia eti namsifia Spika kwa sababu ameweeka *lift* eti za kupandia kwenye ghorofa. Karne hii wazungu wameanza kupanda lifte sijui mwaka gani?

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

MHE. JOHN W. HECHE: ...leo eti mtu anakuja hoja ameandika eti ngazi sijui *lift*...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kemilembé Lwota.

T A A R I F A

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nilikuwa nataka kumpa taarifa msemaji anayezungumza, Mheshimiwa Heche kwamba anapotosha. Anaposema kwamba hakuna kitu chochote cha Upinzani ambaco kinakuja Bungeni kinashukughulikiwa. Vyote vinakuja vinapigwa nyundo, siyo kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Upendo Pendesa alikuwa hapa na Hoja zake za *pad* na zilisikilizwa na zilipewa nafasi na wote tulizingumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Heche kengele ya pili imeshagonga, lakini una fursa ya kujibu kwa sababu ulikuwa unapewa taarifa. Unaipokea ama huipokei taarifa hii?

MHE. JOHN W. HECHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakumkumbusha tu kwamba ilikataliwa ile hoja, ilikuja kwa njia nyingine. Haikuja kama ya Mheshimiwa Upendo.

NAIBU SPIKA: Haya, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, atafutiwa na Mheshimiwa Elias Kwandikwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama ajiandae.

(Hapa baadhi ya Wabunge walitoka Ukumbini)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lema muwe mnapenda kusikiliza na wengine wakiwa wanachangia. (*Kicheko*)

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu kwenye maazimio haya yote mawili; Azimio la Serikali Kuhamia Dodoma na pia Azimio la Kumpongeza Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa Serikali kuhamia Dodoma. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchukua maamuzi magumu ya kuweza kuhakikisha kwamba Serikali sasa inahamia Dodoma. Mchakato wa Serikali kuhamia Dodoma uliana mwaka 1970.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamepita Marais wengi na mchakato huu ukaendelea kufanyika kwa muda mrefu na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli mara baada ya kuingia tu mara baada tu kuingia madarakani miezi tisa baadaye alifanya maamuzi magumu ya kuhakikisha kwamba Serikali inahamia Dodoma. Huo ni uthubutu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uthubutu huo, ni kweli Waziri Mkuu pamoja na Serikali nzima wakaanza kumiminika kuja Dodoma na Watendaji wote wa sekta mbalimbali. Changamoto ilikuwa ni kubwa kwamba Ofisi nazo zilikuwa ni shida, lakini mpaka sasa hvi tunavyozungumza tayari umeshajengwa mji mzuri, Mji mahiri wa Kiserikali pale Mtumba. Kwa hiyo, shughuli za Kiserikali zinaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limewezeshwa kufanyika hivyo ambapo litakwenda kusaidia kurahisisha utoaji wa huduma. Pia litarahisisha kwa sababu hapa Dodoma ni katikati ya nchi, basi maeneo mbalimbali ya mikoa ya pembezoni wanaweza kupafikia Dodoma kwa haraka zaidi, wataokoa muda na hata gharama zile za usafiri zitapungua. Pia gharama za uendeshaji kwa ujumla, kwa sababu Serikali nzima iko hapa, gharama zimepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nawaunga mkono Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia kwa maana ya kuunga mkono hoja. Leo hii tarehe 8 tunakwenda kukubaliana kwamba asitokee mtu ye yote yule akafanya maamuzi tofauti ya kuahirisha Makao Makuu haya kuwa Dodoma. Pia isitokee Serikali na taasisi zote kutengua maamuzi haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii sasa kumwongelea Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai.

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, naomba nirudie hapo. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai kwa kazi nzuri ambayo ameifanya katika Bunge hili la Kumi na Moja. Kiukweli mnyonge mnyongeni, haki yake apewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemtambua Spika kwa umahiri wake, nimemtambua kwa uchapakazi wake, kwa mwongozo mzuri ambao amekuwa akitupa na kwa namna ambavyo amekuwa ameweza kutushirikisha mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, walipofanya maamuzi ya kutafuta michango ili waweze kuweka alama katika Bunge hili kwamba wamefanya ninikama *TWPG* aliunga mkono asilimia 100 na alijitokeza pia yeye mwenyewe kwenda kufatuta michango ya aina mbalimbali kwa maeneo

mbalimbali. Kwa hiyo niseme tu kwamba Spika katika hili ana mchango wake mkubwa lakini ameacha alama kubwa. Shule tayari imeshajengwa na shule hii itaenda kusaidia watoto wote wa nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipata hapa na bado tatizo hili lipo lakini siyo kwa ukubwa huo, janga la *corona*. Mheshimiwa Rais alitusaidia kutupa uimara yaani katuondoa hofu lakini akifuatiwa na Yustino Job Ndugai pamoja na Waziri Mkuu na Makamu wa Rais; walitutia moyo kwamba askari ni mbele kwa mbele hakuna kukimbia vita, lakini wenzetu wa Kambi Rasmi ya Upinzani waliyoyoma hapa wakakimbia wakiongozwa na Mwenyekiti wao. Kwa hiyo sasa tunapozungumzia, weledi, uchapakazi, uthubutu na ujasiri tunamzunguzia Job Yustino Ndugai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu wale wote unaona wanasi mama humu wakimlalamikia Spika wa Jamhuri kwamba hajatenda haki, na kwamba huyo Spika ameshusha hazi ya Bunge hebu waaangalie kwanza anayesi mama anazungumza angalia *feedback* yake, je, ni mtu ambaye yuko makini katika utendaji wake wa kazi? Ni mtu ambaye anazingatia kanuni na taratibu za kibunge, ni mtu ambaye ana nidhamu katika kusimamia majukumu yake ya Kibunge?. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo utaangalia, yaani akisimama tu anapozungumza utamuona kwamba huyu ni ndio walewale. Kwa hiyo kwa vyovypote vile kwa Spika ambaye yuko mahili, Spika ambaye anapenda kusimamia majukumu kwa kufuata kanuni na taratibu huwezi kumpenda hata kidogo. Kwa hiyo mimi nasema kwamba mimi naungana na wenzangu wote wanaomkubali Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwakumbushe tu ndugu zangu yako mambo mengi ameyafanya Mheshimiwa Spika ameyasimamia kwa ukaribu sana, lakini mimi nitataja machache tu kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Rais wetu anaingia madarakani tulipata changamoto kubwa sana ya ukosefu wa madawati katika shule zetu za msingi na Sekondari; na kwa kuwa ndio ilikuwa mwanzo wa elimu bure wanafunzi wengi sana walijitokeza kwenda kujiunga na masomo. Kwa hiyo tulipata shida ya upungufu wa madawati. Lakini Spika wetu aliweza kutushawishi na tukakubalianaye kwamba pesa ambayo ilikuwepo bilioni sita itumike kwa ajili ya kuchonga madawati. Namshukuru sana jambo hilo liliwezekana na kila maeneo ya madawati haya yalipelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pia suala la Bunge mtando wako watu wanakejeli hapa; mimi niseme tu mimi nimefurahi sana, lakini na Wabunge wengine wamefurahi sana. Kwanza tumeweza kujifunza na kujua namna ya kuperuzi kwenye mtando, lakini siku za nyuma mimi nakumbuka tunapovunja Bunge ilikuwa lazima ubebe watu watatu, wannne waje wakusaidie kubeba vitabu na huko nyumbani makabati yanajaa vitabu pasipo kujaa nguo. Kwa hiyo mimi naona kwamba jambo hili limekuwa kubwa, pia limesaidia sana kupunguza gharama za uendeshaji na hata sasa tumeweza kuokoa pesa nyingi zaidi ya bilioni 120.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Suala la Kulinda Hadhi ya Bunge. Kuna Mbunge; amesimama hapa akasema Bunge hili limekosa halijalindwa kwa hadhi yake. Mimi nataka niseme ndugu zangu hapa nimemsikia kaka yangu Mheshimiwa Msigwa ambaye ni Mchungaji amezunguza hili suala, lakini yeye ukimwangalia ni Waziri Kivuli wa Maliasili na Utalii, pia Mheshimiwa John Heche na yeye yako mambo hapa amebezabeza naye pia ni Waziri Kivuli wa Madini; yuko Mheshimiwa Godbless Lema naye amebezabeza hapa naye pia ni Waziri Kivuli wa Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu kabisa kwamba kivuli hata siku moja hakijawahi kupata mdhamana. Unapoambiwa kwamba wewe ni Waziri Kivuli moja kwa moja unakuwa *affected psychologically*; kwamba kivukli hakiwezi kupata mdhamana; saa mbili asubuhi kitakuwa hapa, saa tano asubuhi kitakuwa hapa, saa saba mchana kitakuwa

hana, saa 11 kitakuwa hapa. Kwa vyovyote vile hakina mdhamana kwamba nimeweka pale kivuli nitakuta jambo langu liko pale, inakuwa na hali ya kugeuka geuka, na ndivyo unavyowaona hawa Mawaziri Kivuli, wana hali ya kugeuka geuka. Nimeshuhudia *clip* moja inatembea miaka mitano iliyopita katika nafasi hii ya Ubunge Mheshimiwa John Heche alichangia ndani humu humu akilalamikia kwamba ni nchi gani hii, nchi haieleweke kwamba hata ndege acha tu ya kwenda Nairobi lakini imeshindikana hata ndege tu ya kutembea humu ndani ya nchi. Sasa ndege zilivyoanza kushushwa na Daktari John Pombe Joseph Magufuli amegeuka Heche anasema nani amewaambie mkanunue ndege tunawaaaambia msinunue ndege hamsikii huyo ndiyo Waziri Kivuli wa chama cha Upinzani.(*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini halikadhalika mmemsikia hapa kaka yangu Godbless Lema...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa kengele ya pili imegonga.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:...amewadhalilisha hapa Wabunge wa Viti Maalum napo sikushangaa kwa sababu yeye ni Mjumbe wa Kamati Kuu wametokea Wabunge wanawake...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda umekwisha.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: ...kutoka kwenye chama chake wakilalamikia; samahani, naomba dakika moja tu; wakilalamikia udhalilishwaji unaofanywa katika chama chao udhalilishaji wa kingono, lakini yeye kama Mjumbe wa Kamati Mkuu akiwepo Msigwa Mjumbe wa Kamati Kuu...

NAIBU SPIKA: Haya ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Elias Kwandikwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula ajiandae.

NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia maazimio haya muhimu.

Kwanza nianze niwapongeze pia watoa hoja Mheshimiwa Kitwangwa na Mheshimiwa Mabula. Vilebile uniruhusu nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwasababu yako mambo abayo yamefanyika Dodoma pamoja na kuhamia Dodoma ni kwa sababu ya msukumo na usimamizi mzuri wa Mheshimiwa Rais; na maendeleo makubwa sana yanaonekana hapa Dodoma. Kwa hiyo ninampongeza kipekee Mheshimiwa Rais kwa namna abavyo ametuelekeza na kuongoza kuona kwamba tunahamia Dodoma na sasa tuko Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Spika kwa sababu nikiangalia maazimio haya mawili mkono wa Spika upo. Kwa sababu utaona hata baada ya kuwa tumehamia Dodoma Mheshimiwa Spika amekuwa mahili sana katika kusimamia zoezi hili na mwisho wa safari tulikuja na Sheria kwa sababu Mheshimiwa Spika aliweka msukumo.

Kwa hiyo Mheshimiwa Spika kwenye maazimio haya yote mawili naona mkono wake uko wanguvu kabisa kwa kazi nzuri ambazo amekuwa akizifanya. Niseme tu kuwa anayo haki ya sisi kama Bunge kuweza kupokea azimio; na mimi nianze kusema kwamba naliunga mkono kwa asilimia 100. Nani asiyefahamu kwamba Spika wetu amekuwa akisimamia vizuri kanuni kwenye Bunge hili, na isingekuwa umahili wa Spika na nyinyi mnaomsaidia pamoja Wenyevitii saingine hapa ingekuwa songombingo kweli. (*Makofii*)

Kwa hiyo anayo haki ya kupokea pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Wabunge kama tulivyowasikia kwa sababu amekuwa akisimamia kanuni vizuri. Hata tulishuhudia hapa Spika alikuja hapa na kuwatambua Maspika waliotangulia, siyo jambo dogo. Tuliunga mkono hapa na tuliona majoho yakikabitihwa hapa, lakini nani asiyefahamu Spika wetu kwa ushawishi. Niseme tu kwamba Spika pia ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi. Kwa upande mmoja anasimamia Serikali ya hapa Bungeni, lakini kwa upande mwininge kwenye chama anasimamia utekelezaji wa ilani ya chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo anayo haki na stahili ya kupewa haya yote ambayo kwa azimio ambalo tumelipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Spika kwa kazi nzuri anayofanya na mimi nilivyosema naunga mkono maazimio haya. Lakini niseme tu pia kipee kabisa tumeona kwa umahili wake Mheshimiwa Spika ameweuka msukumo mkubwa kuona tunafanya maboresho ya miundombinu ili kuweza kuunganisha Wilaya za Mkoa huu; akitambua kwamba iko haja ya kuona kwamba Mkoa huu unapata huduma vizuri sana. Lakini yako mambo mengi ambayo nilitaka niyaseme, lakini wale Waheshimiwa Wabunge hapa nimeona Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Heche, Msigwa kuna mambo waliyazungumza hapa na mimi kimsingi nilikuwa naona kama wanabeza maendeleo makubwa ambayo yamefanyika kwenye Makao Makuu hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niyatolee kidogo maelezo ili tutambue Bunge kwamba kazi kubwa inafanya. Kama nilivyosema kwamba kwa msukumu wa Mheshimiwa Rais iko miradi kabambe hapa tumeshuhudia ikiendelea kufanyika kuhakikisha kwamba Jiji la Didoma linaboreshwaa.

Kwanza tumeona tumekuja kuwa na Jiji la Dodoma, lakini miundombinu yake kwa hali ya juu kabisa nilitaka niitaje ili tuone kwamba pamoja na yote lakini mkono wa Spika upo kwenye kuhakikisha kwamba maendeleo makubwa sana yanafanyika hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme iko mipango mizuri ambayo inaendelea na tumeendelea kufanya kazi kwa umahili mkubwa kwa sababu ya kuboresha Dodoma. Nikianza kuzungumza juu ya barabara, kwamba tutakuja na *ring road* barabara ambazo zitajengwa kilometra 112.3. Kwa hiyo mipango inaendeela vizuri na niseme tu kwamba tuko kwenye hatua ya mwisho kabisa ya kuwapata Makandarasi wa kujenga barabara hapa. Kilometra 112 siyo mchezo itafanya Mji huu uweze kuwa na huduma nzuri. Kwa hiyo tunakwenda kufanya ujenzi, unaona. Mikataba itasainiwa kwa sababu ya (*COVID*) tulichelewa kidogo, lakini naamini muda si mrefu tutasaini mikataba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na niseme tu, *commitment* ya ujenzi wa barabara hizi za *ring road* ni takribani dola milioni 214.69; sasa hizi ni fedha nyingi sana. Ukijaribu kuzibadilisha ni kama barabara hizi zitagharimu billioni 490 hadi billioni 500 kujenga barabara hizi. Sasa hebu uone kwamba *design* zilizokuwepo ukubwa wa barabara; Mheshimiwa Lema alizungumza hapa; lakini tutakuwa na barabara ambazo pia zitapunguza msongamamo hapa katikati ya Jiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mipango hii inaendelea vizuri wakati wowote tutakwenda kwenye hatua ya kusaini mikataba twende kujenga barabara hizi kilometra 112, barabara ambazo zitakuwa ni pana kabisa, zitakuwa na njia mbili; uone kwamba kama Serikali imejipanga vizuri. Ndiyo maana naendelea kumshukuru Rais kwa msukumo wake na tumeshuhudia jinsi anavyolisukuma hili jambo ili tuone kwamba tunakuja kufanya maboresho ya barabara ya kutosha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwa upande wa ujenzi wa viwanja vya ndege, natoa mifano michache ili tuone namna ambavyo tumejipanga. Nako utaratibu unaenda vizuri tenda zimeshaitishwa tunakwenda kufanya ujezi wa Uwanja wa Ndege wa Msalato. Na *commitment* ya uwanja huu ni fedha takribani dola milioni 236.17, utaona takriban billioni 540 tunaenda kujenga uwanja ambaa utakuwa na *runway* za kutosha, huduma za kutosha nyingi

na tutakuwa na uwanja wa kisasa. Nilimshangaa Mheshimiwa Lema labda angekuwa ameweza kupata hapa michoro tu kwenye mtandao aone namna nzuri tutaenda kufanya maboresho ya Uwanja huu wa Ndege wa Msalato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tumejipanga vizuri na Jiji la Dodoma litaendelea kupata huduma nzuri kabisa itakayoendana na hadhi ya Jiji lenyewe la Dodoma na Makao Makuu. Kwa hiyo tunakuja na ujenzi wa uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo haitoshi, niseme yako maboresho mbalimbali yanaendelea kufanyika. Hata huu uwanja huu wa ndege wa Dodoma tumeona kwamba tunaendelea tunauongeza urefu wa kurukia ndege na tutaweka na *facility* za taa za kurukia ndege, tutatoa huduma mpaka usiku. Haya ni Makao Makuu, kwa hiyo ni lazima ndege nytingine zishuke hapa Mjini usiku. Bombardier itashuka hapa, nafikiri Waheshimiwa Wabunge mmeshuhudia ujenzi unaendelea hapo. Wakati wowote tutaweza kukamilisha uwanja ule, tutaweza kwenda kutoa huduma vizuri kabisa katika uwanja huu wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilitaka nitolee mifamo mingine ya barabara za Mjini. Tumeshuhudia, hata mimi napita kwenye mitaa ya Mji barabara nydingi sana zimeendelea kuboreshwa hapa Mjini. Najua changamoto bado zipo, lakini kupitia *TARURA* na wenzetu wa *TAMISEMI* kuna ujenzi mbalimbali unaendelea kwenye mitaa. Niseme kuanzia mwaka 2010 mpaka leo hapa barabara zilizoboreshwa katika mji huu takribani kilometra 150 zimejengwa hapa na tunaendelea kufanya ujenzi na Mheshimiwa Rais ameelekeza au fedha nydingi zitaendeela kuja katika mji huu kuboresha ili tuhakikishe kwamba Mji huu wa Dodoma unafanana na Makao Makuu. Kwa hiyo harakati zinaendelea. Hivi ninavyozungumza pia kuna kilometra 51 kwenye Mji wa Serikali ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa mambo haya yote haya mtu anasimama hapa kubeza mimi nashangaa, lakini

kwa sababu ya kuwa na *character* ya kubeza kila kitu, Mheshimiwa Mwakajoka unaniangalia unafamu sisi tunasema ukweli kwamba kazi nzuri na kwa macho tunaishuhudia kwamba kazi inaendelea kufanyika vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo yako mambo yanaendea mazuri. Watu wamebeza hapa kwamba mji haufanani, si kweli kuna mambo makubwa yanafanya hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninasema kwamba pamoja na yote haya mkono wa Spika wetu hauwezi kukosekana hapa kwasababu yeye kama kama Mjumbe wa Kamati Kuu wa chama cha Mapinduzi, lakini nafahamu pia ni Mbunge kwenye Mkoa huu wa Dodoma. Yako mengi ambayo anaendelea kushawishi na kusukuma ili kuona maendeleo katika Mkoa wa Dodoma na huduma mbalimbali zinaendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kupongeza maazimio haya mazuri maazimio mawili yaliyoletwa na Waheshimiwa Wabunge hapa na mimi naunga mkono na niseme tu kwamba mambo mazuri yanaendelea na sisi kama Serikali tunaendelea kujipanga kuhakikisha kwamba Mji huu wa Dodoma unapata huduma na miundombinu mbalimbali mizuri kulingana na hadhi ya Mji wa Makau Makau.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, nashukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Mabula, Mheshimiwa Kitwanga ajiandae.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niunge mkono maazimio yote mawili na kwa dhati ya moyo wangu nimpongeze sana ndugu yangu Kitwanga , nimpongeze sana ndugu yangu Mabula kwa kutuletea maazimiuo mazuri sana ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze kwa kuwakumbusha Wabunge wenzangu kuzingatia kanuni na utaratibu wa mijadala Bungeni. Azimio linalomuhusu Spika linasema ni azimio la Bunge la kumpongeza Spika kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mafanikio ya Bunge la 11. Nilifikiri kwanza tulitakiwa tutambue kwamba hili azimio litapozungumza mafanikio ya Bunge la 11 ni pamoja na sisi Wabunge wenyewe wote na Spika ye ye akiwa kiongozi wetu tu, lakini mafanikio haya yote ni pamoja na sisi wenyewe. Kwa hiyo anaposimama Mbunge kubeza ni kwamba kwanza anajibea ye ye mwenyewe yaani tunajibea sisi wenyewe Wabunge, tunajibea sisi wenyewe Wabunge, kwasababu alipokuwa anaongoza Spika alikuwa anatuongoza sisi tufanye na tufanye kwa kiwango cha ubora wa hali ya juu. Mimi nilifikiri tulitakiwa Wabunge leo tuunge mkono Azimio hili kwa sababu ya uongozi mzuri wa Spika na Bunge hili ndiyo limeweza kuwa na mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninasema hivyo kwasababu gani leo hii hata Watanzania watatushangaa kwasababu ndani ya uongozi wa Spika huyu ambaye tunasema tunakuwa na Azimio la kupongeza ndiyo mambo yale ambayo watanzania walikuwa wanayategemea kwa Serikali hii yameweza kuitishwa vizuri na Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba Watanzania wawashangae wanaobeza Azimio hili na ukitizama wanabeza kwa misingi ya ubinasi lakini siyo kwa misingi ya faida ya Watanzania wote na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mdogo; hivi Spika alipoongoza Bunge hili la Kumi na Moja kwa dhati na leo taifa letu limeweza kuweka kumbukumbu ya mageuzi

makubwa ya tiba za kimkakati; tumekuwa na hospitali, zinatibu magonjwa ya figo, zinatibu magonjwa sugu ya moyo, zinapandikiza vidude vya kusikilizia kwa watoto, tiba zile kubwa ambazo zilikuwa hazifanyiki ndani ya taifa hili zimeanza kufanyika ndani ya taifa hili kwa sababu ya kazi nzuri ya Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli, lakini kwa sababu fedha zimepitishwa na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Spika Job Ndugai. Hivi Mtanzania akisikia leo tunabeza sifa hizo ambazo zinarudi mpaka kwetu sisi Wabunge za kuwasaidia watanzania kila mtu atatushangaa.(Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili pamoja na Wabunge chini ya uongozi wa Spika ndilo liliolunda Kamati maalumu kabisa za Bunge; zimekwenda kufanya utafiti wa namna gani taifa hili kwa uongozi wa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli tutanufaika na rasilmalli za taifa. Bunge hili lilichukua wiki nzima kufanya mjadala wa mageuzi makubwa kwenye Sekta ya Madini, Sekta ya Mafuta, na Sekta ya Uvusi. Matokeo ya kazi hiyo nzuri iliyofanywa na sisi Wabunge tukiongozwa na Spika wetu na ninyi mkisaidia na kila kitu ambaye alifanya kazi hapa leo tumezuia utoroshaji wa makinikia kwenye taifa letu kwa faida ya Watanzania. Mtu anabeza anasema kwamba haya siyo mafanikio. Leo tumeweza kuipa Serikali nafasi ya kuongeza mapato makubwa ya madini; Mheshimiwa Waziri wa Madini anajua, imepafanywa na Bunge hili, mtu anabeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale Wenye viti waliokuwa kwenye hizo Kamati leo Mheshimiwa Dotto ndio Naibu wa Wizara hiyo ya Madini, Mheshimiwa Zungu alikuwa kwenye Kamati ya Bahari Kuu leo ndio Waziri wa Mazingira na mambo ya Bahari yapo humo ndani na mafanikio ni makubwa sana. Nawaomba Watanzania waelewe hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwambia Watanzania wanatushangaa. Tusiendeshwe na ubinafsi, tuendeshwe na *fact* na uhalsia wa Azimio lenyewe ambalo linaonyesha ni matunda gani Serikali ikiongozwa na Mheshimiwa Rais, lakini

Bunge likiongozwa na Mheshimiwa Spika na mafanikio makubwa tuliyoyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweza kufanya mabadiliko kwenye sekta ya Miundombinu. Ni Bunge hili lilioongozwa na Mheshimiwa Spika na sisi Wabunge tukiwa chini ya Mheshimiwa Spika. Leo kweli Mtanzania atatushangaa tunabeza miundombinu ya reli ambayo inaenda kulipambanua Taifa hili kuwa ni Taifa lingine tunabeza kwamba Bunge hili halijafanya kazi. Tunabeza kwamba Kiongozi wa Bunge hili hakufanya kazi, ni vitu vyatuhangaza Mheshimiwa Spika. Tuelezeee mafanikio, elimu bure, tunabeza ni sisi Bunge tulipitisha hizo fedha za elimu bure, tunapitisha hapa ndani, ni sisi Wabunge tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati; kwa Uongozi huo tumefanikiwa kupeleka nishati mpaka vijiji huko, leo uchumi wa nchi hii unaenda mbele kabisa, ni Bunge hili. Nimpongeze sana Mheshimiwa Kitwanga, sijali ametumia lugha gani lakini Mheshimiwa Spika na nyinyi wasaidizi wake na sisi Wabunge, Azimio linasema Bunge la Kumi na Moja kwa mafanikio tujipigie makofi tumefanya kazi kubwa sana. Kazi tulioifanya imeacha alama ya utendaji mzuri wa Serikali ya Awamu ya Tano na maendeleo endelevu yanayoonekana kwa wananchi wa Tanzania. Mwenye macho haambiwi tazama, asiyetaka kukubali shauri yake, lakini sisi tumefanya, Serikali yetu imefanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhamia Dodoma kila jambo jema linakwenda kwa hatua. Tumesema hapa mchakato huu ulikuwa ni toka wakati wa mwaka 1973, Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi ilishafanya maamuzi. Mheshimiwa Msigwa hapa anasema ooh Katiba sijui mmeyunja, *GN* zilishatoka toka mwaka 1973, 1984, mwaka 1994, yalishafanyika hayo maamuzi. Ni utashi dhahiri, ujasiri wa kusimamia maamuzi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ndio maana leo Serikali ipo hapa Dodoma. Kwa hiyo hakuna hapa kitu ambacho tutakiona ni kitu cha ajabu. Sisi tumewaambia tumeshahamia hapa Dodoma na labda

niwaambie Wabunge hawajui kwamba baada ya kuhamia hapa Dodoma tayari wafanyakazi wa Serikali 15,361 wote wapo hapa Dodoma na kazi zinahafanya hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *master plan*, wanafikiri sisi tunakwenda tu, sisi tunakwenda kwa mipango. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameshazindua *master plan* ya Dodoma hii kwa mwelekeo ule tunaoutaka na kama hawajui huko wanakosifia Abuja sijui wapi wapi walichukua hizo *master plan* hapa kwetu. Itakuwaje sisi tupeleke *master plan* kwa watu halafu sisi tuwe na *master plan* mbovu, haiwezekani. Tumeshajipanga na kama Wabunge wangekuwa wanakumbuka wangechukua vitabu nya Bajeti hivi, kwenye vitabu hivi nya bajeti, bajeti zote zimeshaonesha ni namna gani tunaweza kuujenga vizuri Mji wetu wa Serikali na utakuwa ni Mji bora na Makao Makuu ya Serikali hapa yatakuwa bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi, Ibara ya 151; kama ametekeleza Afya, kama ametekeleza Barabara, kama ametekeleza Elimu na hili la kuhamia Dodoma Dkt. Magufuli amelitekeleza na tumefanikiwa na tuko hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida za kuhamia hapa Dodoma kila mtu anazijua. Kwa kuhamia hapa Dodoma, Morogoro imeanza kukua kwa kasi, Singida inakua kwa kasi, Babati inakua kwa kasi na mikoa mingine inakua kwa kasi na mwisho wa siku ni kukua kwa huduma za uchumi, ongezeko la mapato, lakini ni tija kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo dakika ni chache, lakini naomba niseme, nampongeza Mheshimiwa Mabula, nampongeza Mheshimiwa Kitwanga, Maazimio hayo ilikuwa ni lazima yaletwe kabla Bunge hili la Kumi na Moja halijamaliza muda wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Maazimio haya na kwa kweli Mungu Aibariki nchi yetu, ambariki Rais wetu, lakini alibariki Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwemo Mheshimiwa Spika wetu Job Ndugai. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula uhitimishe hoja yako, tutamalizia na Mheshimiwa Kitwanga.

MHE. STASLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuhitimisha hoja ya Azimio nililoleta mbele yako toka mwanzo. Nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri kwa namna ya pekee ambavyo wameweza kutoa michango yao. Jambo kubwa la kufurahisha wote waliochangia juu ya Azimio hilli wamelikubali na wamekubali na kukiri kulismamia na kwamba lilikuwa wazo zuri la Serikali kuhamia Dodoma na hawaoni sababu ya mtu mwingine yoyote awaye atakapokuja kuhamisha Makao Makuu na nchi Dodoma na kuyapeleka pahali popote nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vitabu vitakatifu kitabu cha Warumi 13:7 kinasema maneno yafuatayo, naomba ninukuu: "Wapeni wote haki zao, mtu wa kodi, kodi, mtu wa ushuru, ushuru, mtu wa hofu, hofu, mtu anayestahili heshima, apewe heshima, kwa maana ni haki ya anayefanya vizuri kupewa heshima yake kwa kutambuliwa au kwa kupongezwa". (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sikushangaa sana nilivyokuwa naona kundi la kina Mheshimiwa Mwakajoka wametawaliwa na hofu yaani hofu imewatala kwenye michango yao. Hofu hii ndio sababu kuu inayowafanya hata wawe na roho mbaya ya kusema ahsante japo kwa kiasi ambacho umekifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba uanzishwaji wa Makao Makuu Dodoma kama Waheshimiwa

Wabunge walivyosema na Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Waziri alivyomalizia hapa, kwamba mchakato huu ulianza zamani lakini ni lazima turudishe sifa na shukrani na pongezi nyingi kwa jasiri mwongozo njia Dkt. John Pombe Magufuli. Miaka 47 baadaye, leo anakuja kutekeleza mambo ambayo yalizaniwa kule nyuma hayawezekani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna shaka baada ya miaka 47, Dodoma tunayoiona leo ndani ya miaka minne ni mafanikio na matarajio yetu kwamba miaka michache inayokuja kama kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi alivyosema tunatarajia kuona mabadiliko makubwa ambayo mabadiliko haya yataendana sambamba na ukweli ndio huo na ukuaji wa kiuchumi wa Mji wa Dodoma, lakini na mikoa ya jirani inayoizunguka Dodoma. Halikadhalika hata mikoa mingine leo wakati tunazungumza hapa Mheshimiwa Kwandilkwa amesema hapa kila mkoa unakotoka leo Makao Makuu ya Mkoa kuja Dodoma kumeunganishwa kwa barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mafanikio makubwa sana katika Serikali ya Awamu ya Tano ambayo kimsingi yalikuwa na mchakato wa muda mrefu. Sasa leo tukisema tunampongeza Dkt. John Pombe Magufuli mtu ananuna na mimi sishangai kwa sababu kazi ya Urais sio kazi nyepesi kama watu wanavyoififikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namuangalia hata ndugu yangu Mheshimiwa Msigwa hapo wakati anachangia nikawa najiuliza moyoni, hivi Mheshimiwa Msigwa naye anaamini ni *presidential material* mpaka anakwenda anatangaza nia ya kuchukua Urais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikasema hili jambo linahitaji mtu makini na mtu makini na jasiri, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema hawezi toka Chama kingine tofauti na Chama cha Mapinduzi. Sasa nadhani wanagetumia sana muda huu vizuri kujenga Chama maana tunaona kabisa Chama kinakwenda kuporomoka na hatutarajii kuwa na mpinzani mshindani wa nguvu wa kiasi hicho tunachokififikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeridhika sana na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge na sikusudii kutumia muda mrefu sana. Nikuhakikishie jambo hili ni jambo kubwa na ni jambo la msingi na Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na mimi, tunapokwenda tutakuwa tumekwenda kutenda mema ambayo Watanzania wa miaka ile 47 iliyopita walikuwa na maono makubwa ya kutumia fedha, rasilimali zao na hata uwezo wao wa kufikiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho sikusudii kusema kidumu Chama cha Mapinduzi, lakini naomba kutoa hoja sasa kwamba Bunge lako likubali hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: toa hoja!

NAIBU SPIKA: Ameshatoa hoja Inabidi waunge mkono. Ameshatoa hoja.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshasema.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, anayesikiliza Wabunge wote hapa ndani ni mimi. Mimi nasema amesema sasa wewe unabishana tukaite *hansard*? Amesema kwamba anatoa hoja jambo hilo likubaliwe, sasa Wabunge ni kazi yao kusimama ili waunge hoja mkono.

Mheshimiwa Mwakajoka una siku chache humu ndani tafadhali. Sijui ni Mheshimiwa Mwakajoka sijui ni Mheshimiwa Haonga mnaongea sana. Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. (*Makofi*)

Kwa utaratibu wetu ingebidi niwahoji sasa, lakini kura zimeshapigwa hapa na idadi kubwa ya kura hizi zilizopigwa wamekubali Azimio hili. Kwa hiyo Azimio hili limepitisha. Bunge limepitisha Azimio la Bunge la kuitaka Serikali kutobadili

Uamuzi wa Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi na Shughuli za Serikali.

Sasa Waheshimiwa Wabunge nimuite Mheshimiwa Charles Kitwanga, ahitimishe hoja yake.

MHE. CHARLES M. KITWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu leo nitambue kwamba kuna maneno mawili huwa yanasemwa, nilikuwa sijui leo nimeshuhudia. Kuna watu wenyе akili ndogo na watu wenyе akili kubwa. Leo nimeelewa na nimeshuhudia na baada ya kuelewa hivyo sasa naomba nijikite kuwaelimisha kwa kutumia mfano rahisi sana, watu wale wenyе akili ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mwimbaji mmoja hapa Tanzania nampenda sana anaitwa Harmonize, aliiimba wimbo sasa watu wenyе akili kubwa ndio wanaweza kuelewa alikuwa na maana gani. Aliimba wimbo unaitwa "matatizo"; katika kuimba alisema mama ni mgonjwa sana, wakati anazungumzia mama akasema angalau yale matatizo yaahirishwe. Angalau tu apate muda wa kuahirisha kila siku matatizo, lakin alikuwa na maana hii, mama kwa sisi Watanzania ni nchi yetu Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baba Mungu aliiumba Tanzania na baada ya kutokea Tanzania tuna Kiongozi wetu anaitwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ndio Rais anayeiongoza nchi yetu. Katika kuiongoza nchi yetu ana maono ya mbali, ya kuongoza na kuipeleka nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ya Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Spika, kupitia Mhimili huu, inaonesha kwamba Mheshimiwa Spika, hakumsoma na kumwelewa Rais wetu ame-*play his part* kwa kuongoza huu Mhimili ili usaidie hayo maono ya Rais wetu kuyafikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtu hazungumzii, hatumzungumzii Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yale madogo. Mheshimiwa Spika alichofanya ni kujenga *System*,

na nilizozitaja hapa ni *systems* amejenga *systems* aondoke Mheshimiwa Spika kesho huyu Ndugai kesho kutakuwa na *e-parliament*.

Mheshimiwa Naibu Spika, awe ameondoka Spika, uwe umeondoka Naibu Spika lakini *e-parliament* itaendelea *kue-exist*, ndiyo sababu unamwona mtu mwenye maono kama hiyo anastahili kupongezwa. Mtu mwenye maono kidogo ya chini anazungumzia public *this is a tool to implement e-parliament*, lakini yeye nazungumzia tool badala ya kuona *the system*. Yote yalioko kwenye mambo matano niliyoyasema hapa ni *systems* alizozijenga Mheshimiwa Spika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nyie Wasaidiazi wake mmemsaidia sikumzungumzia Naibu Spika, sikumzungumzia Kagaigai, sikumzungumzia *Secretary*, angalia tulivyo *response so fast*, tulipoona kuna matatizo ya *system* yetu akaja na sehemu ya kuangalia, sasa hatubonyezi ni kwa sababu ya *system* iliyopo iko *flexible it can be changed any time*, mtu mwenye maono ya namna hiyo anaweza kuwa hajafanya yeye, lakini mtu aliye-*rigid* ukimwambia tufanye hivi, Spika alikuwa na uwezo wa kusema tutapoteza pesa tu, lakini kwa sababu na yeye ana maono ya mbali na anatambua kuna Rais mwenye maono ya mbali amekubaliana, amekubaliana tukawa na hiyo *system*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Harmonize anapoimba huo wimbo tuwe tunaangalia nchi yetu Tanzania ndiyo mama yetu na tujifunze nini kutoka hapa. Sisi nazungumzia Bunge, lakini sasa hilo Azimio lina mambo mengi nizungumzie tu upande wetu wa Bunge tukitoka au utakapokuwa unataka kwenda kugombea *put systems where are you come from* ukitoka ujulikane kwamba niliweka *system* hii na hii, mimi siyo Mbunge leo lakini naendelea *ku-exist* ndiyo Spika wetu mwenye maono ya mbali na anastahili kupongezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni Waziri, wewe sijui ni nani upande wa Serikali *put a system*, ningekuwepo rafiki yangu yule mtani wangu wa kule Isimani ningemtania, pale

yuko kwenye ardhi *put a system*, ardhi watu wasigombane wewe ukaenda kusimamia, *system* ifanye kazi. Spika ameweka *system* hapo watu wanatolewa nje *automatically*, si Spika anayekutoa nje, ni kwa sababu Spika ameweka *system* kwamba wewe ukifanya hilli na hilli na lile you *go out*, *they are going out* kwa sababu yana akili hiyo ambayo nimeisema na kwa sababu hayafuati utaratibu, Spika hafukuzi mtu hapa *is the system who takes you out* na mtakaporudi na watakaorudi mkiendelea kuvunja hivyo *system* ambayo ameiweka Spika *you will go out*. Mpaka nacheka nashangaa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuzungumza hiyo ili tuone na mimi nampenda huyo kijana hakuna wimbo anaoimba sina uhakika kama ni ya kwanza ama ya pili, ehee basi jamani naomba tu niseme hivi yote haya tunayoyafanya ni kwa ajili ya kujenga nchi yetu Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mama yetu, mama yetu huyu ndiyo mama, baba yetu ni Mungu, Kiongozi wetu ni Mheshimiwa Rais ambaye kama ningepata muda nikianza kuongea hapa kumsifia ninavyojuwa uwezo wake inaweza kunichukua masaa mawili sasa kwa sababu hiyo na muda na kengele zimelia namfahamu Waziri Mkuu alivyo mzuri anapofanya kazi zake wote ningetaka kusifia kuanza kuzungumzia ingechukua muda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niseme hivi, naomba kutoa hoja yangu muiunge mkono. (*Makofii*)

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono ahsanteni sana. Kwa utaratibu wetu ningekuwa natakiwa kuwahoji, lakini sasa kura zimekwishapigwa na Wabunge walio wengi wamekubali hoja hii ya kumpongeza Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo Azimio la Bunge la kumpongeza Spika la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mafanikio ya Bunge la Kumi na Moja limepita Rasmi. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nami niungane pamoja nanyi katika haya Maazimio yote mawili, niwapongeze Wabunge wenzetu ambaao walichukua hatua ya kuona kwamba haya mawili yote yanastahili; kwanza ni hilo la Makao Makuu ya Dodoma ni jambo jema na naamini litakuwa Azimio hili likiungwa mkono kila mahali kwa sababu kitendo cha kuweka Makao Makuu hapa na utekelezaji kuanza umewasaidia wananchi kupata huduma kwa karibu. Pia namna ya Mji wa Serikali ulivyojengwa umewaweka hawa watu sehemu ambazo zinafikika wote wapo hapo hapo karibu karibu, kwa hiyo mwananchi akienda kuhudumia na Wizara hii anaweza kwenda na Wizara nyingine, maeneo hayo hayo, kwa hiyo tunawapongeza sana Serikali kwa utekelezaji wa jambo hili.

Pia upande wa Mheshimiwa Spika nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wote na naamini wananchi ambaao sisi kama chombo ambacho tunawakilisha wataungana nasi sote kwamba Mheshimiwa Spika chini ya Bunge hili ambalo ameliongoza yamefanyika mambo mengi makubwa sana. Hizi sauti za watu kutokutaka kukubali uhalisia, sidhani kama ni jambo la ajabu ambalo linatakiwa pengine kurudisha nyuma, hatua za wale ambaao wangependa kuwapongeza watu wanaofanya vizuri. Kuna watu hata ukimtaja Mheshimiwa Rais na mambo makubwa aliyofanya wanatamani ungemtaja yeye, sasa haiwezekani anatajwa na kupongezwa yule ambaye amefanya vizuri. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, wengine pengine hawafahamu wanafikiri Spika ni kuja kukaa hapa mbele kuongoza kikao kama hivi hapana, Spika ni Kiongozi wa huu Mhimili na Spika ni Mwenyekiti wa Tume wa Utumishi wa Bunge mambo yote yanayohusu Wabunge Mwenyekiti wake ni Spika. Sasa kama kuna jambo lolote linalofanyika hapa Bungeni halafu ukataka lisihusiane na Spika utakuwa humtendei haki kwa sababu wewe kama Mbunge kuna jambo gani ambalo hujafanyiwa vizuri na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mazingira Mbunge uliadhibiwa siyo Spika aliyekuadhibu, ni Azimio la

Bunge. Kwa hiyo tusifike mahali tukaanza kuonyesha kana kwamba pongezi zinatakiwa zije zitoke baadaye zije zitoke namna gani hapana na hapa nilitisha kamusi kabisa. Pongezi siyo lazima mtu awe ameondoka ndiyo uanze kusema alikuwa, alikuwa, hapana, akiwepo mtie moyo mtie hamasa, ndiyo kamusi inavyosema, ukimtia moyo atafanya zaidi ya hicho ambacho amekifanya.

Kwa hiyo niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge ambaao wamechukuwa hatua ya kutukumbusha mambo mazuri ambayo amefanya na pia Azimio lile la kumpongeza Mheshimiwa Spika ni wazi halikuweza kutaja mambo yote. Nimefurahi kuwasikia Wabunge wengine wameongezea hayo ambayo hayakutajwa kwenye hili Azimio kwa sababu yamechaguliwa matano, lakini mambo yaliyofanywa ni mengi na nadhani mtu anayestahili heshima kama ambavyo tumesomewa kwenye kitabu cha dini, apewe heshima yake na kama yupo ambaye hamuheshimu basi ni kwa kuwa pengine Nabii hakubaliki kwao.

Kwa hiyo basi wale ambaao wameamua kumkubali huyo Nabii basi na sisi tuungane nao nami nakubaliana kabisa na sisi sote ambaao tumeona kwamba Mheshimiwa Spika amefanya jambo kubwa. Nami nimefurahi katika kura nilivyokuwa napitia hapa Maazimio haya mawili wala msitiie na wasiwasi kura nydingi kabisa za ndiyo pia zimetoka upande wa pili kwa Maazimio yote mawili. Kwa hiyo, isije ikaonekana wengi wameamua hata wachache wako ambaao wameungana na wengi kwenye kumpongeza Mheshimiwa Spika, lakini pia kwenye kuhakikisha kwamba hili jambo la Makao Makuu kuwa Dodoma halitaweza kubadilishwa hapo baadaye. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge jambo lingine ninalo tangazo hapa kutoka kwa Katibu wa Bunge, Mheshimiwa Spika ameelekeza kwamba kesho badala ya ile shughuli ambayo ilikuwa imewekwa kwenye zile ratiba tulizonazo kesho siku ya Jumanne tarehe 9 Juni, 2020 itakuwa ni Azimio la Bunge kama ambavyo mtatumiwa hiyo taarifa kwenye *order paper* lakini mwanzoni ilikuwa ni Muswada wa Sheria ya Marekebisho

Sheria Mbalimbali (Na.3) wa mwaka 2020 (*The Written Laws (Miscellaneous) Amendments Bill (No.3), 2020*). Sasa hii ndiyo ilikuwa imetajwa lakini kesho badala ya huu Muswada, huu Muswada utapelekwa Jumatano halafu kesho kutakuwa na Azimio lingine ambalo mtaletewa kwenye taarifa kama ambavyo tumeweka huo utaratibu ambao Mheshimiwa Spika tulikuwa tunampongeza hapa. Kwa hiyo taarifa itakapokuja kwenu kwamba kesho tunajadili nini haitakuwa huu Muswada, Muswada huu utakuwa siku ya Jumatano.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa nane mchana.

*(Saa 12:04 Jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,
Tarehe 9 Juni, 2020, Saa Nane Mchana)*